MWONGOZO WA KUKABILIANA NA UNYANYASAJI KWENYE MAZINGIRA YA SHULE NCHINI TANZANIA

OCTOBER 2017

YALIYOMO

DIBAJI v

UTANGULIZI 1

2.1. Ufafanuzi na dalili za Uonevu 1

2.2. Sababu za uonevu 2

3. Njia nzuri za Tahadhari 3

3.1. Kufikia makubaliano ya pamoja 3

3.1.1. Namna ya kutunga sheria zenu wenyewe 3

3.1.2. Mkataba wa kupambana na Uonevu 4

3.1.3. Tuzo na adhabu zilizo wazi 6

3.2. Jinsi ya kuandaa somo 7

3.2.1. Kuanza Mada mpya 7

3.2.2. Uwezekano mwingine wa kuendesha somo 8

3.2.3. Kazi ya Vikundi/Jamii 8

3.2.4. Mazoezi ya darasani: 9

3.4. Mijadala ya mara kwa mara 13

3.5. Mazoezi na shughuli 16

4. Kuingilia kati kwenye Vurugu za wanafunzi 16

4.1. Orodha: Je, huu ni uonevu kweli? 17

4.2. Mbinu ya „Bila Lawama“. 19

4.3. Mbinu ya Kasi 20

4.4. Mbinu dhidi ya Uonevu – “Olweus” 23

IBARA YA TATU 28

KUZUIA VURUGU 28

Somo la darasani 28

Somo zuri 29

Kazi za vikundi na kujifunza kwa ushirika 31

IBARA YA NNE 36
ULIMWENGU MWEMA 43
IBARA YA TANO 59
HAKI ZA WATOTO 59
Utangulizi: 60
Maadalizi ya mwisho na Tathmini: 60
Ilani kwa mwendesha mjadala: 61
Njia nyingine: 61
Mapendekezo ya kazi ya baadaye 61
Mawazo ya utendaji 62
Maelezo ya ziada 62
Karatasi ya kazi 62
KITUO CHA NGUVU ZA UMEME 65
Maandalizi ya mwisho na Tathmini 67
Ushauri kwa kiongozi wa Mjadala 68
Mapendekezo ya kazi ya baadaye 68
Mawazo ya Utendaji 68
Utangulizi: 70
IBARA YA SITA 71
BUSTANI YA MBOGAMBOGA 71
Utangulizi: 72
Ushauri kwa kiongozi wa Mjadala 74
Mapendekezo ya kazi ya baadaye 75
Mawazo ya Utendaji 75
Kumbukumbu: 75
Ushauri kwa kiongozi wa Mjadala 75
Njia nyingine 76
Mapendekezo ya kazi ya baadaye 76

Mawazo ya Utendaji 76
HAKI – Bingo! 77
Utangulizi: 77
Mazungumzo na Tathmini 78
Ushauri kwa kiongozi wa Mjadala 78
Mapendekezo ya kazi ya baadaye 78
KICHWA CHA HABARI 80
Utangulizi: 81
Maandalizi ya mwisho na Tathmini 82
Ushauri kwa kiongozi wa Mjadala 82
Njia nyingine 83
Mapendekezo ya kazi ya baadaye 84
Mawazo ya Utendaji 84
Taarifa nyingine 84
IBARA YA SABA 86
MAISHA YETU YA BAADAYE 86
Utangulizi: 87
Maandalizi ya mwisho na Tathmini 87
Maoni kwa kiongozi wa mjadala 88
Tarehe muhimu: 88
Njia nyingine: 88
Mapendekezo ya kazi ya baadaye: 89
Mawazo ya Utendaji 89
MIMI NI NANI? 90
Utangulizi: 90
Maandalizi ya mwisho na Tathmini: 91
Maoni kwa kiongozi wa mjadala 91
Mapendekezo ya kazi ya baadaye: 93

JE NCHI YA USAWA INAELEKEA WAPI? 94
Utangulizi: 95
Maandalizi ya mwisho na Tathmini: 95
Maoni kwa kiongozi wa mjadala 96
Tarehe muhimu 96
Mapendekezo ya kazi ya baadaye 96
Mawazo ya Utendaji 96
Habari zaidi: 96
UPATIKANAJI WA DAWA 99
Utangulizi: Zoezi hili lina sehemu mbili 99
Maandalizi ya mwisho na Tathmini: 101
Maoni kwa kiongozi wa mjadala 101
Mapendekezo ya kazi ya baadaye 101
Mawazo ya Utendaji 102
Kalenda ya Haki za Binadamu 102
Kalenda ya Haki za Binadamu 103
Ufafanuzi wa Mpango wa Utekelezaji 108
Jaribu kufuata hatua hizi nne na kundi lako: 108
Maswali ya haraka na mada ya Haki za Binadamu 109
Kuthibiti Malengo 110
Kujipanga binafsi 111
Viungo mbalimbali kwenye Mtandao kuhusu Elimu ya Haki za Binadamu 114
Viungo mbalimbali kwenye Mtandao kuhusu Elimu ya Haki za Binadamu 115

DIBAJI

Walimu wapendwa!

Tunayo furaha kubwa, kuwasilisha kwenu leo mwongozo huu juu ya Elimu ya Haki za Binadamu na jinsi ya kupambana na unyanyasaji shuleni. Ndani yake kuna mazoezi mengi ya vitendo ambayo yanaweza kutumika darasani na kwenye vikundi mbalimbali vya watoto na vijana. Ni matumaini yetu kwamba mwongozo huu utawasaidia kwa ushauri na vitendo ili kufanikisha masomo yenu mfundishayo.

Mwongozo huu ni matokeo ya kazi za vitendo mashuleni na kwenye makundi ya vijana duniani kote. Siyo tu kwamba unaweza kutumiwa na walimu mashuleni bali pia kwenye makundi ya vijana nje ya shule.

Kwa nini mwongozo huu ulitungwa?

Kufuatana na Mkataba wa Haki za watoto, kila mtoto mwenye umri wa miaka 0-18 anayo haki ya kulindwa kutokana na ukatili wa kimwili na kiakili. Jumla ya makala kumi na moja za Mkataba wa Haki za watoto zinaeleza kwamba ni lazima watoto walindwe kutokana na ukatili na unyanyasaji wa aina yeyote. Sababu ya kutungwa kwa mwongozo huu ni kwamba watoto wengi na vijana duniani kote wanaathirika kutokana na unyanyasaji unaofanywa na watu wazima, pamoja na ule wanaofanyiana wenyewe kwa wenyewe. Ukatili na unyanyasaji siyo tu vitendo vya kushambuliwa kimwili na kupigwa bali pia ni vitendo vya kinidhamu vitumiwavyo na walimu shuleni kama adhabu kali zinazowafedhehesha na kuwadhalilisha wanafunzi. Kadhalika inajumuisha pia vitendo visivyotakiwa kama maswala ya kujihusisha na mapenzi na kugusagusa mtu bila hiari yake. Pia kutokana na ghasia za kiakili kama vile kunyanyasa na matusi ya kukebehi, humfanya mtu asiwe na maisha mema yenye furaha.

Watu wengi wana matumaini kwamba shuleni ni mahali ambapo watoto na vijana wetu watakuwa katika hali ya usalama. Bahati mbaya, vurugu zimeenea sana hasa katika mazingira ya shuleni. Utafiti uliofanyika duniani kote miongoni mwa wanafunzi unaonyesha kwamba watoto wengi huteseka sana kutokana na uonevu na unyanyasaji baina ya wanafunzi. Kadhalika vitendo vya uonevu vifanywavyo na walimu ambapo husababisha madhara makubwa ya kimwili na kiakili kwa wanafunzi. Wanafunzi wengi duniani huogopa kwenda shuleni kwa sababu wanajikuta wakikabiliwa na misukusuko tajwa hapo juu kutoka kwa walimu wao lakini pia na wanafunzi wenzao. Kwa ujumla hali hii huathiri kujifunza kwao. Utekelezaji wa mwongozo huu utapelekea hali nzuri shuleni kwa wanafunzi sio tu kunufaika na ujuzi wanaoupata darasani bali watajijengea uwezo wa kutumia ujuzi huo kwa vitendo "competence" pamoja na kuleta maisha mazuri shulenina yenye kuleta maendeleo yenye tija katika taifa na kimataifa. Hii itakuwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo endelevu wakimataifa (Sustainability development goals Four. 2020-2030

Madhumuni ya Mwongozo huu

Unyanyasaji na ukatili ni vitendo ambavyo havikubaliki duniani kote. Kwahiyo kumekuwa na hatua kadhaa zinazochukuliwa ili kupambana na vitendo hivyo shuleni. Ni muhimu sana

kuweka miundo mbinu kanuni na sheria zilizo wazi kuwa ni marufuku kupiga na kunyanyasa watoto, vijana au mtu yeyote.

Hata hivyo kukosekana kwa adhabu na viboko hakuleti moja kwa moja hali nzuri shuleni, haki za binadamu wala mazingira bora ya kuishi. Hivyo swali muhimu la kujiuliza ni, Je kitu gani kifanyike ili kuweza kujenga hali nzuri darasani? Wewe mwalimu pamoja na wanafunzi wako ndio wahusika wakubwa katika kazi hii ya pamoja darasani ili kupata majibu ya swali hili.

Lengo la mwongozo huu ni kujenga mazoezi ya vitendo vinavyohusu haki za Binadamu, Haki za watoto na jinsi ya kukabiliana na vitendo vibaya. Kuna vitabu vingi na maandishi mengi yanayoeleza kisayansi nini maana unyanyasaji na ukatili, haki za binadamu na jinsi migogoro inavyotokea shuleni. Swali la msingi la kujiuliza ni jinsi gani migogoro hii inaweza kutatuliwa? Ni jinsi gani ya kuleta uelewano miongoni mwa watu? Na vipi hali ya urafiki na ushirikiano wa pamoja unaweza kufikiwa? Mwongozo huu unawaletea mambo muhimu yanayohusiana na mazoezi ya kawaida ya kila siku. Mazoezi ambayo yanaweza kufanywa kwa urahisi shuleni au kwenye kikundi chochote na yasiyohitaji maandalizi makubwa wala vifaa vilivyo ghali.

Jinsi mwongozo huu ulivyoandaliwa

Leo tunawapeni kitabu hiki mkononi chenye mazoezi ambayo yameandaliwa na watu mbalimbali toka nchi kadhaa duniani. Baadhi ya mazoezi haya yamechukuliwa toka kitabu kiitwacho „Campass“, Mwongozo wa kwanza wa Shirika la Haki za Binadamu kwa watoto na vijana wa Baraza la Ulaya (COMPASS – A Manual on Human Rights Education withYoung People). Mapendekezo mengine yanatokana na mafanikio makubwa ya tathmini juu ya mpango wa kupambana na unyanyasaji na ukatili. Kwa mfano „No Blame Approach“ (Mbinu ya Bila Lawama), ya Wanasayansi George Robinson na Barbara Maines, au „Faustlos“ (Mbinu ya Bila Ngumi), ya kituo cha kuzuia Maafa cha Heidelberg nchini Ujerumani. Mazoezi haya yanaweza kutumika popote pale duniani na wala si nchi moja tu. Mazoezi haya yamefanyiwa majaribio kwenye shule nyingi na vikundi mbalimbali na kuthibitishwa kuwa yanafaa kwenye matumizi ya kila siku.

Kwa kuwa hadi sasa mazoezi mengi yameandikwa katika lugha ya Kiingereza, tumejitahidi kutafsiri kwenye lugha ya Kiswahili ili yaweze kuanza kutumika mara moja. Tungependa kutoa shukrani zetu za dhati kwa Dr. Andreas Wesselnmann, Dr. Isack Majura wa Ujerumani, Sr. Felista Tangi wa Chuo Kikuu cha St. Augustine, Mwanza pamoja na wanafunzi wa chuo kikuu hicho.

Kwenye mwongozo huu tumechagua mazoezi mbalimbali toka sehemu kadhaa na mada mbalimbali. Mwanzoni mwa kitabu hiki tumetoa mwanga wa kutosha juu ya kuleta ushirikiano mzuri darasani, kujifunza kwa pamoja na kuishi kwa amani shuleni. Hapa mtaweza kupata mbinu kadhaa za kutumia darasani.

Mwishoni kuna mazoezi mbalimbali juu ya unyanyasaji na ukatili, uonevu, kujilinda dhidi ya ukatili, ubaguzi na kutengwa, usawa wa jinsia, Haki za Watoto na Binadamu kwa ujumla.

Jinsi ya kutumia Mwongozo huu

Tutafurahi sana kama mtavinjari na kupitia mwongozo huu na kuona kama mazoezi yaliyoonyeshwa ndani yatanufaisha masomo yenu. Haikukusudiwa kuwa mazoezi yote yafanywe kwa mfululizo. La hasha! Mazoezi haya yanaweza kutumika pale ambapo mada fulani inaweza kuzungumziwa na wanafunzi au kikundi chochote shuleni. Mazoezi haya husaidia kuhamasisha ushirikiano wa kujifunza pamoja na kubadilishana mawazo baina ya wanafunzi.

Mnaweza kutumia mazoezi haya kwa kadri ya ratiba ya shule yenu ili kuweka kundi pamoja, au pale mnapotaka kuongelea mada fulani. Ingekuwa vizuri zaidi kama mtatumia mwongozo huu mara kwa mara ili mchakato huu wa kujifunza vizuri uweze kufanikiwa.

Sasa tunakutakieni kazi njema na mafanikio mazuri kwa kutumia mwongozo huu.

Vechta, September 2016

UTANGULIZI

2.1. Ufafanuzi na dalili za Uonevu

„Uonevu ni msemo wenye chimbuko lake toka lugha ya Kiingereza linalomaanisha „kundi la watu“, kumkandamiza mtu au kumdhihaki. Uonevu ni kitendo ambacho mwanasayansi aitwaye (Kaspar 2000b, S. 17) anaeleza kama „Vita ndogo“. Ukatili huu unajumuisha k.m. wizi, uharibifu na ufichaji wa mali, udhalilishaji, kusukuma mtu, kueneza uongo, matusi, kumzomea, kumcheka mtu, kumtenga mtu kwenye kundi fulani na ku**mb**ughudhi mtu. Kumlazimisha mtu kutenda jambo asilopenda kulitenda, inawezekana pia vurugu hizi zikasababisha hata ugomvi na kupigana.

Hata hivyo si kila ugomvi kati ya wanafunzi daima uwe uonevu. Hapa ni lazima iwe wazi kutofautisha kati ya mzozo wa kawaida na „uonevu“, kwani „sera ya kuzuia uonevu“ haifai kutumika kumaliza ugomvi wa kawaida. „Uonevu“ mara nyingi hutokea panapokuwa na nguvu zisizolingana kati ya mwonevu na anayeonewa, yaani mwathiri na mwathirika. Hii inaweza kuwa umbile la kimwili wa huyo mwonevu au pia washiriki wengine ambao kwa vitendo vyao humpa nguvu huyo mtenda maovu. (1)

Mara nyingi uonevu hutokea katika mazingara yanayo muhifadhi na kumlinda huyo mwonevu au kumpa mori wa kutenda maovu yake. Katika hali hii ya kutambulika kijamii, kila unyanyasaji utendwao dhidi ya mwathirika, basi huwa ni uthibitisho wa kutambulika kwake na hivyo kuendelea na vitendo vyake vya uovu. (2)

Jambo jingine la muhimu linalotofautisha "Uonevu“ na mizozo ya kawaida baina ya wanafunzi ni muda na marudio ya vitendo hivyo vya uonevu na mizozo hiyo. Mara nyingi mzozo wa kawaida huisha baada ya muda mfupi ambapo wanafunzi hupatana au hujaribu kuepukana na kila mmoja kwenda njia yake. Ikiwa vitendo vya kufedhehesha dhidi ya mwathiriwa vitatokea zaidi ya mara moja kwa wiki na hali hii kuendelea kwa kipindi kirefu zaidi ya wiki au miezi, basi hali hii inaweza kutafsiriwa kama ni „Uonevu“.Dalili ya mwisho ya uonevu ni ukweli kwamba mwathirika hawezi kujikwamua mwenyewe kutoka katika hali hii. Aidha mwathirika hawezi kuchukua hatua zozote dhidi ya uonevu huu kwa ajili ya hofu juu ya unyanyasaji na athari zinazoweza kumtokea, au majaribio yake yote ya nyuma yameshindikana kwani huyo mwonevu hakuonyesha dalili yoyote ya kujirudi.

Kwa kifupi unatakiwa kuwa makini kabla ya kutatua suala la uonevu kati ya wanafunzi. Vifuatavyo ni viashiria vya uonevu. Ili uwe ni uonevu:

I. Kuwe kuna nguvu zisizolingana baina ya wanafunzi,
II. Maovu haya yawe yanatokea zaidi ya mara moja kwa wiki,
III. Migogoro hii iwe imedumu kwa kipindi kirefu cha wiki kadhaa,
IV. Mwathirika awe hawezi kujikwamua mwenyewe kutoka kwenye athari hizi.

Uonevu unaweza kuelezwa kuwa ni vitendo ambavyo hutokea mara kwa mara kwa kipindi kirefu, ambapo mtu mwenye nguvu hujaribu kumdhuru yule mdhaifu. Mateso hayo huwa ni makubwa kiasi ambacho hata tabia na mwenendo wa mwathirika hubadilika (3). Kwa taarifa zaidi angalia sura ya 1.3.3.)

Suala la muhimu, ni vizuri kumuuliza mwathirika kwa utulivu na bila kuonwa na yeyote, anavyojisikia. Mwathirika anajua kabisa hali yake ya mateso ilivyo, na anajua kabisa kama ni ugomvi wa kawaida tu baina ya wanafunzi au uonezi.Wewe kama mwalimu ikiwa huna uhakika kama migogoro hiyo ni uonevu hasa, basi unaweza kuangalia tena kifungu cha 3.1.

Inapaswa kuzingatiwa kuwa Uonevu siyo kwamba hufanyika tu baina ya wanafunzi peke yao, bali pia hata walimu wanaweza kuwa washiriki au waonevu wenyewe, mara nyingi bila kujijua. Hii hutokea pale ambapo mwalimu huvumilia uonevu miongoni mwa wanafunzi na hivyo kumpa nafasi huyo mwonevu kuendelea kutenda maovu yake. Inapotokea mwalimu kutoa kauli kama ya yule mwonevu kwa kuridhika na vitendo hivyo kwa kauli zifuatazo: (k.m. “ kwa kweli ni mtu wa ajabu na mgumu,. Naweza kuwaelewa wanafunzikama hawamtaki katika kundi lao”), basi mwalimu huyo anasahau mateso anayoyapata mwathirika na hivyo kujiepusha na utafiti wa jawabu kwamba mwathirika hawezi kujikwamua mwenyewe (4). Lakini pia adhabu zitolewazo mbele ya darasa pamoja na matusi ya hadhara yanaweza kukera sana na kumuumiza mwanafunzi. “Kutokuelewa hakuhesabiwi kama ni kosa au kusahau, bali ni kama aibu inayostahili kukomeshwa (5).

Maneno kama vile “we mpumbavu,huwezi kufikiri!”, huwafanya wanafunzi kuiga tabia ya mwalimu wao. Yeye ni mfano wa kuigwa, kwani watoto huchukulia kwamba yale yafanywayo na watu wazima ni sahihi hasa walimu. Tafakari tabia yako mwenyewe, na jiulize ni wakati gani utawaumbua hadharani wanafunzi wako. Katika sura ya 4. nitaonyesha njia nyingine za kutumia (6).

2.2. Sababu za uonevu

Awali ya yote ni muhimu ielezwe wazi kuwa hakuna sababu moja tu maalumu ya uonevu, bali kuna sababu kadhaa zinazohusiana na kusababisha suala hili. Uonevu unatokana na sababu mbalimbali zinazoingiliana na hatimaye kusababisha ukatili baina ya mtu na mtu mwingine kwa kipindi cha muda mrefu. (7). Ni dhahiri kuwa migogoro na tabia mbovu hujitokeza taratibu kwa sababu kadhaa, ambapo mtu binafsi, familia, kundi la rika moja, shule na jamii kwa ujumla ziko kwenye uhusiano wa aina Fulani (8).

Baadhi ya sababu hizo ni bora zitajwe (zimetajwa) hapa ili ieleweke vizuri kuwa hata huyo mwonevu mara nyingi huwa ni mwathirika aliyewahi kupatwa na janga hilo. Utakuta waonevu wengi wamekwisha shuhudia wenyewe maovu hayo katika mazingira yao na hasa kwenye familia zao. Hapa mbinu ya kujifunza kwa kutumia taaluma ya Mwanasayansi Albert Bandura inaweza kutumika ielezayo kuwa watoto hujifunza kwa kuiga mifano ya walezi wao. “Kufuatana na Bandura (1969), taaluma hii ya kujifunza inatumika pale ambapo mtu anaiga tabia ya mtu mwingine na hivyo kuanza tabia mpya au kubadili tabia yake ya awali (9).

Wamejifunza kwamba udhaifu, - hususani hapa ni vijana wadogo – hutendewa maovu na wazazi wao, na kudhani kwamba hii ndiyo njia sahihi ya kuleta suluhu. Mara nyingi watoto hawa hawajui njia nyingine ya kutatua matatizo ili kuleta suluhu. Waonevu hawa yawezekana hawakupata maadili mema au kuwekewa mipaka adilifu na wazazi wao na hivyo kuiga tabia mbaya ya walezi wao (10).

3. Njia nzuri za Tahadhari

Katika surahii napenda kufafanua baadhi ya hatua na mazoezi ambayo yanaweza kuboresha hali nzuri ya darasani. Husaidia kuleta mawasiliano mema kati ya wanafunzi wenyewe na pia baina ya mwalimu na wanafuzi wake. Aidha baadhi ya mazoezi haya yana lengo la kuimarisha imani ya kujiamini kati ya wahalifu na waathirika. Imani ndogo ya kujiamini mara nyingi huwa ndiyo sababu na chimbuko la uonevu na migogoro, jambo ambalo linapaswa kukabiliwavizuri.

Muda ambao unautumia katika juhudi hizi, utazaa matunda hapo baadaye. Ukiwepo uelewano mzuri kati yao, basi wanafunzi wanaweza kuzingatia vizuri yale wanayofundishwa na hivyo wewe kama mwalimu kutumia muda mchache ili kusuluhisha ugomvi na kutoa adhabu. Kadhalika wewe mwalimu utanufaika kutokana na hali hiyo tulivu, wasiwasi mdogo na vurugu chache na hivyo kujiamini kwa matendo yako mwenyewe (11).

3.1. Kufikia makubaliano ya pamoja

Hatua ya kwanza inayobidi kufanywa ni kuweka wazi tabia ya pamoja na sheria zitakazokubalika kwa darasa zima. Hapa kuna uwezekano wa aina mbili:- Unaweza kuafikiana na darasa zima kwa pamoja juu ya sheria zitakazofuatwa au tumia ule mkataba wa Uonevu. Ndani yake kuna uwezekano wa kutunga orodha ya kanuni hizo. Tumia muda wa kutosha kama saa moja kwa kila kipengele.

3.1.1. Namna ya kutunga sheria zenu wenyewe

- Waeleze wanafunzi wako kuwa wakae kwenye duara, ili waweze kuonana wakati wa maongezi. Hii inajenga hali nzuri ya mazingira ambayo itakuwa rahisi wakati wa majadiliano ya pamoja.
- Sasa waambie wanafunzi wako kuwa wanapaswa kufikiria ni hali ipi ya mienendo) wanayoipenda itawale darasani. Jaribu kuorodhesha yale yaliyo mazuri, k.m. “nawaomba mfikirie kwa ufupi, ni matakwa yapi ya mwenendo mzuri munaopenda katika darasa letu na ni yapi hamyapendi. Tungependa kwa pamoja tujiwekee mkataba wa sheria (e) za kufuatwa na kila mmoja wetu, ili sote hapa tujisikie vizuri”. Wape wanafunzi muda wa dakika 2 ili waweze kufikiria.
- Chora ubaoni kielelezo chenye sehemu mbili, ambapo kila mmoja utajaza, “mimi ninachopenda” na “mimi nisichopenda”

Hapa ni mfano wa kielelezo hicho:

Mimi ninachokipenda **Mimi nisichokipenda**

Ninachopenda: Kwamba tunyooshe mkono Tunapotaka kutoa hoja	**Nisichopenda:** Kwamba tusimwite mtu yeyote Mpumbavu / mjinga
Tunapaswa kusema daima Tafadhali na asante	Sipendi wanafunzi wengine Waje wamechelewa
Tuwasaidie wenzetu wanaposhindwa kujibu maswali darasani	Tusiwacheke wenzetu wanapo toa majibu yasiyosahihi darasani
Tunapaswa kuepuka tabia za wizi darasani	Sipendi wanafunzi wengine kuwaibia wenzao vitu
Na mengine mengi...	

Sasa kusanya mawazo mengi, bila kutoa maoni juu ya mapendekezo hayo yaliyotajwa. Andika hivyo hivyo jinsi wanafunzi walivyotoa mapendekezo yao; kwani hii inajenga mshikamano wa sheria hizi. Mara tu mwalimu akianza kusahihisha majibu, basi sheria hizo hupoteza ule uhusiano wake na wanafunzi wenyewe.

- Sasa waruhusu wanafunzi wahamishe sheria hizo kwenye bango kubwa na kuzitundika darasani mahali pazuri zinapoonekana kwa wote. Ni bora wale wanafunzi ambao walikuwa hawajachangia chochote katika mzunguko huo wakaziandike sheria hizo ubaoni.
  Wanafunzi hawa wanaweza kuandika mapendekezo mengine ubaoni bila kubughudhiwa.

- Mara wanafunzi waendapo kinyume na kuvunja sharia hizi, unaweza kuashiria na kuwakumbusha juu yayale waliyoandika kwenye bango hilo na kuwataka wasome tena kwa sauti. Kwa kufanya hivyo basi sheria hizi zinaweza kuhifadhiwa daima (12).

3.1.2. Mkataba wa kupambana na Uonevu

Mkataba wa kupambana na uonevu unaweza kutumika kwenye shule nzima na hata kwenye darasa moja moja. Hii inahusu sheria kadhaa ambazo zitawezesha kudumisha hali ya nidhamu na amani darasani.

- Tengeneza mduara kama ilivyoelezwa katika ibara 3.1.1.
- Tundika bango linaloweza kusomeka vizuri darasani la mkataba wa kupambana na uonevu na acha nafasi ya kutosha kuweka sahihi. Unaweza kuwapa nakala wanafunzi ili waweze kusoma sheria hizo baada ya masomo.
- Sasa unaweza kumruhusu kila mwanafunzi kusoma sheria hizo kwa hiari yake
- Baada ya kila sheria kusomwa, uliza wanafunzi, „Tafadhali nitajie mfano halisi“. Kwa kila kanuni chagua mwanafunzi mmoja hadi wawili ili waelezee hiyo kanuni jinsi walivyoielewa na kuitafakari kwa uelewa wao wenyewe. Usitoe maoni au

mapendekezo yoyote, kwani wanafunzi wanakuwa na uhusia no wa karibu na kuzielewa sheria na kanuni walizojiwekea wenyewe katika lugha yao wanayoilewa wenyewe.

- Baada ya hapo kila mwanafunzi aweke sahihi yake katika bango hilo, ili kukubali sheria hizi.
- Hapa pia endapo sheria hizo zitavunjwa, unaweza kumtaka mwanafunzi huyo asome sheria hizo kwa sauti ili kanuni hizo zisije kusahaulika (13).

Kigezo:

Kukabili Uonevu na Unyanyasaji – Azimio la Ushirikiano mwema

Mkataba wa kupambana na Uonevu

Uonevu:

- Hulenga kwa madhumuni ya kumdhuru mwingine
- Unajumuisha aina yoyote ile ya kuleta vurugu na chuki (matusi, kimwili na dhidi ya vitu/vifaa
- Unafanyika kwa marudio na kwa kipindi cha muda mrefu
- Umekithiri kwa uwiano wa nguvu zisizolingana – yaani wengi dhidi ya mtu mmoja
- Unadhihirika katika makundi yote (shuleni, klabu, kazini, n.k.)
- Mwathirika hujikuta hana njia au nafasi yoyote ya kujinusuru mwenyewe kutoka katika hali hiyo.

Kwenye shule yetu Uonevu hauna nafasi. Ndiyo maana tunaahidi kwa pamoja kuzingatia yafuatayo kwenye Mkataba huu wa kupambana na Uonevu!

1. Tunaheshimu kwa maneno na vitendo hadhi ya binadamu wenzetu
2. Tunamsaidia yeyote ambaye anahitaji msaada dhidi ya unyanyasaji, kama vile chuki, kutengwa, matusi au madhara ya kimwili
3. Tunamuunga mkono na kumsaidia kwa pamoja yule anayeonewa, hata kama hatukubaliani na mawazo yake
4. Tunataka kujifunza juu ya uvumilivu na heshima, pale ambapo dalili za uonevu zinaanza kujitokeza.
5. Tunapambana na makosa yawengine kama yetu wenyewe
6. Hatuenezi uvumi wowote.Kimsingi hatumsemi mtu, bali tunaongea naye
7. Tunatoa wito, kuwa hatutamnyanyasa mtu yeyote – yaani kumtenga, kumuudhi, kumtishia au kumkebehi – na tunaahidi kumlinda aliye mdhaifu
8. Tunapenda kujitahidi kushirikiana na kila mtu hapa shuleni kwa heshima na taadhima
9. Pale tusipoafikiana kimawazo hatutengani, bali tunatafuta ufumbuzi kwa pamoja
10. Tunashirikiana kwa pamoja badala ya kutengana/kumtenga mtu yeyote kwa hali yoyote aliyonayo kiuchumi au uwezo wa darasani.

3.1.3. Tuzo na adhabu zilizo wazi

Kama mwalimu mara nyingi ni vigumu kufuatana na idadi kubwa ya wanafunzi, kubaini kila kosa alifanyalo mwanafunzi. Ili kupata uwazi zaidi, wewe mwalimu nawanafunzi wako, mfumo wa kutoa tuzo na adhabu unaweza kusaidia sana. Tumia muda wa kama dakika 15 hivi, ili kuwaelezavizuri wanafunzi wako.

- Tundika bango kwenye ukuta,likiwa na kielelezo chenye sehemu mbili. Mfano:

Umefanya vizuri, hivyo utalipwa	Umefanya usumbufu, hivyo utapewa adhabu
• Wengi wameshirikiana vizuri • Leo kumekuwa kimya darasani • Wanafunzi wote wamefanya kazi za nyumbani	• Zaidi ya wanafunzi 5 hawakufanya kazi za nyumbani • Leo wanafunzi wengi wamepiga kelele darasani • Leo mwanafunzi mmoja amesukumwa na kutukanwa

- Baada ya kila somo, unaweza sasa kuandika hadharani kwenye ubao ili wanafunzi wote waweze kusoma yale mazuri yaliyowapendeza na yale mabaya ambayo hayakuwapendeza. Ukiukaji wa kanuni za kawaida unaweza pia kuorodheshwa hapa, na pia pale wanafunzi wanapoonyesha urafiki baina yao.
- Wanafunzi hujifunza kupitia orodha hii ya wazi, kuwa tabia yao ina athari moja kwa moja na hivyo hawawezi kusahau haraka. Kila mwanafunzi anachukua dhamana na kuwajibika binafsi kwa tuzo na adhabu zitakazotolewa.
- Unaweza sasa kuandika hadharani adhabu na tuzo hizo, hii hujenga uwazi zaidi na hivyo wanafunzi hujifunza kudhibiti vitendo vyao na wewe kukuamini.
  Mfano:

X 10	Kazi ya nyumbani (homework) katika somo fulani inakosekana; matembezi madogo, mjadala ambao wanafunzi wenyewe wameuchagua unajadiliwa darasani, mchezo wa pamoja unaweza kuchezwa
X 10	Kazi ya nyumbani ya ziada (homework), somo la ziada; kufuta ubao na kufanya usafi darasani kwa wanafunzi wanaofanya usumbufu, kusafisha mazingira ya shule kwa wanafunzi wanaofanya usumbufu.

- Ni wangapi watatunukiwa au wataadhibiwa, hiyo unaweza kuamua mwenyewe, lakini unapaswa kuwa mwangalifu. Juu ya tuzo acha wanafunzi waamue wenyewe ni tuzo au zawadi gani wangependa. Unaweza pia kutoa mapendekezo mengine. Juu ya adhabu, hapa chagua mwenyewe. Kwa kufanya hivyo wanafunzi hujifunza kwamba wanapoonyesha tabia njema wanapewa haki zaidi ya kushiriki, lakini wakionyesha tabia mbaya basi watapewa haki ndogo (14).

3.2. Jinsi ya kuandaa somo

Moja ya sababu za vurugu darasani na uonevu miongoni mwa wanafunzi, ni somo ambalo halitoi changamoto ya kutosha kwa wanafunzi na haliwanufaishi kama ipasavyo. Kwa ajili hiyo ndiyo maana kunatokea hali ya kuzubaa bila kujua la kufanya na hivyo kusababisha vitendo vingine ambavyo vinawafurahisha, kama kuwaudhi wenzao, jambo ambalo lingeweza kuepukika. Kadhalika hali hii inaweza kumfanya mwalimu achanganyikiwe na kukata tamaa, kwani somo linalochokesha kiasi hiki linasababisha usumbufu mkubwa na kupoteza nguvu bure. Ili kukabiliana na matatizo ya namna hii inashauriwa kuliandaa somo vizuri kiasi ambacho wanafunzi watashirikishwa kikamilifu na kuwa wasikivu. Hivyo huwa hakuna muda wa kupoteza kutokana na tabia zisizokubalika (15).

Hapa chini tungependa kukupa baadhi ya motisha, ambayo mabadiliko madogo yasiyochukua muda mwingi yanaweza kuzaa matunda mazuri na kufanikisha somo lako.

3.2.1. Kuanza Mada mpya

Maelezo ya awali: mwanzoni mwa somo la kwanza katika nusu mwaka, unaweza kuwaeleza wanafunzi wako, ni mada zipi zitafundishwa na matokeo yapi yanategemewa kufikiwa. Kadhalika ni vipi watatahiniwa. Hii pia inaweza kuwa mwanzoni mwa somo jipya kwa sentensi fupi fupi ili wanafunzi waweze kujiandaa kwa baadaye (16).

Mawazo ya awali: Njia nyingine ya kuanza mada ni kutaka mawazo ya awali. Andika ubaoni maneno ya muhimu kwa herufi kubwa. Sasa wanafunzi wanaweza kunyoosha mikono na kutaja maneno muhimu, ambayo utayaandika kwa kuzunguka neno hilo. Unaweza kuwataka wanafunzi kila mmoja kwa hiari yake kuandika neno lake ubaoni. Baadaye maneno hayo yanaweza kuchambuliwa au kujadiliwa kwa pamoja. Wewe kama mwalimu unaweza kutambua kiwango walichofikia wanafunzi wako na wapi uongezee taaluma yako. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi hujifunza dhana ya kwanza ya kimsingi na kuhusisha uzoefu wao wenyewe na mada hiyo.

Kutoa mifano: Unapoanza mada mpya, kutegemeana na somo lenyewe, unaweza kuanza na hadithi ndogo, kuimba juu ya mada hiyo au kuigiza jambo fulani. Hata mazoezi magumu ambayo wanafunzi watapewa baadaye unaweza kuyaeleza kwanza kwa urahisi, kwa mfano jaribio la Fizikia au zoezi jipya la Hesabati (17).

3.2.2. Uwezekano mwingine wa kuendesha somo

- Kuuliza maswali: Kuuliza maswali wakati wa somo likiendelea huwafanya wanafunzi kuwa makini na kuweza kufuatilia mada inayozungumziwa. Unaweza kuwataka wanafunzi wataje kwa mukhtasari yale waliyojifunza katika somo lililopita na pia kuuliza maswali juu ya mada hiyo. Pia kwa kazi ya nyumbani unaweza kuuliza maswali ya hadhara bila wanafunzi kujua nani ataulizwa. Kwa kufanya hivi utaweza kuamsha motisha yao kwa kusikiliza na kujitayarisha vizuri ili wasije kujiaibisha (18).

- **Kuonyesha mfano:** Unaweza kuleta vitu vya kuonyesha kama mfano darasani ili wanafunzi waweze kuviona. Kulingana na somo lenyewe unaweza kutumia njia tofauti. Mfano: Kwenye Hisabati kupima eneo/ukubwa wa mpira. Kwa Kiingereza – matumizi ya vyombo vya nyumbani.

- **Kutafakari Vifungu:** Wape wanafunzi kifungu cha maelezo kuhusu mada fulani. Kazi ya wanafunzi ni kusoma na kutafakari yale yaliyomo na kunukuu yale ya muhimu. Waulize maswali ya muhimu kama insha ambayo wataulizwa kwenye somo hilo au kwenye mukhtasari wa yale waliyosoma. Kwa njia hii wanafunzi hujifunza kwa kujitegemea wenyewe.

- **Kunukuu Mada muhimu:** Ili kuhifadhi mada nayale ya muhimu kwenye somo fulani, zipo mbinu kadhaa za kufuata:- Kwa mfano kuanzisha daftari la kumbukumbu ambalo kila saa pananukuliwa yale ya muhimu yaliyotajwa darasani. Daftari hili la kumbukumbu linaweza kuazimwa na mwanafunzi anayetaka kusoma jambo fulani au yule ambaye hakuhudhuria somo lile. Pia kuna uwezekano wa kuandika mukhtasari wa yale ya muhimu tu, au kunukuu taarifa ya muhimu baada ya kila saa moja. Zaidi ya hayo unaweza kuwapa wanafunzi waandike yale ya msingi yanayohusu kila mada iliyogusiwa (19).

3.2.3. Kazi ya Vikundi/Jamii

Kazi zifanyikazo katika vikundi/jamii zinajulikana sana situ kwa faida yake ya kujifunza na kuinua utendaji wa mwanafunzi, bali pia kuboresha mawasiliano mazuri baina ya wanafunzi ambapo migogoro na uonevu vinaweza kuzuilika. Wanafunzi hujifunza kusaidiana wenyewe kwa wenyewe na kuwa wazi baina yao na wengine (20).

- **Majadiliano:** Ili kufanya mazoezi juu ya kuwasiliana vizuri kirafiki na kwa usahihi kati ya wanafunzi, mijadala ya wazi yenye kuongozwa na sheria na kanuni maalumu husaidia sana.Hapa kanuni za pamoja darasani juu ya uhusiano mwema zinaweza kutumika. Uliza swali kuhusu mada fulani na wanafunzi wabadilishane mawazo yao. Endapo mmoja wao atakiuka sheria na kanuni hizo, mweleze moja kwa moja hapo hapo, au uwapongeze wanafunzi wako wanapotumia lugha nzuri. Mwisho zungumzia matokeo ya mukhtasari wa majadiliano. Unaweza kuwataka wanafunzi kufanya mjadala mfupi kama insha kwa ajili ya kumbukumbu yao.

- **Kazi ya vikundi:** Wagawe wanafunzi kwenye vikundi lakini isizidi watu kumi (10) vinavyolingana na kuwapa kazi inayoeleweka. Juu ya ukubwa wa kundi unaweza kuamua mwenyewe kulingana na mada na swali lenyewe. Hapa wanafunzi wanaweza kufanya utafiti toka kwenye kitabu fulani na kufanya mukhtasari au kutafuta ufumbuzi wa swali fulani. Wape muda wa kutosha na wakati huo huo wazungukie darasani, jibu maswali yao au wape msaada pale wanapokuwa na matatizo.

- **Maonyesho ya wanafunzi:** Kutoa daraja kwa kazi ya vikundi ni njia nzuri inayotumika ili kuwasilisha matokeo kwa njia ya pamoja. Hapa wanafunzi hujifunza kujieleza hadharani, jambo ambalo linaweza kusaidia hata kazini ili kukabiliana na woga. Unaweza kuwachagua wanafunzi au wao kujichagua wenyewe. Maonyesho kama hayo yanaweza kuwa ya mwanafunzi mmoja au ya kundi zima. Kadhalika kazi za nyumbani zinaweza kuwasilishwa kwa namna hii au kusahihishwa kwa pamoja.

- **Kazi za nyumbani kuelezwa kwa wengine:** Fikiria uwezekano wa kazi mbali mbali za nyumbani kwa wanafunzi wako na kuzigawanya. Kwa mfano unaweza kutumia mada moja yenye dhana mbili tofauti na kuzigawanya. Sasa wanafunzi kazi yao ni kuwasilisha matokeo yao na kuyaelezea kwa wengine. Hii hujenga mawasiliano baina ya wanafunzi ambao hukutana mara chache na kukuza uhusiano wa kijamii kama kuwasilisha mada zilizo ngumu (21).

3.2.4. Mazoezi ya darasani:

Mazoezi ya darasani wakati wa masomo yenye lengo la kupumzika, hutajwa na wengine kuwa ni kupoteza muda tu. Lakini haya ni mazoezi yenye faida kubwa kwa wanafunzi na mwalimu mwenyewe kwani kutokana na mapumziko haya mafupi ya mazoezi ya kunyoosha viungo, humfanya mwanafunzi kuamka na kuchangamka na hivyo kuwa makini tena darasani. Hivyo wanafunzi huweza kushiriki tena kikamilifu kwenye masomo na hivyo kipindi kwenda haraka. Baada ya kila wiki moja unaweza kutumia zoezi lingine jipya. Hii inaweza kurudiwa kama mara 3-5 na huchukua muda wa dakika 3-4. Bora zaidi ni kufanya zoezi mara moja kwa siku katika kipindi cha 4-5, au pale kipindi kinaporefuka, au inapolazimu wakati wanafunzi wamechoka au inapotokea vurugu yoyote darasani. Hapo unaweza pia kufungua madirisha ili kuruhusu hewa safi iingie ndani. Zungumza na walimu wenzako na kuwaeleza hoja na kanuni hizi.

- **Zoezi "Simama/kaa chini/piga makofi"**

  "1. Mazoezi ya kuchangamsha:

  - - simama, kaa chini (mara nne)
  - - Mchanganyiko: simama, piga makofi, kaa chini, piga makofi, simama, piga makofi……

2. Mazoezi ya kuboresha viungo:

- - piga makofi huku umesimama na kuchuchumaa
- - piga makofi kwenye mapaja yote mawili
- - piga makofi mikononi
- - weka mkono wa kulia kwenye bega la kushoto
- - weka mkono wa kushoto kwenye bega la kulia
- - gusa kwa kidole cha kulia upande wa kushoto
- - gusa kwa kidole cha kushoto upande wa kulia
- - piga makofi mara mbili kwenye mikono.

3. Kutulia: „Mzunguko wa vidole“

- - kunja vidole pamoja, zungusha kidole gumba, kidole cha kati, kidole cha pete…….
  (a) zungusha mwili kwenye mduara, vidole tofauti vigusane
  (b) Zungusha mwili upande mwingine

  Mazoezi ya kupumua: weka viganja kifuani, onyesha vidole juu".

❖ **Zoezi "Kuchuma tunda"**

"1. Mazoezi ya kuchangamsha:

- - Elezea hadithi ndogo juu ya kuchuma matunda: "mmesimama chini ya mti wa matunda. Matunda mnayoweza kuchuma yako juu sana. Simamia vidole vya miguu na jaribu kuchuma matunda kwa mkono wa kulia, halafu kwa mkono wa kushoto. Weka tunda hilo kwenye kikapu kwa kutumia mguu (huku mkichuchumaa chini). – rudia zoezi hili mara nane (8) – kikapu kimejaa!

  Nyongeza: kwa kila rudio, nyoosha juu zaidi mikono yenu. Mara ya mwisho wakati mkichuma matunda, mbwa wawili wadogo wanakuja mbio, huku wakiruka na kuninginia `kwenye suruali/kaptula – kulia na kushoto. Tikisa mguu wa kulia na wa kushoto.

2. Mazoezi ya kuboresha viungo: "Alama ya nane"

(a) kwa kutumia kidole gumba –mkono wa kulia ukiwa

usawa wa macho kinyume cha mwelekeo wa saa – chora alama ya nane (8). Macho yaelekeze kufuata njia ya dole gumba.

(b) kwa kutumia kidole gumba – mkono wa kushoto ukiwausawa wa macho – mwelekeo wa saa

(c) kwa kutumia vidole gumba vyote – kinyume cha mwelekeo wasaa

3. Kutulia:

Kaa kwenye kiti; weka vidole kwenye tumbo

Pumua kwa ndani: kiganja cha mkono kinyooshe juu ya kichwa

Pumua kwa nje: kwa kunyoosha vidole (kiganja cha mkono) kuelekea chini ya tumbo– rudia mara nane (22).

Kama mwalimu unaweza kufikiria mwenyewe mazoezi yako nakuyatumia darasani. Maana na shabaha kubwa ya mazoezi haya ni kuwatoa wanafunzi katika hali ya uchovu ili waweze kuwa makini na kuweza kuzingatia tena darasani. Kwani mazoezi haya huleta furaha na mabadiliko darasani, na hivyo wanafunzi kufurahia zaidi muda wa kuwepo shuleni. Kadhalika muziki unaweza kutumbuiza pia.

Baadhi ya mifano ya mazoezi ya darasani inaonyeshwa kwenye Video zifuatazo:

https://www.youtube.com/watch?v=OKgWaBc6e38

• https://www.youtube.com/watch?v=QIzRGPzHbMk

• https://www.youtube.com/watch?v=pbD7Dcmlmws

• https://www.youtube.com/watch?v=x4FZiWwVgNQ

• https://www.youtube.com/watch?v=5i8rG5rKzkY

• https://www.youtube.com/watch?v=5i8rG5rKzkY

• https://www.youtube.com/watch?v=zxyygDRM7ms

• https://www.youtube.com/watch?v=fgQOGORKG5I

• https://www.youtube.com/watch?v=nZK8n17U3-o

3.3. Sanduku la Maoni (wasiwasi):

Sanduku la maoni au wasiwasi, kama jina linavyosomeka, ni sanduku la maoni ya wanafunzi kuhusu wasiwasi wao. (katika kuanzisha hatua hii tunataka tunataka kujua matatizo yao Kuanzisha hatua hii ni kutaka kujua tu matatizo ya wanafunzi. La muhimu kabisa ni kumlinda mwanafunzi asitajwe jina lake wala kujulikana ni nani. Hii ina maana kwamba sanduku hili litasomwa tu na muhusika ambaye ni mwalimu wa darasa au mwalimu mshauri. Hivyo unahitaji ufunguo ili mtu yeyote asiweze kufungua na kusoma barua hizi. Hata jina la sanduku hili la barua unaweza kushauriana na wanafunzi, ili wawe na uhusiano wa karibu na sanduku hili.

Wanaweza kuwa wanakusanya na kusoma barua hizo mara kwa mara kwa utulivu, na ikiwezekana kila siku. Dhiki na mateso ya mwathirika kutokana na uonevu ni kubwa sana, hivyo inalazimu kuingilia kati haraka iwezekanavyo.Sanduku hili linaweza kutumika si kwaajili ya uonevu tu, bali pia kwa masuala mengine (23). Kwaajili ya kuboresha taaluma na hali nzuri ya kujifunza darasani/shuleni.

- Tumia kama dakika 15 hivi ili kuwaeleza wanafunzi wako faida ya sanduku hili. Kwa mfano: “Sanduku hili litatumika hivi karibuni kuandika ndani ya barua kitu chochote kinachowakera, maoni au matakwa mliyonayo kwangu, au kama kuna mtu mwingine mliyemuudhi au aliyewaudhi lakini mnaogopa kumwambia mtu yeyote. Kila jambo mtakaloandika kwenye sanduku hili litabakia kuwa la siri bila kujulikana ni la nani, na ni mimi tu nitakayelisoma. Halitachapishwa wala kuonyeshwa kwa mtu mwingine. Baadaye nitawajia tena ili tuweze kuzungumzia masuala hayo kwa pamoja, kama mtakavyopenda wenyewe. Hakuna mtu mwingine yeyote atakayejua”. Sisitiza “kutojulikana” kwani hiki ndicho kipengele muhimu katika utumiaji wa sanduku hili.
- Unaweza sasa kuendesha mjadala mfupi na wanafunzi. Waulize: “Ni katika hali ipi mngependa kuandika barua hiyo na kuitumbukiza kwenye sanduku hilo?”Usijadili au kutoa maoni yoyote kuhusu maelezo yao. Kwa kutumia mifano kadhaa inabidi wanafunzi waelewe wazi shabaha halisi ya kutumia sanduku hili: uonevu, unyanyasaji wa ndani, unaposhindwa kupata njia au msaada wowote wa kukutoa kwenye matatizo kama haya, mapendekezo ya masomo darasani au matembezi nje ya shule.
- Sasa kusanya mapendekezo ya wanafunzi wako wapendekeze ni jina lipi lipewe sanduku hili. Wanaweza kupiga kura. Linaweza kuitwa sanduku la maoni, la wasiwasi, la huzuni, la kandamnasi, n.k. Ubunifu hauna mpaka.
- kifuatacho waeleze wanafunzi mahali ambapo sanduku hilo litatundikwa. Hapa pawe mahali ambapo bado hapajatumika, ambao hapaonekani kwa kila mtu pia lifungwe kwa kufuri.
- Kama utapenda mnaweza kwa pamoja na wanafunzi wako mkalifanyia urembo sanduku hilo. Inawezekana likawa la mbao, mkalitengeneza kwa mfano wakati wa kipindi cha Hesabati, ambapo inabidi wafanye vipimo wenyewe au kwenye somo la sanaa au kazi za mikono. Chagua rangi pamoja na wanafunzi ili waweze kulirembesha. Wanafunzi watajifunza kuwa sanduku hili ni lao na linawahudumia wao wenyewe.
- Sasa tundika sanduku hili mahali pake, na ni bora ukiwa na wanafunzi kwa pamoja, ili kila mtu ajue ni wapi limetundikwa. Hapa pawe mahali ambapo hapatumiki mara kwa mara na ambapo hakuna anayeweza kuwaona wanafunzi wanapotumbukiza ndani maoni yao, ili wasione haya au mwanafunzi mwingine kuwasemesha. Kutojulikana kunasaidia kuondoa woga au kueleza wasiwasi wao kunapungua na hivyo kulitumia sanduku hili bila kipingamizi chochote.
- Sasa angalia kwenye sanduku mara moja kila siku, bora kwenye kipindi cha mwisho. Hivyo unaweza kuingilia kati haraka panapotokea dharura yoyote.

3.4. Mijadala ya mara kwa mara

Ni muhimu sana kwa wanafunzi kupata nafasi ya kujadili masuala mbalimbali ambayo pengine yasingeweza kujadiliwa katika somo la kawaida. Mazungumzo kama haya yanaweza kuhusu vurugu na uoenevu shuleni, migogoro ya darasani, kufanya marekebisho ya nakshi darasani, maswali yahusuyo mwalimu, kuandaa matembezi nje ya shule, n.k.

Tumia muda wa kutosha mara kwa mara ili kuwawezesha wanafunzi kufanya mazungumzo haya. Kwa mfano unaweza kupanga mara moja kwa wiki, hata nusu saa baada ya kipindi cha mwisho. Kaeni chini na wanafunzi katika duara/mzunguko, ili uweze kuona kila upande wakati wa mjadala wenu. Mjadala kama huu husaidia kuongeza stadi za kijamii na kusaidia kutunza sheria na nidhamu darasani, na pia kujenga uwazi baina ya wanafunzi. Unaweza pia kujadili matukio yaliyopita, yale yaliyokwenda vizuri na ambayo hayakwenda sawa nabado yanawasumbua. Inapotokea nguvu ya kundi zima kwa kumsema au kumuonya huyo muhusika, basi tabia ya usumbufu na fujo alizokuwa akifanya zinaweza kuepukwa (24).

Majadiliano haya ya darasani unaweza kuyatumia ili kuzungumzia masuala ya uonevu na unyanyasaji. Jadiliana kwa uwazi na wanafunzi wako. Katika mwanzo wa mjadala unapoanza mada mpya unaweza kutumia alama za uonevu, kama ilivyoelezwa katika fungu la 2.1. Baada ya hapo unaweza kuwauliza wanafunzi ni mambo gani wamekumbana nayo katika hali ya uonevu. Wewe kama mwalimu sisitiza kwamba lile ambalo kwa mwingine analiona kama mzaha tu au la kufurahisha, kwa mwingine inaweza kuwa dhihaka mbaya sana. Kwa kufanya hivyo utakuwa unahamasisha wanafunzi wajadili mada hii na kuwafanya wafikirie suala hili kwa undani zaidi. Kwa ajili hiyo unaweza kuwapa vifaa vya kuwasaidia au kujadiliana nao jinsi ambavyo wangependa kutendewa au kutotendewa. Hapa chini kumetolewa vifaa kadhaa vya kuchapishwa kwa ajili yao.

Yanayotakiwa uyafahamu:

Kuhusu uonevu huzungumziwa pale panapotokea mambo 4 yafuatayo:

- **Nguvu zisizowiana:** Mwathirika hujikuta yuko peke yake dhidi ya mwonevu au waonevu wengi.
- **Marudio:** Usumbufu huo hutokea zaidi ya mara moja kwa wiki.
- **Muda:** Usumbufu huo hujitokeza kwa muda mrefu (zaidi ya wiki au miezi).
- **Utatuzi wa migogoro:** Mwathirika hawezi kujinusuru kwa nguvu zake toka kwenye uonevu huo.

Uonevu huweza kufanikiwa tu endapo hakuna ajuaye. Endapo mtu atajaribu kumsema huyo mwonevu, basi yeye huanza kukanusha na kujitetea kwa ujanja tu. Hueleza matendo yake kana kwamba mwathirika ndiye ameanza uchokozi. Kwa matukio ya aina hii ni muhimu sana, kila shambulizi, kila tusi, kumcheka mtu, n.k. kuandika kila kitu kilivyotokea.

Unachoweza kuandika:

- Andika tukio hilo jinsi ulivyoliona na kulishuhudia mwenyewe. Nani walihusika, umetendewa kitu gani?
- Andika tarehe, muda na mahali tukio hilo lilipotokea
- Andika watu wote ambao unadhani wameliona tukio hilo (walimu, wanafunzi, mwangalizi wa shule). Hawa wanaweza kusikilizwa baadaye kama mashahidi).
- Ikiwa uonevu huo umesababisha maafa yoyote upande wako nukuu kila kitu (k.m. vitu vyako vilivyoharibika, kama umekwaruzwa au kuwa na uvimbe usoni).

Tarehe:	Muda:	Mahali:

Yaliyotokea:

Watu wafuatao walikuwa watenda maovu:

Watu wafuatao walishuhudia vitendo hivi:

Tukio hili lilisababisha haya yafuatayo:

Kwenye kielelezo hiki unaweza kuwapa wanafunzi muda wa dakika kumi hivi ili kufikiria na kuandika, kabla ya kuanza kujadiliana na wanafunzi

Hivi ndivyo ningependa kutendewa   1. 2. 3.
Haya nayaona kuwa ya kijinga   1. 2. 3.

3.5. Mazoezi na shughuli

Kwenye sura hii yataonyeshwa baadhi ya mazoezi ambayo wewe na darasa lako mnaweza kuyafanya. Yanasaidia kuzuia uonevu kati ya wanafunzi na kufanya majaribio ya kuishi vizuri pamoja kwa amani.

4. Kuingilia kati kwenye Vurugu za wanafunzi

Kwenye tukio baya la uonevu, ambapo mwanafunzi anapata mateso makali na kuonewa, unapaswa wewe kama mwalimu kuingilia kati mara moja. Katika sura hii utapewa orodha ya kukusaidia kujua kama vurugu hizi kweli ni uonevu. Baada ya kuthibitisha hivyo, unaweza kurejea katika mbinu zilizodokezwa, ambazo zinakupatia utekelezaji ulio na uhakika. Mwanzoni mwa kila hatua imeelezwa ni hali gani na masharti gani ya kuzigatiwa na ni hatua zipi za kufuatwa.

4.1. Orodha: Je, huu ni uonevu kweli?

Ili kuwa na uhakika kama kweli tatizo hili ni uonevu na siyo mgogoro wa kawaida, kuna baadhi ya dalili zinazoweza kuonyesha tendo hilo. Hapa tutajaribu kuorodhesha kwa ufupi:-

- **Mabadiliko ya tabia kwa mwathiriwa:** Mwathiriwa huonyesha dalili fulani ambazo zinatokana na mateso yake. Huzuni, uchokozi usiotarajiwa, woga na mvutano, kupoteza vitu au mali yake mara kwa mara, kutojiamini, kujitenga na jamii, maendeleo mabaya shuleni, kutozingatia darasani, dalili za udhaifu wa kimwili kama vile maumivu ya kichwa, maumivu ya tumbo, kupoteza hamu ya chakula, utoro shuleni na kujitafutia cheti cha daktari kwa kujifanya ni mgonjwa (26).
- **Mgogoro huu huonyesha nguvu zisizo na uwiano mzuri:** Mwathiriwa huonekana kuwa mnyonge kuliko mwonevu, aidha kwa sababu ya kimo chake kimwili au mwonevu anao wanafunzi wengi upande wake ambao wanamsaidia matendo yake au kuyavumilia bila kuyakemea.
- Vitendo hivi hufanyika mara kadhaa kwa wiki na huwa vimeanza tangu wiki na miezi kadhaa, bila kukoma.
- Mwathirika hawezi kujikwamua kwenye hali hii yeye binafsi, aidha kwa ajili ya kuogopa huyo mwonevu wake au majaribio yote ya kujinusuru yameshindikana mpaka sasa. Msaada wa kutoka nje unahitajika sasa (27).
- Mwathirika huelezea hali hiyo kuwa ni mbaya sana au ambayo haiwezi kuvumilika na kwamba mateso yamekuwa makubwa mno. Unaweza kuelewa sasa ni jinsi gani mwathirika anajihisi na ni mateso gani ya uonevu yanampata. Unaweza kupima uaminifu wa mwathiriwa kwa kutumia kielelezo kifuatacho kwa kumwuliza jinsi anavyojisikia.

Kigezo/Nakala ya mazungumzo:

Inahusu:	Darasa/Mwalimu wadarasa:
Waliopo:	Tarehe / Muda:

Yaliyomo kwenye Mzungumzo:

Ufumbuzi:

Yafuatayo ni muhimu kuzingatiwa:

- Endapo baadhi ya dalili za uonevu hazitajitokeza wala kutajwa na wanafunzi, basi mateso hayo hayatakuwa makubwa. Yawezekana ni ugomvi tu wa kawaida na hivyo haihitaji kuingilia kati.
- Ikiwa mwanafunzi ataorodhesha chini kabisa ya kielelezo, lakini kwenye maongezi akaonyesha wazi na kuwa mwaminifu, yawezekana pengine anahusika kwa namna fulani. Hapa inabidi wahusika wote waulizwe na uchunguzi kufanyika zaidi.
- Kama kweli sifa kadhaa za uonevu zimeonekana na kukubaliana, na pia alama iko kwenye robo tatu ya kielelezo, basi hii itakuwa ni dalili kubwa inayothibitisha kuwepo kwa uonevu. Hapa itakuwa muhimu na wajibu kuingilia kati.

Kielelezo hiki kinaweza kutumika pia ili kupima mafanikio au kushindwa baada ya wiki kadhaa, ambapo mwathirika ataombwa tena kulinganisha hali hiyo na kielelezo hicho (29).

4.2. Mbinu ya „Bila Lawama“.

Kama jina linavyojieleza njia hii iitwayo „Bila Lawama“ hutumika kutatua matatizo bila kulaumiana. Lengo si kukabiliana na muhusika kwa sababu ya vitendo vyake ili ajisikie vibaya, bali kutoa msaada kwa mwathiriwa. Jambo la muhimu ni kumlinda mwathiriwa. Kwa hivyo ni kuwawezesha wanafunzi kuchukua jukumu la kutatua matatizo yao wao wenyewe. Hii ni kuamsha moyo wa ustadi wa kijamii na hivyo kumpunguzia mzigo mwalimu kwa kuelekeza wajibu mahali pengine. Mbinu hii inaweza kutumika katika shule yoyote ile na haina kiwango cha umri. Kiwango cha mafanikio kimethibitishwa kuwa asilimia 87%. Kwa vile wanafunzi wengi wanahusishwa, njia hii inaonyesha athari kubwa ya kinga dhidi ya uonevu. Kutotumia adhabu kunamfanya mwonevu asiendelee kufanya maovu yake wala kuchokoza wenzake.

- Mara tu ukigundua kuwa mwanafunzi fulani anaonewa, mwite kwa ajili ya mazungumzo. Mweleze kuwa unahisi hajisikii vizuri na kuwa una mpango wa kuanzishakikundi kitakachotatua matatizo haya. Mwombe idhini yake na mwambie kuwa anaweza kuwasiliana nawe kila wakati kama kuna dharura yoyote.
- Baadaye mwite mhusika mkuu wa uonevu kwa mahojiano: Mwonevu mwenyewe na washiriki wenzake au watazamaji wa tukio hilo. Kundi la washiriki ni bora liwe na idadi ya watu 6-8. Mwathiriwa mwenyewe asiwepo kwenye mazungumzo haya.
- Usiwasukumie hatia watenda maovu hayo au kuwaulizia juu ya tukio hilo.Haja kubwa ni kupata ufumbuzi na wala siyo kujua sababu. Hata kama wanafunzi wenyewe wataanza kujitetea, usiwasikilize. Unaweza kusema kwa mfano: „ haja yetu si kujua ni nani amefanya nini. Tunataka leo kutafuta suluhisho“.
- Sasa anza kwa utulivu na kwa njia ya kirafiki, kwa kuwataka msaada. Mfano:“Nimegundua kwamba,…fulani….siku zilizopita hajisikii vizuri. Nina imani mnaweza kumsaidia“. Ni muhimu sana kuwa maelezo haya yaeleweke kama ombi la kutaka msaada. Kwa kawaida wanafunzi wako tayari kusaidia hata kama hapo awali walikuwa watenda maovu wenyewe.
- Uliza kundi lote juu ya uwezekano wa ufumbuzi wa tatizo hili na kunukuu mapendekezo hayo. Waeleze kuwa uchunguzi utafanyika ili kuona utekelezaji wake. Kundi zima liwajibike na waeleze wazi juu ya suala hili.
- Panga muda wa kukutana nao tena kama wiki 1-2 zijazo.
- Baadaye fanya mazungumzo mafupi na kila mshiriki wa kundi hili (pia waathirikawa zamani), kama kumekuwepo na mabadiliko yoyote. Mara nyingi huwa ni hivyo.
- Ikiwa hapatakuwepo na mabadiliko yoyote, kaa tena na kundi hili na kutafuta njia nyingine ya ufumbuzi (30).

Maongezi na Waathiriwa	Kuadhimisha wanakundi	Kutatua matatizo na kundi	Majadiliano ya baadaye

Angalia chini link:

https://www.youtube.com/watch?v=USpkIt4Lr-w

4.3. Mbinu ya Kasi

Tofauti iliyopo kazi ya njia hii na ya awali, ni kuwa kwenye mbinu hii ijulikanayo kama Kasi“, mwonevu hukabiliwa kikamilifu kwa vitendo vyake alivyovifanya. Hapa inatakiwa iundwe kamati yenye kujumuisha walimu kama 2 hadi 5 au wafanyakazi wa jamii. Ishara muhimu ya mbinu hii ni kuweka mipaka iliyo wazi na kumkabili muonevu katika maongezi haya. Ni muhimu kwanza kwa kutumia orodha, kuhakikisha kama kweli suala la uonevu lipo, vinginevyo kutumia hisia tu kunaweza kuleta kutoelewana na wasiwasi wa bure. Kadhalika mbinu hii isitumike kwa wanafunzi wa umri mdogo, bali kwa tahadhari ni bora kuanzia miaka 14.

- Kwanza chagua kundi la „kuzuia uonevu“ na walimu wenzako lenye walimu kama 2-5. Waeleze shabaha na madhumuni ya kundi hili na jinsi gani wafanye endapo tukio la uonevu litatokea.
- Kwanza muulize mwathiriwa na kumhakikishia kuwa utatatua matatizo haya. Angalia pia kuwa wanafunzi hawajulikani majina yao na hakuna yeyote anayepata taarifa hii. Uliza maswali ya kina na yanayolenga shabaha na kunukuu kila jambo ili baadaye uweze kukabiliana na huyo muonevu. Lini, wapi na nani alihusika? Nani aliona tukio hilo? Alifanya nini?Panga sasa mazungumzo na mwenzako wa kamati ya kupambana na uonevu, na mweleze vizuri juu ya tukio hilo. Tafuta tarehe mwafaka ili kupambana na mwonevu na chagua atakayeandika mukhtasari.
- Mwisho mweleze mwalimu muhusika wa somo na kwamba utamwita huyo mwonevu wakati fulani toka darasani.
- Wakati ukiwadia mchukue huyo mwonevu nje ya darasa kwenye maongezi katika chumba cha faragha. Kama ni waonevu wengi, basi waite wote kwa pamoja.
- Sasa waeleze wanafunzi kwamba unazo taarifa tayari kuhusu matukio haya na watajie baadhi yake.Waeleze wazi kuwa uonevu hauwezi kuvumiliwa hata siku moja, huku ukiwa mtulivu na makini. (mwongozo wa mahojiano unaonyeshwa kwenye makala zifuatazo). Usiruhusu mambo ya kuanza kujitetea. Kisha jaribu kwa pamoja wewe na wanafunzi wako kutafuta mikakati ya ufumbuzi wa kuzuia uonevu na unyanyasaji. Toa muda wa majaribio, ili kuona kama hali imejirekebisha.
- Mwonevu atarudi tena darasani kwake, bila kusema kwa nini alitolewa nje ya darasa wakati wa masomo.

- Endesha mazungumzo ya mwisho (31).

Mazungumzo na mwathirika na maswali ya wazi	Andaa kamati ya kuzuia maovu na ratiba	Mtaarifu mwalimu wa darasa	Kukabiliana na mtenda maovu	Mazungumzo ya mwisho

4. Maelezo kuhusu Mbinu ya Farsta „Nyongeza kwa hatua ya tatu ya maelekezo ya Mbinu ya Farsta“

Jina la muhusika:_____Darasa :_____Tarehe:_____

Unafahamu kwa nini tunataka kuongea nawe ?
(Ngoja, na usikubali kudanganywa)

.....anayo matatizo. Je unajua lolote ?

(jina la mwathirika)

(Tumia jambo lolote dogo kuchimbua ukweli na bakia kwenye uamuzi wako).

Fungua karatasi na kuanza kukabiliana naye:

Tunajua kwamba unahusika. Tarehe.....umetenda yafuatayo:

1.
2.
3.

(Usiruhusu majadiliano. Usiruhusu ujanja wa kujitetea).

Hii ni mbaya sana. Hii siyo masihara, hii ni uonevu.

Uonevu ni mashambulizi ya ziada kwa afya ya kiroho. Hii lazima ikomeshwe mara moja !

Unaweza kuchangia nini ili uonevu dhidi ya.....ukome ?

(Uliza ni jukumu gani mwenyewe alilonale, tafuta makubaliano na kuyazingatia)

Utafanya nini ikiwa utaona wengine wanafanya hivyo ?

(Andika na kueleza mtanzamo bora kwamba hata mhalifu anaweza kuwa mshiriki mwema dhidi ya uhalifu wa aina hii.)

Tutakuagalia kwa muda wa..... Tutaongea na wahusika wengine.

Baadaye tutaongea nanyi kwa pamoja.

Je unasemaje?

Mhalifu asieleze darasani kwa nini aliitwa nje kwa maongezi.

(Uliza ni jukumu gani mwenyewe alilonalo, tafuta….)

Andika na kueleza mtazamo bora, ……

…nje kwa maongezi.

4.4. Mbinu dhidi ya Uonevu – "Olweus"

Mbinu hii dhidi ya uonevu inaelezea mwelekeo sahihi wa vitendo ambao mwalimu inabidi aufuate endapo dalili za uonevu zitajitokeza. Suala la muhimu kwenye mbinu hii ni kwamba wanafunzi wenyewe huandika kwa mukhtsari matukio yote na kutoa maoni yao. Mbinu hii inafaa kwa wanafunzi ambao wanaweza kuandika vizuri. Mwalimu anaweza pia kuchukua jukumu hili la kuandika. Kwa hali yoyote inampasa mwalimu kufanya mukhtasari wa mjadala wote na kuwataka wanafunzi maoni yao wale wote waliohusika, nahata kuwahusisha wazazi wao. Aidha Mwanasayansi Olweus anasisitiza kuwa uangalizi wakati wa mapumziko ni wa muhimu sana, kwa sababu vurugu nyingi shuleni hutokea wakati ambapo hakuna uangalizi au usimamizi (32). Aidha sheria za wazi darasani zitawezesha kuleta mwelekeo mzuri (kama ilivyoelezwa kwenye kifungu cha 3.1.), na majadiliano ya mara kwa mara juu ya vurugu na uonevu ni lazima yafanyike.

- Mtake mwathirika aje kwenye maongezi ya faragha, mara tu unapopata taarifa za tukio la uonevu. Mtake mwanafunzi akueleze kwa ufupi, jinsi hali hiyo ilivyo, ni nani wahusika na tangu lini matatizo haya yameanza. Mhakikishie kwamba sasa utamsaidia na wale wote waliohusika itabidi wawajibike.
- Nukuu yale yote ya muhimu. Sasa mtake mwanafunzi huyo aandike aliyokueleza. Ikiwa mwanafunzi hataweza, basi unaweza kumsaidia kuandika.
- Linalofuata sasa anza majadiano na mwonevu, vile vile akiwa peke yake, kama ilivyotajwa hapo juu. Mweleze wazi kuwa vurugu na uonevu hapo shuleni hauwezi kuvumiliwa hata kidogo, na kuwa utafanya kila liwezekanalo ili kukomesha tabia hii. Nukuu maongezi haya. Mwonevu naye aandike mongezi haya na kujieleza ni kitu gani kilichomfanya atende maovu haya. Athibitishe kwa maandishi kuwa hatarudia kutenda maovu haya.
- Ikiwa wanafunzi kadhaa watakuwa wameshiriki katika uonevu huu, basi zungumza na kila mmoja peke yake. Baadaye zungumza na wote waliohusika katika kundi hilo kwa pamoja. Ni muhimu sana kusisitiza kanuni na sheria zinazotakiwa kufuatwa darasani.
- Nakili kila kitu tena. Nakala hizi wapewe wahusika wote:
- Kila mwathirika apewe nakala
- Muonevu na wazazi wake wapewe nakala
- Waombe wazazi waeleze kwa maandishi maoni yao na ni hatua gani wamechukua kuhusu suala hili.

- Weka kumbukumbu katika nyaraka za wanafunzi kwa matukio yoyote hapo baadaye.
- Endapo vitendo hivi vitarudiwa, waite wazazi shuleni kwa mazungumzo ili kutafuta sababu za uonevu huo na jinsi ya kupata ufumbuzi. Watake wazazi wamweleze mtoto wao kuwa vurugu na uonevu wa hali yoyote ile hauwezi kamwe kuvumiliwa shuleni na madhara yake ni makubwa. Itakuwa ni jambo la maana kama wazazi wataweka sheria zao ambazo mtoto wao anapaswa kuzifuata na kuzizingatia.
- Ni wajibu wako pia kuongea na wazazi wa mwathirika. Waeleze kuwa ni muhimu sana mtoto wao ajifunze jinsi ya kujiamini, k.m. kupitia kwenye michezo ili kujenga urafiki na vijana wenzake.

Manzungumzo na mwathirika + Mukhtasari →	Mazungumzo na mwonevu + Mukhtasari →	Wote wapewe mukhtasari →	Maoni ya wazazi →	Mazungumo nawazazi

Mbinu hii ni ya wazi kabisa yenye mkakati ulio rahisi kueleweka na kufuatwa; hata hivyo yawezekana kuwa baada ya mazungumzo hayo uonevu unaweza kuendelea. Kinga kamili ya mwathiriwa haiwezi kuahidiwa. Hivyo ni vema kutayarisha wakufunzi wa kufuatilia hali hii ili mwathirika asiendelee kuteseka. (Angalia sura ya 4.5.).

Aidha haijulikani ni vipi wazazi watakavyofanya baada ya kupata taarifa hii. Kwa familia ambayo ina tabia ya malezi makali au kutumia malezi ya adhabu tu, matokeo yake yanaweza kuwa na athari mbaya. Njia nyingine badala ya kuwataarifu wazazi ni kupendekeza wanafunzi kufanya mazungumzo kati yao wenyewe. Hapa inabidi mwonevu amwombe radhi mwathiriwa na kuthibitisha kwa ukweli kuwa hatarudia tena kutenda maovu hayo (33). Huu unaweza kuwa mkataba wa ushahidi wenye uzito wa kumbana kisheria.

Video kuhusu mbinu ya Anti-Bulling na vifaa vingine vinapatikana hapa chini:

https://www.youtube.com/watch?v=P9C5wJ6uAk0

https://www.youtube.com/watch?v=Vd5nWSrgYMc

https://www.youtube.com/watch?v=w0YBmiac0vw

http://olweus.sites.clemson.edu

http://www.violencepreventionworks.org/public/olweus_bullying_prevention_program.page

---

1 Jannan, Mustafa (2010): Das Anti-Mobbing-Buch. Gewalt an der Schule – vorbeugen, erkennen, handeln. 3.Auflage. Weinheim und Basel. S. 21 - 27

2 Blum, Heike / Beck, Detlef (21.8.2007): Ohne Anklage und Strafe. Frankfurter Rundschau 63. Jahrgang Nr.193D/R/S. Link: http://www.no-blame-approach.de/media/downloads/FR21082007Dokumentation.pdf

3 Jannan, Mustafa (2010) S. 21 - 27

4 Blum, Heike / Beck, Detlef (21.8.2007)

5 Kasper, Horst (1998): Mobbing in der Schule. Probleme annehmen Konflikte losen. 2. Auflage. AOL Lichtenau.Beltz Verlag, Weinheim und Basel. S. 56

6 Kasper, Horst (1998) S. 56 f. Und: Jannan, Mustafa (2010) S. 16

7 Melzer, Wolfgang / Schwind, Hans-Dieter (Hrsg.) (2004):Gewaltpravention in der Schule. Grundlagen –Praxismodelle – Perspektiven. Baden-Baden. Nomos Verlagsgesellschaft. S. 54.

8 Cierpka, Manfred (2011): Faustlos. Wie Kinder Konflikte gewaltfrei losen lernen. 8. Auflage. Freiburg im Breisgau,Verlag Herder. S. 16

9 Baade FW, Brock, J./ Koebe, S / Zumvenne, G. (1982): Theorien und Methoden der Verhaltenstherapie. EineEinfuhrung. DGVT, Tubingen, S. 111

10 Jannan, Mustafa (2010) S. 37. Und: Deegener, Gunther (2010): Kindesmissbrauch. Erkennen – helfen – vorbeugen.5. Auflage. Beltz Verlag, Weinheim / Basel. S. 59 ff

11 Cierpka, Manfred (2011): Faustlos. Wie Kinder Konflikte gewaltfrei losen lernen. 8. Auflage. Freiburg im Breisgau,Verlag Herder. S. 57 – 59. Und: Jannan, Mustafa (2010) S.44 – 46

12 Jannan, Mustafa (2010) S. 72

13 Kasper, Horst (1998) S. 190d e/dwld/schulprofil/ AntiMobbingKonvention.pdf

www.friedenspaedagogik.de/content/download/6590/35573/file/Kapitel%204.3.pdf

http://www.rims-fulda.de/fileadmin/dateien/ueber_uns/Anti-Mobbing-Konvention.pdf

14 Jannan, Mustafa (2010) S. 72 ff

15 Jannan, Mustafa (2010) S. 28 – 29. Und: Brundel, Heidrun. In: Melzer, Wolfgang / Schwind, Hans-Dieter (Hrsg.)(2004): Gewaltpravention in der Schule. Grundlagen – Praxismodelle – Perspektiven. Baden-Baden. NomosVerlagsgesellschaft. S. 139 – 151

16 Kasper, Horst (1998) S. 167 – 168

17 Kostka, Michael (2007): Spannend unterrichten –Unterrichtsmethoden zur aktiven Einbindung der Schuler. PDFDatei:http://www.erdkunde-sonderschule.de/Dokumente/Skript%20zum%20Methodeneinsatz.pdf

18 Kasper, Horst (1998) S. 167 - 168

19 Kostka, Michael (2007)

20 Johnson, D. W. / Johnson, R.T. / Maruyama, G. (1983): Interdependence and interpersonal attraction amongheterogeneous and homogeneous individuals. A theoretical formulation and a meta-analysis of the research. Reviewof Educational Research, 52, S. 5 - 54

21 Kostka, Michael (2007)

22 Lesniak, Elisabeth (2005): Bewegungspausen wahrend des Unterrichts. Fruhjahrsakademie „Gesunde Schule“ 2005, Lernstation. Stadtgymnasium Detmold.

23 Kasper, Horst (1998) S. 190. Und: Jannan, Mustafa (2010) S. 74

24 Olweus, Dan (2006): Gewalt in der Schule. Was Lehrer und Eltern wissen sollten – und tun konnen. 4. Auflage.Verlag Hans Huber, Hogrefe AG, Bern. S. 89 – 90Und: Schubarth, Wilfried (2010): Gewalt und Mobbing an Schulen. Moglichkeiten der Pravention und Intervention.W. Kohlhammer GmbH Stuttgart. S. 145

25http://www.beltz.de/fachmedien/paedagogik/buecher/produkt_produktdetails/15216-das_anti_mobbing_buch.html

26 Jannan, Mustafa (2010) S. 27. Und: Kasper, Horst (1998) S. 65

27 Jannan, Mustafa (2010) S. 21 – 27

28 http://www.beltz.de/fachmedien/paedagogik/buecher/produkt_produktdetails/15216-das_anti_mobbing_buch.html

29 Jannan, Mustafa (2010) S. 133

30 http://www.no-blame-approach.de Und: Blum, Heike / Beck, Detlef (21.8.2007) Link: http://www.no-blameapproach.de/media/downloads/FR21082007Dokumentation.pdf und: Jannan, Mustafa (2008): Das Anti-Mobbing-Buch. Gewalt an der Schule – vorbeugen, erkennen, handeln.Weinheim und Basel. S. 127 – 129 und: Schubarth, Wilfried (2010): Gewalt und Mobbing an Schulen. Moglichkeiten der Pravention und Intervention.W. Kohlhammer GmbH Stuttgart. S. 153 – 154

31 Jannan, Mustafa (2008) S. 115 – 118 und: Schubarth, Wilfried (2010) S. 154 – 155Und: Cirillo, Filomena (Mai 2012): Die Farsta-Methode. Link: https://sozarb.h-da.de/instituteveranstaltungen/stoppt-die-mobber/belastungen/mobbing/praeventionsansaetze/farsta-methode/

32 Olweus, Dan (2006): Gewalt in der Schule. Was Lehrer und Eltern wissen sollten – und tun konnen. 4. Auflage.Verlag Hans Huber, Hogrefe AG, Bern. S. 74 – 76

33 Jannan, Mustafa (2010) S. 121 – 124Und: Haller, Birgitt / Stogner, Karin / Pelinka, Anton (Leitung) (2004): Gewaltpravention in der Schule. Finanziertvon: bm:bwk, Abteilung Schulpsychologie und Frauenburo der Stadt Wien (MA 57). S. 9 – 11. Link:http://www.ikf.ac.at/pdf/gewaltpraevention.pdfUnd: Olweus, Dan (2006) S. 97 – 104 und: Schubarth, Wilfried (2010) S. 142 - 146

34 http://www.beltz.de/fachmedien/paedagogik/buecher/produkt_produktdetails/15216-das_anti_mobbing_buch.html

IBARA YA TATU

KUZUIA VURUGU

Somo la darasani

Maelezo: A

Migogoro hutokea mara kwa mara darasani. Hutokea kutoelewana baina ya wanafunzi na hata matatizo mengine makubwa. Hii husababisha hasira, mvutano, kuchukiana na kuvimbiana. Mara nyingi huwa hakuna muda wa kukabiliana na migogoro hii ili kutafuta ufumbuzi. Kwa sababu ya muda mfupi uliopo, walimu huwa hawataki kupoteza muda wao bure kwa ajili ya matatizo kama haya. Mara nyingi hutokea migogoro kati ya walimu wenyewe au walimu na wanafunzi. Haja ya kuzungumzia matatizo haya ili kutafuta ufumbuzi inabakia pale pale. Hivyo inashauriwa hapa kupanga muda maalumu kwenye ratiba „Saa ya mjadala".Ni muhimu kutenga saa nzima mara moja kwa wiki, au ikiwezekana mwishoni mwa siku, ili kujadili masuala mbalimbali yanayowahusu wanafunzi na kubadilishana mawazo. Wewe kama mwalimu hutakiwi kuingilia mazungumzo haya. Utatuzi wa migogoro huwa umo mikononi mwa wanafunzi wenyewe. Ni jukumu lao kutoa maoni yao.

Lengo:

Vijana inabidi wajifunze jinsi ya kutatua matatizo yao wenyewe kwa kushirikiana na wenzao. Ni wajibu wao kutafuta suluhisho baina yao na kutumia fursa hii kwenye kundi kupata jibu linalokubaliwa na wote. Wewe mwenyewe kama mwalimu inakubidi ujifunze kukabidhi madaraka na majukumu yako na kujiweka kwenye kinacholingana na wanafunzi wako.

Vifaa:

Viti, „ mada", Ubao, Kanuni zinazotawala mjadala (angalia nakala ya kielelezo).

Utekelezaji:

- Fanya mduara wa viti pamoja na wanafunzi wako.
- Tundika kanuni za mjadala wenu kwenye ubao.
- Chagua wanafunzi wawili ambao watakuwa viongozi wa mjadala huu. Mwanafunzi mmoja achukue orodha ya wajumbe na kuwaruhusu waongee. Mwingine atakuwa kiongozi wa mjadala.
- Mwanafunzi mwenye tatizo ataongea mbele ya wote na kumtaja moja kwa moja yule aliyeanzisha ugomvi huu. Wakati anaongea, atakuwa ameshikilia mkononi „mada". Wakati wa maelezo hairuhusiwi yeyote kuongea. Hakikisha wewe na kiongozi wa mjadala kuwa hakuna anayetoa maoni yake.
- Endapo wanafunzi wengi watakuwa wanahusika katika mzozo huu, mada watapewa kwanza hawa wahusika, kabla wanafunzi wengine hawajatoa maoni yao. Wote wanaohusika kwenye mgogoro huu watatoa maelezo yao mmoja mmoja kama

walivyoshuhudia. Wanafunzi wanaotaka kusema lolote, lazima waombe ruhusa na wataongea tu ikiwa wataruhusiwa na kiongozi wa mjadala.

- Baada ya wahusika wote kwenye ugomvi huu watakuwa wametoa maoni yao , maswali ya nyongeza yanaweza kuulizwa. Hakikisha kuwa mada inapitishwa kwenye mzunguko.
- Mwishoni kiongozi wa mjadala atauliza wahusika mmoja baada ya mwingine, matakwa yao toka kwa wenzake. Mara nyingi kufikia hatua hii akili huanza taratibu kuwa shwari na wahusika huanza kuelewana. Wakati mwingine wahusika huhitaji msaada wa wengine toka kwenye kundi, ambao watatoa maoni yao kuhusu mgogoro huu.
- Kila mgogoro utamalizwa na kiongozi wa mjadala. Tatizo jingine linaweza kufuatia kujadiliwa kama bado kutakuwa na muda wa kutosha.
- Kumbuka: mwishoni mwa kila mjadala ni muhimu kuimarisha ushirikiano wa kundi lako kwa njia ya ishara fulani, ili kuondoa hali mbaya ya kutoelewana nje ya darasa. Ishara fulani inaweza kutumika (kama kupeana mikono au kuimba wimbo).

Kielelezo 2: Nakala ya „Sheria za Mjadala“

Sheria hizi zisomwe na kiongozi wa mjadala kabla ya kuanza majadiliano

1. Nitakuwa mkimya na kusikiliza wakati mwanafunzi mwenzangu anapo ongea.

2. Nitaongea tu, pale msimamizi wa mjadala atakaponiruhusu na nitakapokuwa na mada mkononi.

3. Nitabakia kuwa mkweli, bila kutania au kutukana mtu yeyote.

4. Nitaheshimu wazo la kila mtu bila kudharau au kuzomea

Somo zuri

Utangulizi:

Somo zuri ni muhimu kwa kuwa huu ndio msingi wa mafundisho yasiyokuwa na usumbufu wowote. Pasipo kuwepo na usumbufu, basi hapawezi kuwepo na uwezekano wa kutokea uchokozi au mzozo wowote darasani. Lakini lazima tujiulize ni somo gani lililo zuri? Je, inakubidi ufanye nini ili kujenga mazingira mazuri yanayoweza kuzuia ghasia darasani? Ufundishaji mzuri unategemea vigezo vingi, hata hivyo matendo ya mwalimu ndilo jambo la muhimu sana katika kufanikisha somo lenyewe.

Lengo:

Kwa msaada wa kuwepo na mazingira mazuri ya kujifunza, ni tegemeo kubwa kwamba somo zuri ni lile linaloweza kutoa maarifa pia furaha na mchanganyiko wa vitendo unaweza kufikiwa. Kwa kufanya hivyo somo linaweza kuepukana na kuduwaa na vitendo vya kuleta ghasia darasani. Hivyo hata upande wa walimu hapatatokea usumbufu au uchokozi wa aina yoyote.

Somo lenye mafanikio:

1. **Mchanganyiko:** Hakikisha kuwa somo lako linakuwa na mchanganyiko wa mazoezi na vitendo. Hapa tumia mbinu mbalimbali na kazi zinazotofautiana. Pia hakikisha kuwa hukai muda wote umesimama mbele ya darasa wakati wa kufundisha. Tumia njia nyingine za mafunzo ya kijamii, kama vile kazi za vikundi zinazoamsha motisha ya wanafunzi. Usitumie vitabu vya kiada tu, bali pia vifaa vingine kama vile karatasi, picha, mapango, kalamu za rangi, CD`s, ubao, n.k. Kwa njia hii somo litakuwa la kusisimua kwa kuwa na vitu mbalimbali vya mchanganyiko na hivyo kuchangamsha darasa zima.
2. **Hali halisi:** Unaweza kuwahamasisha wanafunzi wako ikiwa mada za masomo zitahusiana na maisha ya vijana kwenye manzigira wanayoishi. Wanafunzi wanakuwa na usikivu zaidi kwani yale yanayofundishwa yanapendeza na kumvutia kila mmoja wao.
3. **Kujifunza kwa Marudio:** wape wanafunzi wako uwezekano wa kurudia yale waliyojifunza na kuyatafakari. Kwa msaada wa mazoezi mbalimbali unaweza kuwapima wanafunzi wako kama wameelewa na kuzingatia yale waliyojifunza. Baada ya kuona mafanikio hayo basi vijana watafurahi na kujivunia hatua waliyofikia.
4. **Kutofautisha:** Jaribu kufikiria kuwa kila mwanafunzi anao uwezo wake wa kujifunza tofauti na wengine. Kufuatana na idadi kubwa ya wanafunzi hii si rahisi hata kidogo. Jaribu kujiandaa mapema kabla ya kuanza kipindi kwa kazi mbalimbali, k.m. karatasi zenye maswali tofauti au kazi za ziada kwa ajili ya wale wenye uwezo mkubwa zaidi. Hii itasaidia kuepukana na kutokuwa na utulivu darasani kwa wale watakaokuwa wamemaliza haraka kazi zao ili wasiweze kuduwaa bure kwa kukosa la kufanya na hivyo kuanza kusumbua wengine.
5. **Kusifia kazi nzuri:** Motisha nzuri kwa wanafunzi ni kupata maoni mazuri toka upande wa mwalimu. Wasifie wanafunzi wako kwa kazi nzuri waliyoifanya na waonyeshe ili waone kuwa unafurahia na kujivunia kazi njema waliyoifanya. Unaweza kutoa mfumo fulani wa zawadi kwa kuthibitisha jambo jema au alama ya furaha kwa kuonyesha kidole juu na wenzake kumpigia makofi na kupewa zawadi. Utaona jinsi kitu kama hiki kinavyosaidia sana kuleta motisha kwa wanafunzi.

Kazi za vikundi na kujifunza kwa ushirika

Maelezo na Malengo:

Mfumo wa kazi za vikundi na kujifunza kwa ushirika hukuza hali ya kujitegemea na kujenga ushirikiano mzuri miongoni mwa wanafunzi. Huongeza morali wa kujifunza pamoja na ustadi wa kijamii na kuheshimiana. Kwa njia ya kubadilishana mawazo, wanafunzi huweza kufahamiana vizuri, pengine kwa mara ya kwanza na hivyo kushirikiana vizuri zaidi. Hii itasaidia kuondoa hali ya kubaguana miongoni mwao. Wanafunzi hujisikia wako huru bila kulazimishwana mwalimu wao na hivyo kuimarisha ushirikiano na kuvumiliana miongoni mwa wanafunzi. Hufanya kazi ambazo wanazipenda na wana uwezo nazo. Hii huongeza motisha miongoni mwao. (angalia: www.finken.de/media/musterseiten/1630.pdf; Blumenberg 2006 http://home.uni-leipzig.de/didakrom/Methoden/Methoden%..)

Aidha kwa kutumia njia hizi za kujifunza kijamii huweza kujenga uaminifu na mikakati imara ya utatuzi wa migogoro. (www.finken.de/media/musterseiten/1630.pdf)

Kazi za Vikundi

Kazi za vikundi ni mfumo wa kazi ambao unashirikisha wanafunzi 3-6 kufanya kazi pamoja kwa kujitegemea. Mara nyingi matokeo ya kazi za vikundi huwasilishwa mwishoni mbele ya darasa. Walimu hukaa nyuma na kuangalia jinsi wanafunzi wanavyofanya kazi kwa kutoa huduma na ushauri pale ambapo msaada unahitajika. (tz. Blumenberg 2006)

Tumia mfumo huu hasa kwa kujifunza mada mpya

Kujifunza kwa ushirika

Tofauti iliyopo kati ya kazi za vikundi na za ushirika ni kuwa kwenye mfumo wa kazi za vikundi hakuna uhakika kama wanafunzi watafanya kazi kwa pamoja na kwa ushirika. Kwenye mbinu hii ya kujinufaisha kwa ushirika ni kuwa kila muhusika anawajibika kuchukua hatua maalumu ya ushirikiano na wengine (taz. Finken Verlag). Kila mmoja anahesabika kuwa sehemu ya kundi zima ili kutatua jambo fulani na kufikiria lengo lililokusudiwa ili kuleta mafanikio ya pamoja. Kazi ya kila mmoja ni nyongeza ya wote na kila mmoja anamtegemea mwenzake.

Mbinu ijulikanayo kama „***Think-Pair-Share***“ ***(„Fikiria na kugawana pamoja“)***, ndiyo msingi wa kujifunza kwa ushirika. Kwanza kila mmoja huanza kufikiria mwenyewe na kukusanya mawazo yake. Baada ya hapo wote hubadilishana mawazo yao kabla ya kufanya mukhtasari na kuwasilisha matokeo yao mbele ya darasa zima (taz. Finken Verlag).

Utekelezaji

- Gawa darasa lako katika makundi madogo ya wanafunzi 4-6. Mbinu inayofaa kugawanya makundi haya itaelezwa hapo mwishoni.
- Wape wanafunzi muda wa kutosha kufikiria jina la kundi lao. Hii hukuza kujitambulisha kwao na kundi hilo.
- Fafanua kwanza lengo ni nini, njia gani itatumika na jinsi gani kazi ya kundi itaonekana kwa maandishi. Hakikisha kuwa kazi waliyopewa imeeleweka.
- Taja muda unaohitajika kumaliza kazi hii.
- Waache wanafunzi wafanye kazi wenyewe, ingilia tu kama kuna maswali, kuna tatizo lolote au kupiga kelele. Wewe uwe tu mwangalizi.
- Tumia kadi ya kuashiria (taz. Nakala 2-4) ili kuwataarifu wanafunzi ni hatua gani wanatakiwa kuwa wameifikia sasa na nini wafanye ***(„Think-Pair-Share“)*** – ***(„Fikiria na kugawana pamoja“)***. Kwa njia hii siyo tu kuwa unabakia nyuma, bali pia hupotezi muda wa kutoa maelekezo. Mtiririko wa kazi unafanyika bila usumbufu wowote (taz. Morgenthau 2004, uk. 3).
- Baada ya hatua hii ya vikundi inafuatia hatua ya kutoa matokeo mbele ya darasa zima. Wakati wa kipindi andika matokeo na kutathmini utendaji wao wa kazi.
- Wape wanafunzi wengine muda wa kutoa maoni yao kwa kundi jingine kabla wewe hujatoa maoni yako juu ya matokeo au makosa yao, na baadaye kujadili kwa pamoja (taz. Druyen 2004).

Usiwaruhusu wanafunzi wauunde vikundi wao wenyewe. Vinginevyo vitaundwa vikundi visivyolingana au kutokea ugomvi au kutengana. Kila mwanafunzi lazima ajifunze kushirikiana na wanafunzi wenzake, bila kujali kama ni mvulana au msichana, au uwezo alionao (taz. Müller 2016, uk. 101)!

Jinsi ya kuunda vikundi

1. **Kucheza karata**: wanafunzi wanavuta kadi moja baada ya nyingine; na hivyo kuunda makundi (Kundi 1: Mfalme, Kundi 2: msichana, Kundi 3: mvulana n.k.)
2. **Maneno**: Mwalimu anaadika maneno fulani kwenye vipande vidogo vya karatasi, ambavyo kila mwanafunzi atavuta. Maneno yanayofanana yataunda kundi moja. (Kundi1: Matunda, Kundi 2: Rangi, Kundi 3: Wanyama, n.k.).
3. **Kuhesabu**: Ikiwa vikundi saba vitaundwa, basi wanafunzi wahesabu 1-7. (Kundi1: wote waliotaja namba 1, Kundi 2: wote waliotaja 2, n.k.). Kwa kufanya hivyo utahakikisha kuwa wale wanafunzi wanaokaa karibu na walio marafiki hawaundi kundi moja.

Kielelezo 3: Nakala „Kazi ya mtu mmoja“ (Fikiria)



Kielelezo 4: Nakala “kazi ya kikundi” (Pamoja)

Kielelezo 5: Nakala “Elezea” (kushiriki pamoja)



Kushughulikia unyanyasaji wa jinsia

Lengo la Mada hii:

> “Vijana wanazungumza hali ilivyo ndani nanje ya shule, ambapo wanasumbuliwa au kusumbua na kunyanyasa wenzao”.

Yafuatayo ni baadhi ya mazoezi na michezo, ambayo ni mafunzo muhimu ya kukabiliana na unyanyasaji wa jinsia. Kwa ajili tu ya mazoezi, ni bora kutenganisha wavulana na wasichana kwa kuunda makundi mawili. Mazoezi yafuatayo yana malengo mawili. Kwanza ni kutoa mafunzo kwa ajili ya wasichana, ili watambue mipaka yao na jinsi ya kujilinda. Pili ni wavulana, kwa kutumia mazoezi haya kujifunza na kutambua mipaka ya wasichana inapoanzia na kuishia.

Maigizo: Sema Hapana

Lengo: wanafunzi wajifunze kusema “Hapana” kwa hali wasiyoipenda.

Muda: Dakika 30.

Utekelezaji:

- Gawa darasa katika makundi mawili: Kundi la wavulana na kundi la wasichana.
- Kundi moja litoke nje ya darasa. Kundi jingine lipe kazi ya kufanya huko nje, k.m. kujifunza kukariri kichwani hadithi fulani, kujaza mazoezi fulani kwenye karatasi, kuigiza mchezo fulani, n.k.

- Waulize wanafunzi darasani, ni hali ipi ambayo hawakuweza kukataa kusema „Hapana“.
- Wanafunzi wanyooshe mikono mmoja mmoja na kueleza walivyokuwa wanajisikia wakati ule.
- Kwenye makundi madogo na kwa maelekezo ya kiongozi wataonyesha hali hiyo kwa vitendo vya kuigiza na baadaye kujadiliana pamoja.
- Sasa wape fursa wabadilishane mawazo na kutoa mapendekezo yao nini kifanyike hapo baadaye.
- Sema kwa sauti ndogo na kwa sauti kubwa ukitumia neno „HAPANA“ kwa kumaanisha kukataa. Waeleze kwamba kukataa ni kukataa, yaani mtu akisema „HAPANA“, lazima ieleweke hivyo kuwa hapendi na hakuna mjadala tena.
- Fanya mazoezi kwa kusema „HAPANA“ kwa sauti kubwa. Waonyeshe kimwili ishara ya kitendo cha kukataa.
- Mwisho onyesha tena hali ya awali, safari hii kwa ishara nyingine.
- Uliza muhusika na kisha wengine kwenye kundi, walivyojisikia na tofauti ipi wameweza kuitofautisha.
- Ita kundi jingine ndani na kuwapa kazi ya kufanya kama hapo mwanzo.
  (taz. Walker 2000, uk. 124).

Kugusagusa na kusababisha hali isiyopendeza

Lengo: wanafunzi wajifunze kusema “HAPANA” na kutambua hali isiyopendeza.

Muda: vipindi viwili

Maandalizi: Fikiria na kuandika kwenye kadi mifano ya hali isiyopendeza yaani hali mbaya. Kwa mfano: “…Fulani anakwambia unyanyue juu shati au gauni lako”, “….fulani anakuita “mjinga”, “…..mwanafunzi mwenzako anakuchungulia wakati ukivaa nguo”, n.k.

Utekelezaji:

- Waulize wanafunzi ni ubaya gani au uzuri gani uliopo mtu akikikuita mjinga.
- Waeleze wazi maana ya kujisikia vizuri, kujisikia vibaya, au kutokuwa na uhakika kama hali hiyo ni nzuri au mbaya kwako
- Wanafunzi wataje mifano hiyo – hali nzuri, hali mbaya, na hali yenye wasiwasi. Kila mtu ana mawazo yake, wakati mwingine jambo fulani linamfurahisha yawezekana mwingine linamuudhi na ni wazi hataki.
- Waeleze wazi kuwa wanaweza kusema “HAPANA” wakati wowote wanapojisikia hivyo.
- Gawa kundi katika vikundi vidogo.
- Kila kundi likiwa na kadi 6 ambazo zitatayarishwa kabla ya kuanza kipindi.
- Vijana wawe na muda wa kusoma na baadaye kuamua ni hali ipi wanaiona ni mbaya zaidi ya nyingine, moja baada ya nyingine. Baadaye watawasilisha na kuzungumzia ile hali mbaya zaidi kuliko zingine zote. Zingatia kwamba: kuna mawazo na hisia tofauti.

- Jadiliana na kundi zima juu ya hali hizo na kubadilishana mawazo na kutoa mapendekezo.
- Waulize wanafunzi juu ya hali mbaya ambazo wamezishuhudia wao wenyewe. Jadiliana pamoja na kutoa mapendekezo.
- Mwisho unaweza kutoa ilani kwa kusema pamoja kwa sauti kwamba,

  „MIMI MWENYEWE NDIYE NAAMUA NIFANYE NINI NA MWILI WANGU“! Mayowe.

IBARA YA NNE

JE INAWEZEKANA NJIA NYINGINE?

„Tuna wasiwasi, nini kitatokea kwa watoto wetu hapo baadaye – lakini tunasahau kuwa tayari hivi sasa wamekwisha komaa.“ Stacia Tauscher

Mada: Amani na Vurugu/Ukatili, Watoto, Ubaguzi na Chuki dhidI ya watuna watu wengine aumtu na mtu.

Utata: hatua ya 3

Ukubwa wa kundi: 9-24

Muda: dakika 90

Maelezo ya jumla: Mchezo wa kuigiza:

- Vurugu na ukatili miongoni mwa watu
- Uonevu

Shabaha:

- Haki ya Uhuru na Amani kwa kila mtu
- Haki ya Binadamu na ulinzi dhidi ya Ubaguzi
- Watoto wana haki ya kulindwa kutokana na uharibifu waufanyao na matendo mabaya kama unyanyasaji wa kimwili na kiakili.

Lengo:

- Kujifunza sababu na matokeo ya uonevu
- Kuchunguza ni jinsi gani unaweza kumaliza tatizo hili
- Uelewano na waathirika wa uonevu

Vifaa:

- Nakala ya mchezo wa kuigiza (tukio moja kwa kila kikundi)

- Nakala moja ya Hadithi ya uonevu

Matayarisho:

- Hakikisha kwamba chumba kina nafasi ya kutosha kufanya mchezohuu wa kuigiza.

Utangulizi

1. Eleza zoezi hilo. Fafanua hatua zinazotakiwa kufanyika kwenye vikundi vidogo. Kazi inayotakiwa kufanywa ni mchezo wa kuigiza kuhusu uonevu.
2. Ikilazimu, unaweza kuanza kwa kuuliza maswali ya awali kama wote wanafahamu uonevu ni nini na kwamba unaweza kutokea mahali popote kama shuleni, vyuoni, kwenye klabu au kazini.
3. Vikundi vitatu vitaundwa na kila kundi litapewa igizo lake. Toa dakika 15 za kutayarisha na kufanya mazoezi ya kuigiza.
4. Baadaye kila kikundi kitaonyesha igizo lake.
5. Epukana na kutoa maoni mwanzoni mpaka vikundi vyote vimefanya maigizo yake. Baada ya hapo wote wakae pamoja na kuanza kujadiliana.

Maandalizi ya mwisho na Tathmini

Anza kwa marudio ya mchezo wa kuigiza.

- Kundi linapata wapi vifaa vinavyotumika? Toka kwenye hadithi, Filamu juu ya uonevu au uzoefu wao wenyewe?
- Matukio hayo ni ya kweli?
- Igizo la 1: ni jambo gani ilikuwa la manufaa na la kusaidia. Ni kitu gani kimeleta matatizo?
- Igizo la 2: ni rahisi kiasi gani kumweleza waziwazi yule anayeonea? Ni mbinu gani yenye athari nzuri na athari mbaya?
- Igizo la 3: ni rahisi kiasi gani kuongea wazi na yule anayeonewa. Je ni vipi ufumbuzi unaweza kupatikana ambao utakubaliwa na yule anayeonewa?

Waombe wanafunzi watatu ambao wataelezea hadithi ya kweli. Waombe watoe maoni yao juu ya hadithi hiyo ya uonevu na kisha jadiliana juu ya chanzo cha uonevu na jinsi gani ya kukabiliana na hali hiyo.

- Ni hisia gani unapoonewa?
- Je ni makosa yao wenyewe wale wanaoonewa?
- Wale wanaoonea wenzao wanafanya hivyo ili kuonyesha kitu chochote? Kama kipo ni kitu gani?
- Je, uonevu ni mfumo fulani wa vurugu na ghasia?
- Je,uonevu una uwiano wowote na madaraka?
- Je, uonevu unaweza kuzuiwa?

- Kama una urafiki na yule anayeonewa, je unaweza kumwarifu kiongozi mwenye mamlaka kuhusu jambo hili ingawa huyo rafiki yako amekueleza matatizo yake kwa faragha?
- Ni chuki zipi zinafanywa dhidi ya yule anayeonewa?
- Ni nani anahusika kukomesha tatizo la uonevu?

Ilani kwa kiongozi wa mjadala

Kuna uonevu wa moja kwa moja na uonevu wa kujificha. Uonevu wa moja kwa moja ni tabia ya matusi, kuchokoza, kusukuma, kupiga au mashambulizi ya kimwili, kunyangànya au kutupa mfuko au mali ya mwingine, kumchukulia mtu fedha yake, kushambulia au kumtishia mtu kwa ajili ya dini yake, rangi ya mwili wake, ulemavu, au nguo alizovaa. Uonevu usiokuwa wa moja kwa moja, yaani uliojificha, ni kwa mfano kueneza uongo kwa makusudi ya kumuudhi, kumsingizia au kumtenga huyo anayeonewa. Tabia kama hii hufanywa na mtu mmoja au watu wengi dhidi ya mtu au watu fulani. Kimsingi tabia hii ya uonevu ni kumtishia mtu kimwili au kiakili, ambayo huchukua muda fulani na baadaye unyanyasaji huo kudumu kwa kipindi kirefu.

Kama unafanya kazi kama mshauri wa kundi fulani, kwenye klabu, shuleni, chuoni au sehemu yoyote kazini, unaweza kuigiza hali hiyo. Zingatia kama wanafunzi kwenye kundi lako wamewahi kuwa na uzoefu wa uonevu huko nyuma. Gawa wanafunzi kwenye makundi na wape maigizo kama inavyostahili.

Mapendekezo kwa aliji ya ufuatiliaji

Fanya utafiti kama kwenye sehemu yako kuna mpango wa usuluhishi wa migogoro ya vijana. Mwombe msemaji aje kuzungumza na kundi lako na toa wazo la kuanzisha mpango wa usuluhishi shuleni, chuo kikuu au kwenye klabu yako ya michezo. Pengine kundi lako lina mpango wa kuanzisha sera ya kupambana na uonevu hapo shuleni au kwenye shirika lako. Mbinu zinazoelezwa katika zoezi liitwalo „nini kifanyike dhidi ya ubaguzi“? zinafaa sana kwenye mkakati wa sera ya kupambana na ubaguzi. Kama kundi litapenda kufanya maigizo juu ya udhibiti wa migogoro, basi zoezi la „kucheza pamoja“ linaweza kutumika.

Hatua za kuchukuliwa

- Tafuta kundi au shirika linaloshughulika na Uonevu na ulizia msaada wao.
- Unaweza kushauri kikundi kilicho kibunifu, kuandika mchezo wake wa kuigiza na kisha kuonyesha kwa umati wote.
- Kila mwana kundi anaweza kutayarisha au kuongoza mjadala shuleni au kwenye jumuiya yake juu ya Uonevu.
- Unda kundi hapo shuleni au kwenye jumuiya yako ukishirikiana na marafiki zako ili kuwasaidia wale wanaoonewa.
-

KARATASI

Matukio ya kuigiza

Tukio 1: Mwanafunzi anaenda kwa kiongozi shuleni na kujaribu kueleza kuwa mwenzake shuleni anaonewa. Kiongozi wa Shule ni mtu mkali sana. Anasema kuwa maadili ya siku hizi ni mabaya mno na anayo maoni mabaya juu ya vijana wa siku hizi. Mwalimu wa darasa anadai kuwa yeye si wajibu wake kwenye jambo hili na hahusiki hata kidogo. Walimu wengine wanalichukulia juujuu suala hili na kuwa tabia ya huyo mwonevu haielezi kabisa jinsi alivyo. Mwalimu mshauri wa shule anapatwa na wasiwasi, lakini anakabiliwa na kazi nyingi. Hana muda wa kuweza kuingilia kati jambo hili.
Tukio 2: Kundi la wanafunzi linajaribu kuzungumza na rafiki yao msichana ambaye anamwonea mwanafunzi mwenye umri mdogo.
Tukio 3: Wanafunzi wengi wamekutana pamoja na wanaongelea juu ya mwenzao ambaye anaonewa na kundi la wanafunzi wenye umri mkubwa kuliko yeye. Wanataka kumsaidia mwenzao na hivyo kuongea na kufanya kila liwezekanalo ili kuweza kumsaidia.

Hadithi za Uonevu

Hadithi 1	**Hadithi 2**	**Hadithi 3**
„Umri wangu ni miaka 12 na ninachukia shule kwa sababu hakuna ninayempenda. Baadhi wananitukana kwa maneno mabaya pale wanapoweza kufanya hivyo. Wanasema mimi ni mbaya wa sura na ni mnene na mweusi na kuwa wazazi wangu wanaona aibu. Rafiki yangu mpenzi haongei nami tena na sasa hivi amekuwa rafiki wa baadhi yao. Namchukia kweli. Najisikia ni mpweke na ninaogopa kuwa huenda yale wanayoyasema kuhusu wazazi wangu ni ya kweli.“ *Rosana*	“Nimehamia kwenye shule mpya ya sekondari. Tangu siku ya kwanza ninahisi kuwa baadhi ya wasichana wananionea wivu kwa sababu vijana wengi wa kiume wananipenda. Sasa nataka kuhama shule hii kwani wananitumiavikaratasi vya siri vyenye vitisho. Nikiwa nyumbani napokea simu za matusi. Wameniibia pia vitabu na madaftari yangu.Wiki iliyopita nilipokwenda chooni, wasichana watatu walikuja nyuma yangu. Wamenitishia na kisu na kunitaka nihame shule hiyo na kwenda shule nyingine. Wameniita kuwa mimi ni malaya. Siwezi kuvumilia tena. Ninaogopa na nimechukia sana. Nimejaribu kuongea na Mkuu wa Shule lakini hakunisikiliza vizuri. Sijui nifanyeje” *Lisbeth*	“Rafiki yangu amenieleza kuwa hapo shuleni kwetu kuna wanafunzi wanaomwonea. Nilitaka kumsaidia na hivyo kuamua kuongea nao, lakini tangu hapo mie pia wameniandama. Sasa sisi sote wawili wameanza kutuonea. Wameanza kututania na kutuchezea, na wametutishia kuwa watatupiga. Tumeamua kuwa sote tunyamaze kwani tunaogopa kuwa tukimweleza yeyote hali itazidi kuwa mbaya.” *Andrey*

TazamaVideo iliyoandaliwa na kikundi cha wanafunzi wa SAUT kutoka kitivo cha ualimu

Vurugu katika maisha yangu

"Zingatia sheria tatu: jiheshimu wewe mwenyewe/heshimu watu wengine/wajibika kwa matendo yako" *Dalai Lama*

Mada: Vurugu na Amani, Usalama wa Binadamu, Haki za Binadamu

Utata: 3

Ukubwa wa kundi: lolote

Muda: dakika 60 – 120

Maelezo ya jumla: Mada hii inahusu kuchunguza na kujadili uzoefu wa washiriki ambao wameshuhudia wao wenyewe

Lengo/shabaha:

- Haki ya kuishi**,** Uhuru na usalama wa mtu
- Haki ya mawazo, dhamira na uhuru wa kuamini dini yoyote.

Lengo:

- Mtazamo wa mtu mwenyewe siyo tu kama mtendewa bali pia mtenda vurugu mwenyewe.
- Kujifunza mikakati ya kukabiliana na vurugu
- Kuvumiliana na kuwajibika

Utangulizi

1. Somo hili linatoa fursa kuongea pamoja juu ya uzoefu, kimawazo na kihisia kama mlivyowahi kutenda au kutendewa na wengine.
2. Hakikisha kwamba wote wanazifahamu sheria za mjadala kwenye kundi na wanaelewa kwamba: kila mmoja ni lazima aheshimiwe, kwamba kila yeyote atakalolisema linabakia kuwa la siri miongoni mwenu, na mtu yeyote asilazimishwe kusema lile asilotaka kulisema.
3. Uliza kwanza maswali machache juu ya ukatili" na waulize wataje mifano waijuayo katika maisha ya kila siku, k.m. matusi, kukejeli, kusukuma kwenye mstari, kupiga kofi, wizi, uaharibifu wa vitu.
4. Waombe wote wafikirie kama dakika 5 hivi matukio haya:
   a) Fulani anaanza kukufanyia ukatili

b) Jinsi mtu fulani anavyofanya ukimfanyia ukatili
c) Unaona jinsi mtu mwingine anavyofanya vurugu, lakini hufanyi lolote.

Maandalizi ya mwisho na Tathmini

Anza kwa kuuliza kama washiriki waliona ugumu wowote kutafuta mifano yao wenyewe. Kisha chambua sababu na madhara ya hali hizo: a), b), na c). Kila mmoja anaweza kwa hiari yake kutoa maoni yake. Aeleze nini kilitokea, jinsi alivyojihisi na kisha anzisha mjadala wa pamoja.

Baadhi ya maswali yanaweza kuwa yafuatayo:

1. Kwa nini kulitokea ukatili huo
2. Je wengine wangefanya nini katika hali kama hiyo?
3. Kwa nini ulifanya hivyo?
4. Je kuna njia nyingine ambayo ungefanya? Je wengine wana maoni gani?
5. Je mtu mwingine wa tatu angefanya nini ili kuzuia hiyo fujo isitokee?
6. Kwa nini hakuna aliyesaidia katika mfano (c) hapo juu?
7. Nini kilisababisha ugomvi huu?
8. Ni matukio mangapi yamesababishwa na kutoelewana? Matukio mangapi yametokana na chuki, uadui au wivu, ni matukio mangapi yamesababishwa na tofauti za utamaduni, tabia, maoni au tofauti za dini?
9. Nini maana ya Uvumilivu? Je unaweza kufafanua vipi neno „Uvumilivu“?
10. Je ni sawa kuvumilia yote yafanywayo au yasemwayo na wengine?
11. Kwa nini Uvumilivu ni maadili muhimu hasa kwa ajili ya kukuza haki za binadamu?

Ushauri kwa kiongozi wa mjadala

Somo hili linahitaji hasa wajibu, unyeti na moyo wa kujituma kwa kiongozi wa mjadala.Hivyo ni jambo zuri kama kazi hii itafanywa na watu wawili kuendesha somo hili. Ukiwataka washiriki waelezee juu ya yale waliyoshuhudia wenyewe kuhusu vurugu, basi wachague mifano ya matukio ya kila siku ambayo hayataleta kero kwao na ambayo kweli wangependa kuelezea kwenye kundi lao hilo. Ikiwa kikundi kitakuwa na washiriki zaidi ya kumi, basi ni bora kuunda vikundi vidogo wanapoelezea juu ya masiha yao ya kila siku. Sisitiza kwamba shabaha ya zoezi hili ni kujifunza njia za kukabiliana na vurugu ambapo washiriki watajua ni kwa nini vurugu zinatokea, ni mwenendo gani unatakiwa kuwa nao ili kujiepushana vurugu.Wakumbushe washiriki juu ya Ibara ya 1 ya Azimio la Haki za Binadamu:

” Watu wote wamezaliwa huru na wako sawa kwa heshima na haki”

Kama mtu anategemea kuwa wengine wafuate na kutimiza Ibara hii, basi naye pia inabidi afanye hivyo.

Karibu watoto na vijana wote wameshuhudia vitendo viovu maishani mwao. Vitendo hivi vingine ni vibaya sana na huleta kiwewe (k.m. kunajisi kwa nguvu). Yawezekana zoezi hili

likamkumbusha muhusika yale ya siri yaliyowahi kumpata. Au utagundua kuwa wengine wanaanza kubadilika tabia zao kama ilivyokuwa desturi huko nyuma, wanarudi nyuma au wanaanza uadui. Hapa lazima ujiandae.

Ni vema kuwa na orodha ya simu na anwani ya taasisi za ushauri ambazo unaweza kuzigawa kama zitahitajika.

Tofauti nyingine ya kuigiza

Zoezi hili linaweza kuchezwa vizuri kwa kuingiza. Waombe watu wawili, watatu au wanne waigize tukio fulani. Wengine kwenye kundi wataangalia tu. Unaweza kukatisha igizo hilo na kuwataka watazamaji watoe maoni yao, au wapendekeze ni vipi igizo hilo lingeweza kuendelea. Mtazamaji yeyote anaweza kuingilia kati na kuchukua nafasi mojawapo kwa kuendeleza igizo hilo tofauti.

Mapendekezo ya kazi ya baadaye

Tafuta Mashirika au Taasisi zinazosaidia waathirika wa unyanyasaji, k.m. simu au mtandao wa wasaidizi wa waathirika. Pia tafuta mashirika ambayo yanashughulikia kuleta Uelewano naUvumilivu kwenye jamii. Ikiwa utapenda kuendelea na mada ya Amani na Vurugu, unaweza kuangalia kwenye Maandishi ya “Heile Welt” (Ulimwengu mwema), uk. 158. Utayapata majibu yanayolingana na Amani.

Mawazo ya utendaji

Wasiliana na shirika ambalo linajihusisha na Amani na hali isiyo ya Vurugu, ili kuona kama kuna uwezekano wa kufanya kazi huko.

ULIMWENGU MWEMA

Si vis pacem, para pacem

(Kama unataka Amani iandae hiyo Amani kabla)

Mada: Amani na Vurugu, Afya na Mazingira

Utata/Ugumu: **3**

Ukubwa wa kundi: 15 – 30

Muda: **dakika 90**

Maelezo ya jumla: Somo hili linaanza na jaribio kuhusu methali na maneno ya busara kuhusu vipengele muhimu juu ya Amani. Baadaye washiriki wafikirie juu ya mambo haya:

- Maana ya Amani
- Amani ya ndani, Amani baina ya watu na Amani baina ya mazingira.
- Tabia yenye Amani

Lengo/Shabaha:

- Haki ya Amani
- Haki ya kuishi
- Haki ya mazingira yenye Afya

Lengo:

- Kutambua mambo ya muhimu yanayohusiana na Amani
- Mjadala kuhusu maana mbalimbali zinazohusiana na Amani na matumizi yake katika maisha yetu ya kila siku
- Kukuza heshima, ushirikiano na kuwajibika.

Vifaa:

- Karatasi kubwa (A3) au bango kubwa la karatasi
- Kalamu za rangi na kalamu za kawaida
- Nakala ya karatasi kwa kila kikundi

Matayarisho:

- Toa nakala ya Mduara wa Amani (1) kwenye karatasi kubwa

Utangulizi

Somo hili lina sehemu mbili. Sehemu ya 1: Kukamilisha ....(Mandalas) (dk. 25) na Sehemu ya 2: Mjadala wa Amani (dk. 30).

Sehemu ya 1: Kukamilisha ... Mandalas (dk. 25)

1. Waonyeshe washiriki wa kikao karatasi kubwa iliyo wazi ya Mduara wa Amani. Waeleze sehemu za mduara: Amani ya ndani yako (wewe mwenyewe), Amani baina ya watu na Amani baina ya mazingira. Waeleze kuwa kukamilika kwa mduara huo kunaonyesha kuwepo na Amani. Washiriki watafute "Maneno ya Ukweli 21" ambayo yanahusu vipengele muhimu vya kuishi kwenye Amani. Maneno haya yanapatikana kwenye Methali na maneno yenye busara duniani kote.
2. Vikundi vitatu vitaundwa. Kila kundi litapewa kalamu, nakala ya karatasi (Mandala) na nakala ya jaribio. Watafute neno linalokosekana kwa kila methali. Huu ndio ufunguo muhimu wa maadili ya mambo mbalimbali yanayohusiana na Amani.
3. Vikundi vyote vikishamaliza, basi watajumuika wote kwa pamoja. Waombe washiriki, moja baada ya mwingine, kusoma hizo methali zilizokamilika. Hakikisha kama ni sahihi, na mwombe huyo aliyesoma aandike neno hilo kwa kalamu ya rangi katika Mduara wa Amani.
4. Pitia methali zote namna hiyo mpaka hiyo Mandala imekamilika na kuonyesha hali kamili ya Amani.

Sehemu ya 2: Mjadala wa Amani (dk. 30)

1. Washiriki watarudi tena kwenye vikundi vyao vya awali. Kila kundi litapewa mwongozo wa mjadala huo. Wajadiliane kuhusu maswali na maadli yaliyomo yanayohusu kila sehemu katika Mduara huo wa Amani. Wajaribu kukubaliana juu ya maswali hayo na kuwa tayari kutoa taarifa ya mjadala wao.
2. Mwishoni waite wote kwenye kikao cha pamoja ili kila kikundi kitoe taarifa yake.

Maandalizi ya mwisho na Tathmini

Zungumzia kwanza juu ya Mduara na usahihi wa maadili hayo pote duniani.Baadaye zungumzia sehemu ya 2 ya zoezi hili.

Sehemu ya 1:

- Ni vipi ilikuwa vigumu kutafuta maneno yanayokosekana? Ni methali ngapi au maneno mangapi ya busara waliyokuwa wanajua kabla? Je kweli haya ni maneno ya „Hekima" ambayo ni muhimu kwa maisha yetu ya leo?
- Je maneno yaliyopo ndani ya mduara yanaeleza maadili ya kawaida duniani kote? Je maadili haya ni muhimu katika tamaduni zote duniani? Ni maadili yapi ni muhimu katika tamaduni yako?
- Je yapo maadili mengine ya msingi ambayo hayakutajwa hapa?

Sehemu ya 2:

- Mwombe mwakilishi mmoja toka kila kikundi aweze kueleza kwa mukhtasari maswali yaliyomo kwenye mwongozo wa mjadala huo. Zungumzia maswali yafuatayo katika kila mjadala huo:

    - Je ilikuwa rahisi kufikia makubaliano katika vipengele vyote vya majadiliano?
    - Ni swali gani lilikuwa na utata zaidi? Kwa nini?
    - Washiriki wa kundi wanasemaje juu ya utata huo?
    - Kwa nini watu wanakuwa na maoni tofauti juu ya mada hii ya Amani?
    - Watu wengi wanahusisha mada hii ya Amani ya ndani yako (wewe mwenyewe) na Dini? Kwa nini?
    - Je ni lazima kila mtu awe muumini wa dini ili kuwa na maadili ya Amani ya ndani?
    - Ni kitu gani kinahusisha majadiliano haya na Haki za Binadamu?
    - Je, Amani ndiyo sharti au msingi wa Haki za Binadamu, au ni wajibu kwanza kuheshimuHaki za binadamu kabla ya kufikia hali ya Amani?

Ushauri kwa kiongozi wa mjadala

Katika swali lililoulizwa kwenye somo hili kuhusu Amani na vurugu kuna taarifa za msingi kwenye ukurasa **343.** Hizi zitasaidia katika mjadala kwenye kikao cha pamoja. Jaribu kufafanua uhusiano uliopo baina ya mielekeo hiyo mitatu ya Amani. Usiwe na shaka au kuogopa utata utakaotokea, kwani hii ni mada ambayo ina utata mkubwa! Badala yake jadili sehemu zote mbili, wanaounga mkono na wanaopinga, na kusisitiza kuwa hakuna jibu lililo sahihi au lisilo sahihi. Ikiwa kundi litakuwa na zaidi ya watu 18, basi unda vikundi vidogo zaidi na bora kuwa na vikundi sita vidogo kuliko vikundi vikubwa vitatu. Usisahau kufanya nakala zaidi!

Tofauti nyingine

Unaweza kufanya Sehemu ya 1 ya kukamilisha mduara kwenye kikao. Soma methali moja baada ya nyingine na kuuliza wakamilishe maneno yanayokosekana. Safari hii andika maneno haya moja kwa moja kwenye karatasi kubwa ya kutundika. Baada ya hapo fanya nakala ya mduara mzima uliokamilika.

Mapendekezo ya kazi ya baadaye

Baada ya kupata mwanga huu pengine kikundi kitapenda kuzungumzia matukio waliyoyapata maishani mwao, ambapo pengine hakuna Amani nchini mwao na kubuni mikakati ya kukomesha vurugu kwenye maisha yao. Angalia zoezi la ,"Vurugu maishani mwangu" uk. 147.

Maelezo zaidi

Wazo la Mduara wa Amani lilianzishwa na Pierre Weil, ***"El Arte de Vivir en Paz, Hacia una nueva conciencia de Paz"***. Errepar, Argentinien, 1995. Maana yake ni ***"Sanaa ya kuishi kwenye Amani, hadi kuelewa maana ya Amani".***

Mduara wa Amani unaweza kutafsiriwa kwa namna nyingi. Maoni yafuatayo yanaweza kusaidia katika mjadala wenu:

- Katikati ya mduara huu kuna maana nyingi, hazina mwanzo wala mwisho.
- Maneno yaliyomo ndani ya mduara yanaelezea maadili na tabia au hali ambayo inapaswa kuwepo katika maisha yetu. Kwa mfano kuhusu uwezo wetu, ambao unatuwezesha kuishi kwa amani kwenye jumuiya, ungekuwa kwenye eneo la uchumi, maisha ya kijamii na utamaduni.
- Kuhusu Akili, mwili na hisia inatubidi tujiagalie ndani yetu binafsi ili kufikia Amani ya ndani. Amani ya ndani inaweza kufikiwa tu kama kutakuwepo na hekima, upendo, uvumilivu, huruma, furaha, na kujali afya ya mwili wako wenyewe.
- mwelekeo wa tatu wa amani ni mazingira au amani ya Mali Asili. Hapa tuna sehemu tatu: Maarifa, ili tujifunze na kuelewa, Heshima ya maisha, kujali mali (kama Mali Asali, Miti, Maua, Wanyama, n.k.).

MDUARA WA AMANI (Karatasi ya Maelezo 1)



Jaribio – Maswali ya kujaza (Karatasi ya Mazoezi 2)

Je, unaweza kupata methali na maneno ya busara yanayokosekana kwenye misemo ifuatayo? Kama ni ndiyo, basi utakuwa umepata jibu au ufunguo wa Duara la Amani. Haya ndiyo maneno yanayotakiwa kujazwa ndani:

Uzuri, mwili, huruma, ushirikiano, utamaduni, uchumi, hisia, mazingira, uvumilivu, maelewano, afya, mtu binafsi, maelezo, furaha, haki, maarifa, maisha, upendo, roho, heshima, maisha ya kijamii, jumuiya, mshikamano, muhimu, ukweli, ustawi, hekima

Kifungu cha 1: Uzoefu ni mama wa.....

Kifungu cha 2:

a) .....ni kuliko kifo. (methali toka Burundi)
b) .....na uvumilivu zina athari ya miujiza, kulingana na matatizo hayo na vikwazo
c) Binadamu anapenda.....toka moyoni mwake, lakini Mungu la. (William Cowper)
d) Usiahidi kitu, kama....., usijibu barua kama bado una hasira. (methali ya Uchina)

Kifungu cha 3: .....ni bora kuliko utajiri.

Kifungu cha 4: Shaka ndio ufunguo wa.....(methali ya Iran)

Kifungu cha 5: Ukitaka kuheshimiwa, ni lazima.....wewe mwenyewe (methali ya Spain)

Kifungu cha 6: Kugusa dunia ni.....mazingira. (Oglala Sioux Mhindi)

Kifungu cha 7: Mali iliyo yako.....usiipuuze.....ya mwingine, hata kama ni kubwa; lengo liwe, cha kwako.....kufikiria zaidi.(methali ya Buddhi)

Kifungu cha 8: "Serikali na .....ni katika mambo yote na Sheria za milele maishani. Machafuko na ushindani ni katika mambo yote sheria ya kifo.

Kifungu cha 9:

a) ……bila hekima ni kama maua kwenye matope (methali ya Romania)
b) Mapema au baadaye huja……. ……kwenye mwanga (methali ya Uholanzi)
c) Juu……..Juu……Juu…….Kwani ushirika wa wafanyakazi unatufanya tuwe na nguvu. (Ralph Cgaplin).
d) Vurugu ikiingia nyumbani, sheria inapotea na ……kupitia jikoni (chini ya tanuru). (methali ya Uturuki).

Kifungu cha 10: ……. wa ya roho unajisalimisha kwa moyo (Mahatma Gandhi).

Kifungu cha 11: Dhamira yetu haikufanywa kwa ukweli wa milele. Inabadilika na ……., na hali mpya ya kijamii ina maana ya mabadiliko makubwa ya dhamira yetu.(Walter Lippmann, 1889-1974).

Kifungu cha 12: Ambapo hakuna ufanisi hapawezi kuwepo na……(Beaconsfield)

Kifungu cha 13: Usidanganywe na umbo la nje, kwani maumbile si..... (methali ya Mwingereza)

Kifungu cha 14: Subira ndogo yaweza kuzuia balaa kubwa na kukosekana kidogo kwa subira unaweza.....kuangamiza kabisa. (methali ya Uchina).

Kifungu cha 15: Hekima iko wapi, ambayo imepoteza maarifa? Maarifa yako wapi, ambayo.....tumepoteza (T.S. Eliot).

Kifungu cha 16: Ni rahisi.....kupinda kuliko matakwa. (methali ya Uchina).

Kifungu cha 17: Kama.....njaa, hatutacheka, kwa kuhukumu haraka, tukigandamiza tutakuwa wahubiri, wanaelimu na wahubiri kuliko Baba Mtakatifu, kuyaweka maisha manukato, kutokuwa na ujasiri, kuwapa sumu. (Joseph Collins).

Kifungu cha 18: Angalia kwa.....sikia kwa moyo. (methali ya Wakurdi).

Kifungu cha 19:

Binadamu hujiumba mwenyewe kutokana na uamuzi.....(Rene Dubos)

Kifungu cha 20: Kila moyo ni mwingine, kila nafsi ni nyingine, kila uso ni mwingine.....ndio udanganyifu mkubwa (Margaurite Young).

Kifungu cha 21: Jinsi urefu wa.....ulivyo, inaweza kujulikana kutokana na takataka zilizosagwa (Tahanie)

Mwongozo wa Mjadala (Karatasi ya Mazoezi 3)

Mwongozo wa mjadala: Amani yako wewe mwenyewe (Kundi la 1)

1. Ina maana gani, wewe mwenyewe kuwa na amani?
2. Ni yapi ambayo tunayasema na kuyatenda kila siku yanaonyesha kuwa sisi wenyewe tuko kwenye vita na hatuna amani ya ndani?
3. Je kuna uhusiano wowote kati ya mwili, roho na hisia? Ni uhusiano upi?
4. Tunawezaje kuwa binadamu, ambao wanaishi wenyewe kwenye amani?
5. Je, inawezekana kuwa na uhusiano mwema na wengine kama mtu mwenyewe hana amani ndani yake?

Mwongozo wa mjadala: Amani na mazingira (Kundi la 3)

1. Je, manzingira yanalindwa na jamii?
2. Je, ina maana gani kuishi kwa maelewano na mazingira?
3. Ni nani anawajibika na kuhifadhi mazingira?
4. Ni vita vingapi vitafanywa kwa siku zijazo kuhusu raslimali muhimu (k.m. maji), ikilinganishwa na vita vingine kama vile migogoro ya kimaadili, kitamadunu au kidini?
5. Je, ni muhimu kuishi kwa amani na mazingira ili kufikia hatua ya amani iliyokamilika?

Mwongozo wa mjadala: Amani na wengine (Kundi la 2)

1. Je sisi kama binadamu, tunao uwezo wa kuishi na watu wengine katika amani?
2. Je, kutokuwa na vita ndiko kunamaanisha kuwa kuna amani?

3. Je, tunaweza kujifunza kuishi kwa amani na binadamu wenzetu katika maisha ya kila siku?
4. Kuna sababu za kuwa na matumaini ya dunia yenye amani katika siku zijazo?
5. Je makovu yaliyoachwa na vita yanaweza kuondoka ili watu waweze kuishi tena kwa amani?

Uzuri, mwili, huruma, ushirikiano, utamaduni, uchumi, hisia, mazingira, uvumilivu, maelewano, afya, mtu binafsi, maelezo, furaha, haki, maarifa, maisha, upendo, roho, heshima, maisha ya kijamii, jumuiya, mshikamano, muhimu, ukweli, ustawi, hekima

Majibu ya Duara ya Amani:

Kifungu cha 1: Hekima

Kifungu cha 2:

a) Upendo
b) Uvumilivu
c) Huruma
d) Furaha

Kifungu cha 3: Afya

Kikundi cha 4: Maarifa

Kikundi cha 5: Heshima

Kifungu cha 6: Maelewano

Kifungu cha 7: Ustawi

Kifungu cha 8: Ushirikiano

Kifungu cha 9:

a) Uzuri
b) Ukweli
c) Mshikamano
d) Haki

Kifungu cha 10: Utamaduni

Kifungu cha 11: Maisha ya kijamii

Kifungu cha 12: Uchumi

Kifungu cha 13: Muhimu

Kifungu cha 14: Maisha

Kifungu cha 15: Maelezo

Kifungu cha 16: Mwili

Kifungu cha 17: Hisia

Kifungu cha 18: Roho

Kifungu cha 19: Mazingira

Kifungu cha 20: Mtu binafsi

Kifungu cha 21: Jumuiya

Mduara wa Amani uliokamilika



Mambo ya ndani

"(....) the police always come late/ if they come at all."

"(....) kila mara askari wanakuja wamechelewa/ kama wataweza kuja kabisa." Tracy Chapman

Mada: Haki sawa kwa kila jinsia, Amani na vurugu, Afya

Utata: 3

Ukubwa wa Kundi:6-30

Muda: Dk. 120

Maelezo ya jumla: Somo hili linahusu vurugu kwenye familia ambayo ni moja ya vurugu zinazotendeka mara nyingi, lakini huongelewa mara chache.

Lengo/shabaha:

- Haki ya kulindwa dhidi ya vurugu, mateso na udhalilishaji mbaya.
- Haki ya usawa na kulindwa dhidi ya ubaguzi
- Haki ya usawa mbele ya Sheria (kutendewa haki mbele ya mahakama).

Lengo:

- Uhamasishaji kuhusu mada ya vurugu katika familia na maelezo juu ya uvunjaji wa Haki za wanawake.
- Kukuza ujuzi, kuchambua na kujadili uvunjaji wa Haki za Binadamu
- Kukuza uelewano na kujiamini dhidi ya unyanyasaji wa nyumbani.

Vifaa:

- Karatasi kubwa au Ubao na kalamu za rangi kwa ajili ya maswali ya kutafakari pamoja na kazi za vikundi.
- Amua kati ya ushahidi ulioandikwa hapo chini au andika mwenyewe. Toa nakala kwa kila mtu.
- Kwa kila kundi toa nakala moja kuhusu "Mwongozo wa mjadala wa vikundi"

Matayarisho:

- Kusanya maelezo yoyote yanayohusu sehemu za kuhifadhi wanawake wanaonyanyaswa au taasisi zinazosaidia waathirika wa namna hii. Fanya uchunguzi katika kijiji chako, Wilaya au Mkoa wako.
- Fikiria vizuri ni masuala gani unapenda yazungumziwe, kwa kuwekea maanani uzoefu wa binafsi wa washiriki wako.

Utangulizi:

1. Kwa matayarisho fanya maswali ya kutafakari kuhusu unyanyasaji utokeao mara kwa mara katika mazigira yetu. Andika yote yatakayosemwa, kwanza bila mjadala. Weka karatasi hiyo kubwa au ubao ili kila mtu aweze kuona (Dk. 10).
2. Unda vikundi vidogo vya washiriki wawili hadi sita. Unahitaji angalau vikundi vitatu.
3. Gawa karata zenye ushahidi.Kuna karata za aina tatu/matokeo matatu., lakini unaweza kuvipa vikundi vingi vyenye tukio lile lile. Kadhalika gawa nakala za "Mwongozo wa mjadala wa vikundi".
4. Toa muda wa dakika tatu kwa ajili ya kusoma ushahidi. Waambie kuwa mjadala huu unahusu ajenda hii. Wote waelewe kuwa mjadala huu kuhusu matatizo haya unaweza kumhusu mtu binafsi, hivyo haitakiwi mtu kumlazimisha aseme mengi zaidi ya yale atakayo.
5. Lipe kundi muda wa saa moja kwa zoezi hili.
6. Baadaye mwishoni wote waje kwenye kikao kwa ajili ya mjadala wa mwisho na tathmini.

Maandalizi ya mwisho na Tathmini

Anza kwa kuuliza ni jinsi gani kazi imefanyika kwenye vikundi. Ni vipi ushahidi ulikuwa na maswali yamehusika vipi? Je, vikundi vimetumia njia tofauti na waeleze uchambuzi wao kwa kila kosa. Jadili kuhusu uhusiano uliopo na hali ya kawaida ya kijamii:-

- Zikoje vurugu za ndani kwenye jamii yako na nchini kote kwa ujumla?
- Ni Haki gani za Binadamu ziko hatarini?
- Ni vitu gani vinasababisha vurugu za nyumbani?
- Kwa nini vurugu nyingi zinasababishwa na wanaume dhidi ya wanawake na siyo wanawake dhidi ya wanaume?
- Ni vipi vurugu za nyumbani zinaweza kukomeshwa? Nini kinaweza kufanywa na:

    - Mamlaka za Serikali
    - Taasisi
    - Waadhiriwa
    - Marafiki na majirani?

- Linganisha matokeo ya kundi pamoja na vipengele vya mjadala vilivyotolewa wakati wa kuchangia mawazo ya awali. Je vurugu za ndani ziliorodheshwa? Kama hapana, ni kwa nini?
- Ni aina gani nyingine za vurugu dhidi ya wanawake zilitajwa kwenye mjadala? Hizi pia ziorodheshwe. Uliza kama mmoja wa washiriki anapenda kujadili moja ya mada hizi na zungumzia juu ya utekelezaji au jinsi ya kuendelea na kazi hii.

Vidokezo kwa Mkuu wa mjadala

Uwe mwangalifu sana kwa masuala yaliyo nyeti, kutomtaja mtu jina lake na masuala ya faragha (pengine baadhi wamekwisha kukumbana na vurugu kama hizi kwenye familiia zao). Wote waelewe kwamba hakuna yeyote atakayelazimishwa kueleza yale asiyoyataka. Mazoezi yote yalengwe kufuatana na matakwa ya washiriki.

Zoezi hili linaitwa "masuala ya ndani", kwa sababu vurugu na fujo nyingi dhidi ya wanawake hutendwa ndani ya familia. Moja ya matukio makubwa ya vurugu za ndani ni ugomvi au ukatili wa kimwili, na ndiyo maana ya kuchagua usemi huu wa "ushahidi". Maelezo yote yanahusu uhalifu halisi na waathirika wenyewe. Unaweza kubadilisha yaliyomo au kuleta maelezo mengine ili kuyalinganisha na hali halisi ya mahali hapo au kundi hilo.

Maoni kuhusu vurugugu ni nini, yanatofautiana sana. Maoni ya jinsi ya kukomesha ukatili huu dhidi ya wanawake, ambao ulipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1993, unafafanua ukatili huu kuwa ni:

" vurugu zozote zitendwazo dhidi ya wanawake kwa sababu ya jinsia yao, yanayosababisha madhara ya kimwili, kijinsia, au kiakili, na mwisho kusababisha vitisho, mateso au kumnyang'anya uhuru, iwe hadharani au faraghani".

Inajumuisha unyanyasaji wa kimwili, kijinsia na kiakili kwenye familia, kadhalika kunajisi kimwili, kunajisi watoto wa kike, vurugu za mahari, kunajisi ndani ya ndoa, kutahiri wanawake, na mambo mengine ya kimila yanayodhuru wanawake, vurugu nje ya ndoa, unyonyaji wa kimwili, kunajisi na vurugu za kiakili kwenye jumuiya, usumbufu auvitisho kazini, taasisi mbalimbali za elimu, utumwa wa wanawake na umalaya wa kulazimishwa pamoja na vurugu zozote zile za kimwili au kiakili ambazo zinaruhusiwa au kuvumiliwa na vyombo vya dola mahali popote pale.

Washiriki wa kiume wanaweza kuguswa na mjadala huu na hivyo kuwa wakali. Usisahau kuwa shabaha kubwa ya zoezi hili siyo kuwa wanaume na vijana wawe na hisia mbaya, bali ni kutambua na kujadili juu yamfumo unaowapendelea wanaume katika jamii mbalimbali. Kwa hiyo huu unaweza kuwa mjadala mzuri kuzungumzia matokeo ya athari za unyanyasaji dhidi ya wanaweke.

Jambo la kuvutia linaweza kuwa kumaliza zoezi hili kwa kimya cha dakika moja kama ishara ya kuonyesha mshikamano na waathirika wa maovu haya.

Njia nyingine

Kuna aina nyingi ya vurugu na unyanyasaji dhidi ya wanawake. Unaweza kubuni nyanja nyingine za tatizo hili na kuzichunguza kinaganaga.

Mapendekezo kwa ajili ya ufuatiliaji

Vikundi vinaweza kuwasiliana na Polisi na kuuliza ni hatua gani huchukuliwa pale mwathiriwa anapotoa taarifa ya maovu aliyotendewa kwenye kituo cha Polisi. Njia nyingine ni kuwasiliana na taasisi zinazosaidia wanawake au kualika mwakilishi wa shirika hili ili azungumze nanyi na kuwaeleza hali ilivyo katika eneo linalohusika.

Jambo jingine linalochukuliwa kama mwiko katika nchi nyingi duniani ni suala la kujamiiana na ushoga. ***Ikiwa vikundi vitapenda kuzungumzia kwa undani suala hili, basi wanaweza kufanya zoezi la "Let`s talk about sex". Hapa tungependa kusisitizia kuwa suala hili liangaliwe kwa makini sana kufuatana na utamaduni wa sehemu inayohusika, ili kutunza heshima miongoni mwa washiriki.***

Habari zaidi

Changamoto ya Haki za Binadamu

Haki za wanawake na wasichana haziwezi kuuzwa wala kugawanyika, ni sehemu muhimu ya Haki za binadamu. Hii haina maana kwamba haki hizi ni takatifu au zimelindwa. Ni kinyume kabisa, kwani unyanyasaji dhidi ya wanawake ni tatizo kubwa sana. Hasa wasichana wako kwenye hatari kubwa ya kunyimwa haki zao za msingi. Uovu dhidi ya wanawake na wasichana ni tatizo kubwa hususa kiafya na Haki za Binadamu. Kati ya watu watano karibu mwanamke mmoja amewahi maishani mwake kutendewa maovu mabaya na mwanamme au wanaume wengi. Wengi, wakiwemo wajawazito au wasichana, wanajikuta hawana kinga yoyote dhidi ya mashambulizi haya ya mara kwa mara.

Duniani kote uonevu huu dhidi ya wanawake ndiyo sababu kubwa ya vifo vya wanawake au kutopata kizazi (utasa),na inakadiriwa kwamba idadi ya vifo inalingana na ile inayosababishwa na ugonjwa wa kansa au hata zaidi ya ajali za barabarani au ugonjwa wa Malaria kwa pamoja!!! Mateso haya dhidi ya watoto wa kike ni tatizo la ulimwengu mzima na halina kikomo. Mfano mzuri ni uuzaji wa wanawake katika biashara ya umalaya. "Hakuna nchi yoyote duniani ambako wanawake hawateseki na madhara haya. Hakuna sehemu yoyote katika maisha ya mwanamke ambapo hapati vitisho au kushuhudia mwenyewe uonevu wowote ule. Uonevu dhidi ya wanawake hauna mpaka, hauna umri, hauna tabaka, hauna mila wala tofauti za kitamaduni, na unajidhihirisha kwa aina mbalimbali". (1)

Uonevu dhidi ya wanawake ni suala la kisiasa, ambalo ni pingamizi kubwa la usawa na kijinsia. (2). Hili ni suala la kisiasa kwani ni tishio kubwa la demokrasia. Katika Azimio la Bunge la Ulaya linasema kwamba, "Kukosekana kwa usawa na uwiano usiolingana kijamii na kiuchumi kati ya wanawake na wanaume (k.m. ajira, huduma au miundombinu), hauendi pamojanaHaki za Binadamu na kanuni za demokrasia ya kweli. (3)

Vurugu tangu utoto hadi utu uzima

Vurugu dhidi ya wanawake katika umri wao wote

Awamu	**Aina ya vurugu**
Kabla ya kuzaliwa	Utoaji mimba kwa kujali jinsia, kupigwa wakati wa uja uzito unasababisha idadi ya kizazi.
Mtoto mchanga – Utoto	Kuua watoto wachanga wa kike, vurugu za kimwili, kiakili na kijinsia, unyanyasaji wa kijinsia, ukahaba wa watoto na picha za uchi. **Vitu kama hivi ambavyo havilingani na utamaduni wa mwafrika visiruhusiwe hata kidogo na lazima tuvipige vita kali.**
Ujana na utu uzima	Vurugu dhidi ya mwenzako au mpenzi wako (k.m. mashambulizi ya tindi kali (asidi), au "Date Rape – kupanga tarehe ya ubakaji"; kulazimisha mapenzi kwa sababu za kiuchumi (k.m. wasichana, ambao wanaathiriwa na "Sugar Daddies", yaani mabwana wanaotumia fedha kuwatongoza watoto wa kike, kwa ajili ya karo ya shule), vitishio vya kimapenzi kazini, ubakaji, kulazimisha umalaya na picha za uchi, biashara za wanawake, vurugu za wanaume, ubakaji katika ndoa, vifo vinavyosababishwa na mahari, kuuawa na mme, unyanyasaji wa kiakili, unyanyasaji wa wanawake vilema, mimba za kulazimisha.
Mzee	Kujiua kwa kulazimishwa au mauaji ya mjane kwa sababu za kiuchumi (mali), vurugu za kijinsia na kiakili.

Chanzo: Taarifa kuhusu ukatili dhidi ya wanawake - Shirika la Afya Duniani 1997

Takwimu kadhaa zinazoonyesha ukubwa wa tatizo hili

Takwimu hizi kuhusu mateso wayapatayo wanawake nyumbani zinatisha na kusikitisha mno. Zinaonyesha ukubwa wa tatizo hili na pia yale yaliyojificha ambayo hayajulikani. Kila mwanamke miongoni mwa wanawake watano ni mwathirika wa maovu haya. Kwa sababu ya uonevu huu barani Ulaya kila mwaka wanawake wengi huuawa na wanaume au kuumizwa vibaya kuliko ugonjwa wa kansa au ajali za barabarani. (4). Huko Urusi kila mwaka wanawake wapatao 14.500 hupoteza maisha yao kutokana na mateso ya nyumbani. (5).

Uchunguzi uliofanywa na Shirika la kutetea wanawake nchini Ulaya mwaka 1999 unaonyesha kuwa mwanamke mmoja kati ya wanne anatendewa uovu na mme wake. Asilimia 95% ya

uovu huo hutendwa majumbani. Uchunguzi uliofanyika nchini Finnland mwaka 1998 unaonyesha kuwa asilimia 52% za wanawake wenye umri zaidi ya miaka 15 ni waathirika wa maovu hayo kimwili au kijinsia, mwaka mmoja kabla yaani 1997 ilikuwa ni asilimia 20%. Uchunguzi mwingine uliofanywa nchini Portugal mwaka 1997 unaonyesha kuwa asilimia 53,3% ya wanawake waishio nje kidogo ya miji mikubwa, asilimia 55,4% ya waishio ndani ya miji mikubwa na asilimia 37,9% ya waishio vijijini wameathirika na uonevu huu wa wanaume.; asilimia 43% ya uonevu huu umetendwa ndani ya familia (1998). Pia uchunguzi uliofanywa nchini Ubeligigi mwaka 1998 unaonyesha kuwa asilimia 68% ya wanawake wameathirika na uonevu kama huo kimwili na kijinsia. (6).

Unyanyasaji wa majumbani

Haki za binadamu upande wa wanawake siyo kwamba huvunjwa tu wakati wa vita, bali kwanza majumbani. Mwenendo huu wa "binafsi", ndio hasa umesababisha kutoingilia na kuzuia vitendo hivi visifanyike na hivyo kuzidi kuendelea kufanyika. (7).

Utafiti unaonyesha kwamba uwezekano wa mwanamke kudhuriwa, kunajisiwa au kuuawa na mme wake wa sasa au wa zamani ni mkubwa kuliko mtu mwingine baki. Uovu kama huu wa majumbani hauwapati wanawake peke yao bali pia watoto, zaidi ni wasichana na wanawake wa umri mdogo.

Maonyesho, " Mashahidi bubu"

Shughuli hizi zilionyeshwa kwenye maonyesho ya unyanyasaji wa wanawake yaliyoandaliwa na Umoja wa Wanawake (NANE, Budapest,nchini Hungary), kwenye kituo cha Vijana. Baadaye walionyesha mchezo wa Eszter na Kati. Madhumuni ya maonyesha haya yalikuwa ni kuelezea ukubwa wa tatizo hili na ukatili wa wanawake nyumbani, ambapo kwenye mchezo huo ilionyeshwa mwanamke alivyouawa na hadithi ya "Mashahidi" bubu ilielezwa.

"Mashahidi bubu" ni mchezo ulioanzishwa huko Minnesota, nchini Marekani na sasa umesifika nchi nzima na kuwa sehemu ya kundi linalopigana ili kukomesha maovu haya dhidi ya wanawake. Maonyesho haya ya "Mashahidi bubu" yanafaa sana kwa mada hii ya uonevu dhidi ya wanawake ili kuweza kujadili suala hili kwenye sehemu unayoishi, kijijini, mjini au kwenye Mkoa wako. Kitabu kiitwacho, "Matokeo" kinaelezea tangu mwaka wa kwanza mkakati huu ulipoanzishwa nchini Marekani, na kuna mifano mingi inayoweza kutumiwa. Kwenye mtandao www.selentwitness.net kuna orodha ndefu ya kimataifa inayoonyesha sehemu ambazo maonyesho haya yamefanyika. mnawezakuigiza mfano wa mashahidi.

Ushahidi wa 1

Ushahihi wa 2

Ushahidi wa 3

Miongozo kwa ajili ya majadiliano yavikundi

IBARA YA TANO

HAKI ZA WATOTO

„Mtoto asiye na ujasiri ni kama Mbingu isiyokuwa na nyota“

Mada: Watoto, Haki za Binadamu, Elimu.

Utata/Ugumu: ngazi ya 2

Ukubwa wa kundi: idadi yoyote

Muda: dakika 60

Maelezo ya jumla: Zoezi hili linakusudia kuleta motisha ya majadiliano juu ya Azimio la Haki zaWatoto duniani likizingatia mada zifuatazo:

- Haki za Binadamu naHaki za Watoto kulingana na Azimio la Haki za Watoto Duniani.
- Wajibu na Uwajibikaji kulingana na Azimio hili
- Uwezekano wa kudai Haki hizi

Lengo:

- Haki ya kutambua Familia yako na kuishi nayo pamoja
- Haki ya kulindwa kutokana na unyonyaji wa kiuchumi
- Haki ya kupata msaada wa kutetewa kwenye kesi Mahakamani

Lengo/Shabaha:

- Kutangaza Azimio la Haki za Watoto Duniani
- kujifunza kutathmini habari na yale unayofundishwa kwa undani na kulinganisha ukweli huo na maisha halisi katika mazingara unayoishi
- Moyo wa kuwajibika, kupigania Haki, mshikamano, kuhamasisha na kudai Haki ya usawa.

Vifaa:

- Kila kikundi kipewe kadi ya kutoa maoni
- Karatasi kubwa ya gazeti la ukutani
- Kalamu za rangi
- Nafasi ya kutosha ili kila kundi liweze kufanya kazi peke yake

Matayarisho:

- Andika kwa ufupi Azimio la Haki za Watoto Duniani kwenye karatasi kubwa na kutengeneza gazeti la ukutani

- Toa maoni yako juu ya sentesi zilizoko kwenye kadi ya maoni (Uk. 184) kuhusu Azimio la Haki za Watoto. Fikiria ni kifungu gani kinaweza kupendeza kwa majadiliano kwenye kundi lenu. Ni hoja zipi zinaeleweka na ni zipi zinaleta utata kwenye majadiliano.
- Tayarisha kadi ya maoni yenye sentensikwa kila kundi. Weka kila sentensi hiyo ndani ya bahasha ili sentensi zisichanganyike.

Utangulizi:

1. Anza kwa kutoa maelezo mafupi kuhusu Azimio la Haki za Watoto Duniani. Uliza kama kuna wanayoyajua kuhusu Azimio hili. Zungumzia ibara muhimu kwa kutumia gazeti la ukutani.
2. Unda vikundi vidogo vya wanafunzi kati ya 3-4. Gawa bahasha zenye kadi za maoni.
3. Eleza juu ya „mbinu ya uwiano“:
   - Kila kundi dogo lijadili maelezo 9 na kufikiria ni vipi kila hoja inavyohusiana na maisha yake. Baadaye waweke hizo kadi moja baada ya nyingine katika umbo la almasi kulingana na umuhimu wake: - zenye maelezo muhimu ziwekwe juu; zile mbili zinazofanana ziwekwe chini, zifuate nyingine tatu zenye umuhimu wa wastani ziwekwe chini. Mstari wa nne utakuwa na kadi mbili, na mstari wa tano utakuwa na kadi moja ambayo ina umuhimu mdogo Zaidi. Kwa kufanya hivyo umbo la almasi litaundwa.
4. Wape muda wa dakika 25 ili wajadili na kukubaliana juu ya uwiano huo.
5. Mwisho wapite na kuangalia uwiano wa vikundi vingine. Baadaye wakutane wote kwenye kikao cha pamoja.

Maadalizi ya mwisho na Tathmini:

Kwanza vikundi vitawasilisha matokeo ya majadiliano yao. Kila mmoja atoe maoni yake jinsi alivyoipenda kazi na alichojifunza.

- Matokeo ya mijadala ya vikundi ikoje kwa kulinganisha na mijadala mingine. Je, kuna uhusiano upi na tofauti gani zilizopo?
- Kwa nini watu wanakuwa na hisia tofauti?
- Je, kuna kundi ambalo baada ya kusikia maoni ya kundi jingine, linataka kubadili msimamowake? Ni hoja zipi zimeweza kuwashawishi zaidi?
- Ni haki zipi ambazo hazizingatiwi katika sehemu unayoishi? Kwa nini?
- Je, kuna haki zozote unazodhani zinakosekana kwenye Azimio la Haki za Watoto?
- Je, unadhani watoto wanahitaji Azimio laowenyewe? Kwa nini?
- Kama unafikiri kuwa Azimio la Watoto ni muhimu, je ni bora kuwa na Azimio la Vijana wenye umri kati ya miaka 18-30?
- Unadhani nihaki zipi zinastahili kuwepo kwa vijana hao wenye umri wa miaka 18-30?
- Je, inawezekana kweli Haki za Watoto kuheshimiwa na kutimizwa?
- Ni vipi watu wanaweza kudai haki wanazostahili?

- Kama kushiriki kwenye Demokrasia ni uwezekano wa kudai haki yako mwenyewe, je unawezaje kudai haki yako nyumbani, shuleni au kwenye klabu yako ya michezo?
- Ni sehemu gani ambapo watoto wanaweza kukimbilia iwapo haki zao zitakuwa vimevunjwa?

Ilani kwa mwendesha mjadala:

Maelezo zaidi juu ya "***Uwiano wa Almasi***" yapo kwenye kifungu cha 1 (uk. 47***) "KOMPASS katika vitendo***". Waeleze washiriki wa vikundi kuwa hakuna mpangilio ulio sahihi au usio sahihi. Watambue kwamba kila mtu ana uzoefu tofauti na ndiyo maana kila mtu anacho kipaumbele kwa kitu anachoona kwake ni muhimu na hiki lazima kiheshimiwe.

Hata hivyo ni juu ya kila kikundi kiafikiane katika kutafuta mpangilio wake. Mwisho inabidi hata kwenye maisha ya kawaida kila mtu kujiwekea malengo, makubaliano na uamuzi kwa manufaa ya wote.

Njia nyingine:

Badala ya kufanya uwiano wa ibara hizo tisa, unaweza kutumia nane na kuacha kadi moja iliyo wazi. Kwa kufanya hivyo kundi litatafuta lenyewe ibara ya tisa.

Weka kadi hizo ndani ya mfuko na kumtaka kila mmoja wao achukue kadi moja na kuijadili kama dakika nzima. Kwenye zoezi liitwalo "Dakika moja" utakuta maelezo zaidi juu ya mbinu hii. Omba kundi lielezee hadithi fupi au maigizo mafupi juu ya tukio walilochagua. Njia nyingine wanaweza kueleza hadithi au mchezo wa kuigiza unaoelezea tukio fulani katika vyombo vya habari, filamu au maigizo, juu ya kitabu au gazeti. Mchezo huo wa kuigiza unaweza kufanyiwa marekebisho zaidi, kwanza kuonyesha tukio hilo na kutafuta njia ya kutatua tatizo hilo au njia ya kuzuia uvunjaji wa Haki za Binadamu ili usitokee tena.

Mapendekezo ya kazi ya baadaye

Mkaribishe mtu yeyote anayejua Azimio la Haki za Watoto Duniani ili atoe hotuba juu ya mada hii muhimu. Huyu anaweza kuwa mwendesha mashitaka ya umma, daktari wa watoto mwenye fani ya Saikologia, au wakili. Tafakari kwanza kwa ufupi juu ya Azimio hilo la Haki za Watoto, k.m. unyanyasaji wa watoto, kuzini na watoto wadogo, kutelekezwa kwa watoto bila mtu wa kuwahudumia na vitisho dhidi ya watoto. Mwulize huyo uliyemkarisha kutoa muhadhara ni nani anahusika na haki za watoto k.m. Wazazi, Polisi, Wafanyakazi wa Idara ya Ustawi wa Jamii, n.k. Omba ushauri ni nini kifanyike kama mtu ni shahidi wa matukio mabaya ya unyanyasaji wa watoto, k.m. jirani anapoona vitendo hivyo vya ukatili. Matatizo haya lazima yaendewe kwa taratibu, busara na kwa umakini sana.

Mara nyingi watoto na vijana hujisikia kama wanabaguliwa. Ikiwa vikundi vitataka kujadili kwa undani suala la Ubaguzi, vinaweza kuangalia zoezi liitwalo ***"wote ni sawa; yote ni tofauti".***

Mawazo ya utendaji

Angalia kwa makini katiba ya Serikali, katiba ya chama cha siasa na Mwongozo wa shule, halafu jiulize yafuatayo:

- Ni vipi shule inatimiza wajibu wake kuhusu Azimio la Haki za Watoto Duniani?
- Je, Elimu inayotolewa inatimiza madhumuni ya kukuza utu, akili na uwezo wa mwanafunzi au ni kujifunza tu kwa nia ya kushinda mtihani?
- Je, wanafunzi wanayo haki kutoa mawazo yao kwa mambo yote yanayowahusu wenyewe shuleni?
- Je, mawazo ya wanafunzi yanazingatiwa kweli?
- Kwa maana nyingine, kuna baraza la wanafunzi na lina ushawishi au majukumu gani katika masuala ya shuleni?
- Nidhamu ya shuleni iliyowekwa inaenda sambamba na haki za watoto?
- Je, shule inachukua hatua gani dhidi ya vitendo vya ubaguzi wa rangi na unyanyasaji?

  Jadiliana juu ya hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kutatua matatizo hayo hapo shuleni. Angali mifano iliyopo katika ukurasa wa 270 „Kushiriki kikamilifu“ na anzisha mradi huo. Angalia walimu wasiingilie kati kwenda kinyume na mradi wenu hasa wakiona mnajaribu kuingilia mamlaka yao.

Maelezo ya ziada

Nakala kamili ya Azimio la Haki za Watoto ambayo hutolewa kila mwaka na shirika la Umoja wa Mataifa la UNESCO kuhusu hali ya watoto duniani na vitabu vingine na makala mbalimbali kuhusu Haki za Watoto utazipata kwenye Chimbuko katika Ibara ya 5 yamaelezo ya kina juu ya watoto (Ukurasa 362).

Karatasi ya kazi

Kadi ya maoni

Nakili makala ifuatayo na kuikata, kisha ibandike kwenye kadi ya maoni.

Mtoto ana haki na uhuru wa kuwakilisha yale yanayomfaa. Maoni haya yanapashwa kufikiriwa. Pia ana haki na uhuru wa kutoa maoni yake.
Haki ya mtoto ya kutoa mawazo yake, dhamiri na uhuru wa kuamini dini yoyote lazima iheshimiwe. Mtoto anayo haki ya kujiunga na watu wengine na kukutana nao kwa Amani.
Hairuhusiwi kisheria kujiingiza katika maisha yake, ya familia yake, nyumbani kwake au maandishi yake. Ni lazima mtoto alindwe kutokana na mambo yasiyo ya kisheria ili kulinda heshima yake.

Jukumu kubwa la Wazazi ni kumpa mtoto Elimu na maendeleo.
Mtoto anayo Haki ya Elimu na malezi bora. Serikali inatoa elimu ya bure na hivyo kuifanya elimu kuwa ni lazima. Sheria za shule zizingatie Haki ya Binadamu. Madhumuni ya Elimu ni kuendeleza utu, kipaji na uwezo wa mtoto. Kuheshimu Haki na Uhuru wa Binadamu, ili kuishi kwa kuwajibika katika jamii huru, kwa roho ya akili na Amani, ya kuvumiliana, usawa wa kijinsia na kuheshimu mazingira ya asili.
Mtoto anayo Haki ya Uhuru na Amani, kucheza na kushiriki katika mambo ya kitamaduni na Sanaa.
Ni lazima mtoto kumlinda kutokana na unyonyaji wa kiuchumi, na asilazimishwe kufanya kazi ambazo zitadhuru maisha na maendeleo yake. Ni lazima mtoto alindwe kutokana na vitendo viovu vya kunajisiwa, umalaya, picha za uchi, na vitendo vingine vilivyo kinyume cha sheria.
Serikali inaazimia kufanya kila iwezalo ili kuwalindwa watoto kutokana na matatizo ya vita.
Ikiwa mtoto atatenda kosa kinyume cha sharia, lazima alindwe mpaka ithibitishwe mahakamani kuwa analo kosa au hapana. Anayo haki ya kutetewa na wakili wake, asilazimishwe kutoa ushahidi wowote, kuheshimu maisha yake ya binafsi kulingana na umri wake. Ikiwa mtenda makossa atakuwa bado hajafikia umri wa miaka 18, hawezi kuhukumiwa adhabu ya kifo au kifungo cha maisha bila uwezekano wa kumtoa kwenye kifungo hicho.

KITUO CHA NGUVU ZA UMEME

Kituo hiki cha umeme kinakusudia kufanya ubunifu wa Nishati

Mada: Amani na Vurugu, Ushiriki wa Kisiasa, Haki za binadamu

Utata: Ngazi ya 3

Ukubwa wa Kundi: washiriki 10 na zaidi

Muda: dakika 90

Maelezo ya jumla: Madaraka ya kutawala huhusishwa mara nyingi na vurugu. Zoezi hili litafanywa kwenye vikundi na kubuni yafuatayo:

- Vurugu katika kijiji chako
- Njia za kutatua vurugu hizi

Lengo:

- Haki ya Usalama wa kila mtu
- Haki ya kulindwa dhidi ya Ubaguzi
- Haki ya kuwa na faragha na kulinda heshima ya mtu

Lengo/Shabaha:

- Kutambua dalili za vurugu na kujua sababu au chanzo chake
- Kuendeleza ushirikiano, umoja na kazi za pamoja
- Kubuni njia za kukabiliana na vurugu na unyanyasaji

Vifaa:

- Kidanke kikubwa cha pamba na kamba yenye urefu wa chumba kizima
- Mkasi
- Karatasi ya ukubwa wa DIN-A4, Karatasi 6 kwa kila mtu
- Kalamu ya rangi kwa kila mtu
- Kengele (kama inapatikana)
- Mkanda wenye gundi ya kufungia

- Vyumba 2 (kama vitakuwepo)

Matayarisho:

- Tumia chumba kilichoko kwenye kituo cha umeme. Unahitaji nafasi katikati ya chumba hicho. Zungusha kamba toka sehemu moja hadi nyingine na kuifunga kwa kuikaza mwishoni. Weka waya wa umeme juu kiasi cha Mita moja toka chini. Usivute sana kwani unahitaji nafasi kwenye mfundo huo, ikiwa waya huo itabidi utengenezwe pakitokea matatizo ya umeme. Unaweza kuweka tangazo mlangoni lenye maandishi - "***KITUO CHA NGUVU ZA UMEME".***

Utangulizi: Zoezi hili liko kwenye sehemu mbili. Sehemu ya 1 ni kutafakari kwa ufupi juu ya dalili za vurugu (dakika 10). Sehemu ya 2 ni shguhuli huko kwenye Kituo cha nguvu za Umeme.

- *Sehemu ya 1. Kutafakari kwa ufupi juu ya dalili za Vurugu na Unyanyasaji.*

1. Kwa ufupi washiriki wajadili ni vipi vurugu hizi zinatokea kwenye kijiji chako, (shuleni, kwenye timu yako ya michezo, chuoni, sehemu unayoishi, n.k.). Eleza wazi kuwa hii si mada kubwa ya kujadiliwa kama Ugaidi au mauaji ya kikabila, bali ni vurugu zitendwazo kila siku kama uonevu, matusi, kukejeli na utani unaoumiza, n.k.
2. Washiriki watumie kalamu za rangi na kutumia herufi kubwa kuandika maneno na sentensi fupi, kila wazo kwenye karatasi moja.
3. Kusanya karatasi hizo na angalia kama maneno yamerudiwa, weka pembeni.
4. Wape muda wa dakika 5 hivi ya mapumziko na wakati huo wajitayarishe kwa sehemu ya pili inayofuata. Kunja karatasi hizo na kuzitundika juu ya waya wa umeme. Acha nafasi kama cm 50 toka karatasi moja hadi nyingine. Zifunge kwenye kamba hiyo kwa kutumia mkanda wenye gundi.

- *Sehemu ya 2: Kwenye kituo cha nguvu za umeme.*

1. Waalike washiriki waingie ndani kwenye kituo cha nguvu za umeme. Wawe kama wataalamu wanaofanya kazi kwenye kituo hiki.
2. Viundwe vikundi viwili

3. Waeleze kuwa Kituo hiki kinazalisha umeme mbaya. Kwa hali hiyo ndiyo sababu kunatokea matatizo ya uzalishaji wa umeme kwenye kituo hiki. Onyesha tatizo hili kwa kukata waya wa umeme sehemu mbili. Madhumuni ni kutafuta njia ya kutatua tatizo hili ili kupata umeme kwenye waya huo.

4. Waeleze kuwa mwanga unatikisika na kengele inagonga mara panapotokea tatizo la umeme. Kila panapotokea tatizo hili la kukatika kwa umeme, atoke mtu mmoja kwenye kikundi akimbie kuelekea kwenye waya. Achukue ncha hiyo iliyokatika na kuifunga tena pamoja ili umeme uweze kupita tena.

5. Kwa kutumia mkono ulio wazi fundi achukue karatasi iliyo karibu na sehemu iliyokatika na kusoma tatizo hilo ili kila mmoja asikie.

6. Sasa inabidi makundi hayo mawili yarekebishe tatizo hili. Wape dakika 5 ili kujadili jinsi ya kutatua tatizo hili.

7. Vikundi vijadili na kutoa maoni yake jinsi ya kutatua tatizo hili. Maoni haya yataandikwa kwenye karatasi mpya na kuwapatia mafundi.

8. Wataalamu watengeneze ili kumaliza tatizo hilo, ambapo wataunganisha waya hizo pamoja, na kufunga karatasi hiyo kwenye fundo hilo.

9. Tundika hizo karatasi za kutatua tatizo hilo ukutani.

10. Sasa kata waya huo tena sehemu nyingine na rudia jaribio hilo tena. Zoezi litamalizika ikiwa hapatakuwepo tena karatasi hizo zilizotundikwa kwenye waya wa umeme na badala yake kuwepo na zile karatasi za kutatua tatizo hilo.

11. Mwisho ondoa karatasi za majibu kwenye waya na kuzitundika ukutani.

Maandalizi ya mwisho na Tathmini

Anza kwa kurejea zoezi lililopita na kujadili jinsi ya kutatua tatizo hili.

- Washiriki walijisikiaje katika kufanya zoezi hili? Je, zoezi hili limependeza au la. Kwa nini?

- Ni sababu zipi zilisababisha tatizo hilo la vurugu?

- Je, njia zilizoshauriwa kwa ufumbuzi wa tatizo hilo ziliweza kusaidia? Kwa muda mfupi? Kwa muda mrefu?

- Ni matatizo gani yanaweza kutokea wakati mtu anatafuta ufumbuzi wa tatizo hilo?

- Ni vipi vijana wanaweza kuzuia, kukabiliana au kukomesha vurugu?

- Ni haki zipi za Binadamu zinavunjwa kutokana na vurugu hizi?

Ushauri kwa kiongozi wa Mjadala

Sehemu ya 1 ya kutafakari kwa ufupi juu ya dalili za Vurugu na Unyanyasaji inachukua kama dakika 10 na shughuli ya kwenye kituo cha nguvu za umeme inachukua kama dakika 60. Maandalizi ya mwisho na Tathmini vinachukua dakia 20.

Jaribu kumaliza zoezi hili haraka ili lisichukue muda mrefu. Kama kutahitajika maelezo ya ziada ni vipi jibu linapatikana kwa kutumia mawazo na itikadi (tz. No. 6 Utangulizi), unaweza kutumia mifano ifuatayo:

- Ikiwa kwenye karatasi kumeandikwa „Uonevu“ na nyingine „Vurugu kwenye Luninga-TV“, basi unaweza kupendekeza kikundi cha Warsha shuleni kiwepo. Watajifunza jinsi ya kupambana na uonevu, na kuongeza muda wa kuonyesha filamu kwenye luninga-TV kuanzia kama saa tano za usiku (ili watoto wawe wamekwisha lala).
- Kundi jingine litapendekeza kuanzisha mafunzo ya „Matatizo ya Uonevu“ kwa wanafunzi watakaokuwa kama wapatanishi na kushauri muda wa kuonyesha filamu zenye kuonyesha vitendo vya vurugu usogezwe mbele kuanzia saa tatu za usiku.
- Baadaye vikundi vitajadiliana juu ya mapendekezo haya, ongezea maoni mengine na kuandika kwenye karatasi ya majibu. Kila kundi linaweza kutoa mapendekezo mawili au zaidi, pia pendekezo moja linatosha.

Kwenye vikundi vidogo unaweza kuongezea kikundi kingine kiitwacho „Ufundi kwa ajili ya tahadhari“. Sababu ya kuunda vikundi viwili ni kuwa mara nyingi vikundivinaweza kubuni njia iliyo tofauti ya kutatua tatizo hilo. Hii inasaidia kupanua upeo na kutafuta njia za kutatua matatizo.

Mazoezi ya awali „Mashine ya Binadamu“ inafaa kwa kuwaunganisha washiriki pamoja. Njia hii husaidia kujua mada na matatizo yaliyopo na hivyo kutafuta ufumbuzi wake.

Mapendekezo ya kazi ya baadaye

Kwenye kituo cha nguvu za umeme yamejadiliwa masuala ya ubaguzi na ya jinsia. Kundi linaweza kutaka kujadili mada nyingine kama Utambulisho, Haki ya Usawa na Heshima. Pendekeza somo la „Mimi ni nani“.

Mawazo ya Utendaji

Ongelea kwa kina zaidi matatizo yaliyoelezwa kwenye zoezi hili. Ikiwa kundi litaamua kujadili juu ya mada ya Uonevu, basi wanaweza kuandaa warsha hapo shuleni na kuiweka kwenye agenda katika mkutano wa shule nzima.

Kumbukumbu: „Kituo cha nguvu za Umeme“ kimetayarishwa na Dariusz Grzemny wa Chama cha Watoto na Vijana, nchini Poland, Glogow.

Maigizo ya kutumia ishara (Pantomime)

Nieleze Haki za Binadamu zina maana gani kwako

Mada: Haki za Binadamu, Watoto, Kushiriki Kisiasa

Utata: Hatua ya 2

Ukubwa wa Kundi: 9 +

Muda: dakika 90

Maelezo ya jumla: Zoezi hili la maigizo linawachangamsha washiriki kwa:

- Kupima Mtazamo wao juu ya Haki za Binadamu
- Kutafuta njia mbalimbali za kuelezea mtazamo huu

Lengo/Shabaha:

- Haki zote za Binadamu

Lengo:

- Kutambua washiriki wanajua nini kuhusu Haki za Binadamu
- Kuendeleza uhusiano wa tamaduni mbalimbali na mawasiliano
- Kukuza ushirikiano na ubunifu

Vifaa:

- Vinavyohitajika: mavazi ya maonyesho, vitu vya kuchezea, vifaa vya nyumbani, n.k.
- Karatasi na rangi za kuchora, chaki
- Gundi, kamba na mfuko wa kubebea vitu

Utangulizi:

1. Eleza madhumuni ya zoezi hili: Kuelezea Haki za Binadamu kwa njia ya maonyesho kiasi kwamba watu wa makabila tofauti na lugha mbalimbali wanaelewa haki hizo.
2. Hairuhusiwi kutumia maneno yoyote. Maonyesho yote yafanyike kwa kutumia ishara peke yake. Vikundi vinaweza kutumia vifaa na vitu vilivyokusanywa kwa ajili hiyo.
3. Makundi ya watu kati ya 4-6 yataundwa. Kila kundi lichukue karatasi, chaki na kalamu ya rangi
4. Vikundi vitapewa kwanza dakika 10 za kutafakari, ili kukusanya mawazo yake juu ya Haki za Binadamu, na hatimaye kuamua mawazo muhimu kama mawili au matatu ambayo wataelezea.
5. Vikundi vipewe muda wa dakika 30 kutunga mchezo wao wa kuigiza na kufanya majaribio. Maonyesho hayo yawe ni matokeo ya kundi zima na washiriki wote wa kundi hilo wahusike katika kazi hii.
6. Baada ya dakika 30 vikundi vyote vitakutana pamoja ili wengine waone maonyesho ya kila kikundi.
7. Baada ya kila onyesho toa muda wa kujadili na kutoa maoni.
8. Watake washiriki wanaoangalia watoe maelezo yao na tafsiri yayale yaliyoonyeshwa kwenye jukwaa.
9. Baada ya hapo kundi linaloigiza linaweza kuongezea yale yaliyotolewa maoni ambayo hawakuyaonyesha hapo mwanzoni. Rudia hivyo hivyo kwa kila onyesho.

Mahali ambapo ni vigumu kuigiza igizo la nguvu umeme bustani ya mboga mboga inaweza kutumika kwa kuigiza

IBARA YA SITA

BUSTANI YA MBOGAMBOGA

(Aina za vurugu na namna ya kuzitatua)

Bustani hii ya mboga inakusudiwa kuboresha afya za watu

Mada: Amani na Vurugu, Ushiriki wa Kisiasa, Haki za binadamu

Utata: Ngazi ya 3

Ukubwa wa Kundi: Washiriki 10 na zaidi

Muda: dakika 90

Maelezo ya jumla: Madaraka ya kutawala huhusishwa mara nyingi na vurugu. Zoezi hili litafanywa kwenye vikundi na kubuni yafuatayo:

- Vurugu katika eneo
- Njia za kutatua vurugu hizi

Lengo:

- Haki ya Usalama wa kila mtu
- Haki ya kulindwa dhidi ya Ubaguzi
- Haki ya kuwa na faragha na kulinda heshima ya mtu

Lengo/Shabaha:

- Kutambua dalili za vurugu na kujua sababu au chanzo chake
- Kuendeleza ushirikiano, umoja na kazi za pamoja
- Kubuni njia za kukabiliana na vurugu na unyanyasaji ma shuleni

Vifaa:

- Kamba yenye urefu wa bustani nzima
- Mkasi
- Karatasi ya ukubwa wa DIN-A4, Karatasi 6 kwa kila mtu
- Kalamu ya rangi kwa kila mtu

- Mkanda wenye gundi ya kufungia
- Bustani ya mboga mboga na eneo la mjadala
- Mfereji wa kusambaza maji bustanini
- Mambo 12 (8 za kubandika matatizo; na 4 za kamba kwa ujumla).
- Kamba
- Maji ya kumwagilia
- Ndoo
- jembe

Matayarisho:

- Tumia chumba kilichoko kwenye Bustani ya Mboga. Unahitaji nafasi katikati ya chumba hicho. Zungusha kamba toka sehemu moja hadi nyingine na kuifunga kwa kuikaza mwishoni ikiwa imefungwa juu ya miti iliyosimikwa. Unaweza kuweka tangazo lenye maandishi ***"BUSTANI YA MBOGAMBOGA".***

Utangulizi:

Zoezi hili liko kwenye sehemu mbili. Sehemu ya 1 ni kutafakari kwa ufupi juu ya dalili za vurugu shuleni (dakika 10)

. Sehemu ya 2 ni shughuli huko kwenye Bustani ya Mbogamboga

- **Sehemu ya 1:**

Kutafakari kwa ufupi juu ya dalili za Vurugu na Unyanyasaji .

5. Kwa ufupi washiriki wajadili ni vipi vurugu hizi zinatokea kwenye kijiji chako, (shuleni, kwenye timu yako ya michezo, chuoni, sehemu unayoishi, n.k.). Eleza wazi kuwa hii si mada kubwa ya kujadiliwa kama Ugaidi au mauaji ya kikabila, bali ni vurugu zitendwazo kila siku kama uonevu, matusi, kukejeli na utani unaoumiza, n.k.

6. Washiriki watumie kalamu za rangi na kuandika kwa herufi kubwa maneno na sentensi fupi, kila wazo lionyeshayo vurugu zinazotokea kila mara kwenye kijiji chetu, shuleni, nyumbani, njiani kutoka shuleni waandike kwenye karatasi moja.

7. Kusanya karatasi hizo na angalia maneno yaliyorudiwa, weka pembeni.

8. Wape muda wa dakika 5 hivi ya mapumziko na wakati huo wajitayarishe kwa sehemu ya pili inayofuata. Kunja karatasi hizo na kuzitundika juu ya **mambo** zilizochomekwa kwenye kikwazo. Zifunge kwenye kamba hiyo kwa kutumia mkanda wenye gundi.

- **Sehemu ya 2:**

Kwenye Bustani ya Mbogamboga.

12. Waalike washiriki waingie ndani kwenye Bustani ya Mbogamboga. Wawe kama wataalamu wa kilimo wanaofanya kazi kwenye bustani hii.

13. Viundwe vikundi viwili

14. Waeleze kuwa bustani hii haistawishi mbogamboga ipasavyo. Kwa hali hiyo ndio sababu kunatokea matatizo ya uzalishaji wa mbogamboga katika bustani hii, mboga haistawi vizuri. Onyesha tatizo hili kwa kuweka kikwazo cha maji katika mfereji wa maji yaelekeayo bustanini. Madhumuni ni kutafuta njia ya kutatua tatizo hili ili maji yapite kwenye mfereji na kuufikia kila mmea bustanini.

15. Waeleze kuwa maji yanakwama mara kinapotokea kikwazo. Kila panapotokea tatizo hili la kukwama kwa maji, atoke mtu mmoja kwenye kikundi akimbie kuelekea kwenye mfereji na kutoa taarifa kuwa maji yamekwama.

16. Kwa kutumia mikono yake mtaalam achukue karatasi iliyo karibu na sehemu maji yalipokwama na kusoma tatizo hilo ili kila mmoja asikie.

17. Sasa inabidi makundi hayo mawili yarekebishe tatizo hili. Wape dakika 5 ili kujadili jinsi ya kutatua tatizo hili.

18. Vikundi vijadili na kutoa maoni yao jinsi ya kutatua tatizo hili. Maoni haya yataandikwa kwenye karatasi mpya na kuwapatia wataalamu.

19. Wataalamu waondoe kikwazo ili kumaliza tatizo hilo, ambapo wataondoa udongo (watazibua) katika mfereji, na kufunga karatasi hiyo kwenye mambo iliyopo eneo hilo.

20. Tundika hizo karatasi za kutatua tatizo hilo kwenye kamba.

21. Sasa ziba mfereji tena kwenye eneo linalofuata sehemu nyingine na urudie jaribio hilo. Zoezi litamalizika ikiwa hapatakuwepo tena karatasi hizo zilizotundikwa kwenye mambo (karatasi zenye matatizo) na badala yake kuwepo na zile karatasi za kutatua tatizo hilo.

22. Mwisho ondoa karatasi za majibu kwenye mambo na kuzitundika kwenye kamba.

Maandalizi ya mwisho na Tathmini

Anza kwa kurejea zoezi lililopita na kujadili jinsi ya kutatua tatizo hili.

- Washiriki walijisikiaje katika kufanya zoezi hili? Je, zoezi hili limependeza au la. Kwa nini?
- Ni sababu zipi zilisababisha tatizo hilo la vurugu?
- Je, njia zilizoshauriwa kwa ufumbuzi wa tatizo hilo ziliweza kusaidia? Kwa muda mfupi? Kwa muda mrefu?
- Ni matatizo gani yanaweza kutokea wakati mtu anatafuta ufumbuzi wa tatizo hilo?
- Ni vipi vijana wanaweza kuzuia, kukabiliana au kukomesha vurugu?
- Ni haki zipi za Binadamu zinavunjwa kutokana na vurugu hizi?

Ushauri kwa kiongozi wa Mjadala

Sehemu ya 1 ya kutafakari kwa ufupi juu ya dalili za Vurugu na Unyanyasaji inachukua kama dakika 10 na shughuli ya kwenye Bustani ya Mbogamboga inachukua kama dakika 60. Maandalizi ya mwisho na Tathmini vinachukua dakika 20.

Jaribu kumaliza zoezi hili haraka ili lisichukue muda mrefu. Kama kutahitajika maelezo ya ziada ni vipi jibu linapatikana kwa kutumia mawazo na itikadi (tz. No. 6 Utangulizi), unaweza kutumia mifano ifuatayo:

- basi unaweza kupendekeza kikundi cha Warsha shuleni kiwepo. Watajifunza jinsi ya kupambana na uonevu, na kuongeza muda wa kuonyesha video,
- Kundi jingine litapendekeza kuanzisha mafunzo ya „Matatizo ya Uonevu“ kwa wanafunzi watakaokuwa kama wapatanishi na kushauri muda wa kuonyesha video zenye kuonyesha vitendo vya vurugu.
-
- Baadaye vikundi vitajadiliana juu ya mapendekezo haya, ongezea maoni mengine na kuandika kwenye karatasi ya majibu. Kila kundi linaweza kutoa mapendekezo mawili au zaidi, pia pendekezo moja linatosha.

Kwenye vikundi vidogo unaweza kuongezea kikundi kingine kiitwacho „Ufundi kwa ajili ya tahadhari“. Sababu ya kuunda vikundi viwili ni kuwa mara nyingi vikundivinaweza kubuni njia iliyo tofauti ya kutatua tatizo hilo. Hii inasaidia kupanua upeo na kutafuta njia za kutatua matatizo.

Mazoezi ya awali „Mashine ya Binadamu“ inafaa kwa kuwaunganisha washiriki pamoja. Njia hii husaidia kujua mada na matatizo yaliyopo na hivyo kutafuta ufumbuzi wake.

Mapendekezo ya kazi ya baadaye

Kwenye Bustani ya Mbogamboga yamejadiliwa masuala ya ubaguzi na ya jinsia. Kundi linaweza kutaka kujadili mada nyingine kama Utambulisho, Haki ya Usawa na Heshima. Pendekeza somo la „Mimi ni nani“.

Mawazo ya Utendaji

Ongelea kwa kina zaidi matatizo yaliyoelezwa kwenye zoezi hili. Ikiwa kundi litaamua kujadili juu ya mada ya Uonevu, basi wanaweza kuandaa warsha hapo shuleni na kuiweka kwenye agenda katika mkutano wa shule nzima.

Kumbukumbu:

Bustani ya Mbogamboga“ imetayarishwa na Sr.Felista na wanafunzi wa SAUT kwa kushirikiana na Prof.Dr.Margit Stein na Daniella Steenkamp wa Vechta Ujeruman

Tarehe Muhimu: **Maandalizi ya mwisho na Tathmini**

10. **December:** Angalia zoezi hili.

(Siku ya Haki za Binadamu)

- Washiriki walijisikia vipi wakati wanafanya zoezi hili? Zoezi lilikuwa rahisi au gumu? Ni kitu gani kilikuwa kigumu kwa maonyesho?
- Je, kuna jambo jipya ambalo washiriki wameweza kujifunza?
- Ni wapi washiriki wamekubaliana na wapi wametofautiana? Je, kulikuwepo tofauti ya mawazo kuhusu Haki za binadamu? Kwa nini?

Ushauri kwa kiongozi wa Mjadala

Ikiwa washiriki hawatakuwa wanafahamu yaliyomo kwenye Azimio la Haki za Binadamu, ni vizuri kiongozi wa mjadala asijiingize sana kwenye zoezi hili. Haja kubwa ni kuwafahamisha vijana wajue Haki za Binadamu ambazo ni muhimu katika maisha yao. Ni bora kama suala hili litajulikana kabla ya kuanza kazi hii ili kila mmoja ajue ni nini Haki za Binadamu.

Eleza wazi Haki za Binadamu zinakusudia nini. Unaweza kueleza haki mojawapo kama mfano, na baadaye kuelezea haki mbalimbali jinsi zinavyohusiana. Mwisho washiriki wawe na uwezo wa kujibu swali, „ni nini Haki za Binadamu“.

Usiruhusu wale wanaodhani hawawezi kufanya vizuri kwa maonyesho ya kuigiza wakae pembeni na kuangalia tu! Waeleze kuwa kila mmoja ana wajibu wa kushiriki kwani hii ni kazi ya kila mmoja katika kundi lao. Maigizo na vifaa vilivyo vya nadra kwenye sehemu hiyo vinaweza kuwa kivutio kikubwa na kufanya maonyesho yapendeze, - k.m. kikaango, vifaa vya kuchezea walivyotengeneza wao wenyewe – mkuki, ngao, mpira wa nyasi, kofia, kisu, jiwe, n.k.

Njia nyingine

Fanya kazi nyingine toka zoezi hili kwa kutumia mchoro. Vikundi vichore mchoro kwenye bango bila kutumia maneno yoyote – wakieleza mawazo yao kuhusu Haki za Binadamu. Zoezi kama hili linasaidia sana kuwafanya vijana kufikiri na kugundua wenyewe masuala mengi na jinsi ya kuyatatua.

Mapendekezo ya kazi ya baadaye

Angalia makala yoyote inayohusu Haki za Binadamu na tayarisha maonyesho haya katika kijiji chako. Ikiwa vikundi vitapenda kuendelea kufanya kazi juu ya mada yoyote kuhusu Haki za Binadamu, basi wanaweza kufanya zoezi la „Haki za Watoto“ na „Azimio la Haki za Watoto Duniani“

Mawazo ya Utendaji

Unaweza kufikiria jinsi ya kuendeleza maigizo hayo na hata kuyaonyesha kwa watu wote. Unaweza kutayarisha mabango na kufanya maonyesho makubwa. Yote yanafaa kwa sikukuu ya Haki za Binadamu.

HAKI – Bingo!

Tunafahamu nini kuhusu Haki za Binadamu?

Mada: Haki za Binadamu, Watoto, Usalama wa binadamu

Utata: Hatua ya 1

Ukubwa wa kundi: 8+

Muda: dakika 10

Maelezo ya jumla: Hili ni jaribio jepesi na aina nyingine ya mchezo wa Bingo. Ni juu ya maarifa na uzoefu wa Haki za Binadamu

Lengo/Shabaha: Haki zote za Binadamu

Lengo:

- Kutambua kuwa Haki za binadamu zinahusu kila mtu na kila mahali
- Kujifunza kusikiliza
- Kukubali na kuheshimu maoni ya watu wengine

Vifaa:

- Nakala ya jaribio na kalamu kwa kila mtu
- Bango la karatasi na kalamu ya rangi

Matayarisho:

- Hamishia hiyo nakala ya jaribio kwenye karatasi au bango kubwa la karatasi
- Zingatia Haki za msingi (Uk. 402) na Azimio la Haki za **Watoto (uk. 407).**

Utangulizi:

1. Gawa Nakala za jaribio hili pamoja na kalamu
2. Washiriki wote kila mtu atafute mwenzake na kumwuliza swali. Jibu liandikwe kwenye nafasi inayostahili kwa maneno machache
3. Baadaye watabadilisha na kutafuta mtu mwingine
4. Haja kubwa si kutafuta jibu tu bali kila swali lijibiwe na mtu mwingine
5. Yule ambaye atajaza nafasi zote na kumaliza atasema “Bingo”! Huyu pamoja na mwenzake watakuwa washindi.
6. Sasa nenda kwenye hatua ya mjadala. Soma swali katika mstari wa kwanza na uliza jibu. Andika maneno hayo kwenye ubao. Unaweza kuruhusu maoni machache.
7. Baada ya kujaza nafasi zote, anza kujadili majibu yote kwa kirefu tangu mwanzo.

Mazungumzo na Tathmini

- Je maswali yote yalihusu Haki za Binadamu? Ni zipi?
- Ni maswali yapi yalikuwa magumu? Kwa nini?
- Ni maswali yapi yalikuwa na utata? Kwa nini haki zina utata?
- Ni wapi au vipi washiriki wamepata taarifa kuhusu Haki za Binadamu? Je, unaamini taarifa hizi walikozipata?

Ushauri kwa kiongozi wa Mjadala

Unaweza kubadili maswali yote ili yalingane na uwezo na maslahi ya washiriki. Unahitaji tu kuandika maneno pale unapoandika majibu. Mchoro unasaidia tu kama kumbukumbu kwa majadiliano ya baadaye. Baada ya mzunguko uliza maswali au tafsiri yake. Weka alama pale mlipojadili ili kuweza kurudia tena hapo baadaye.

Bila shaka mifano kadhaa itatajwa ambayo huijui au chimbuko lake ni la binafsi. Hiyo si kitu. Hakuna anayeweza kujua kila kitu. Uliza washiriki wamepata wapi taarifa fulani na jadiliana juu ya uhakika na ukweli wake. Hii ni njia nzuri ya kuwafanya washiriki wajadili mambo kwa kina na kwa uangalifu mkubwa.

Baadhi ya majibu yataleta utata fulani. Mwingine atasema kutoa mimba ni ukiukaji wa haki za binadamu. Baadhi ya washiriki watapinga wazo hili na wengine watalikubali. Jambo la muhimu ni kwanza kujifunza kwa nini fulani ana maoni tofauti. Kila mada iangaliwe kwa mitazamo mbalimbali, na kutoa sababu juu ya maoni yake. Kila mara kunatokea maoni tofauti juu ya maslahi na haki mbalimbali (hapa ni kati ya maslahi na haki za Mama na mototo ambaye hajazaliwa). Pamoja na tofauti zinazoweza kutokea na tafsiri yake, ni wajibu wa kila mtu kuheshimu maoni ya mwingine. Maoni ya mtu yanaweza kukataliwa, lakini heshima yake lazima itunzwe.

Pili tunajifunza kwamba ni vizuri kuzifahamu Haki za Binadamu kwani zina utata mkubwa. Haikuelezwa na kukubalika kwa kauli moja ni vipi haki hizi zitafsiriwe na kutekelezwa, bali ni lazima zijadiliwe kila mara na kuendelezwa. Kwa hiyo kila mtu anao wajibu wa kukuza na kulinda Haki za Binadamu.

Mapendekezo ya kazi ya baadaye

Chagua jibu moja au mawili ambayo yameleta utata na jadili kuhusu maendeleo ya utamaduni yanayohimiza kuheshimu Haki za Binadamu. Mada hii ya Haki za Binadamu inaweza kuelezwa kwa kutumia picha. Zoezi liitwalo “Je unaona nini?” kwenye ukurasa wa 89 linasaidia kujua mawazo ya mtu kuhusu Haki za Binadamu. Zoezi hili linaweza kusababisha mjadala mkali k.m. kuhusu ubaguzi, juu ya mtazamo na itikadi mbalimbali Ulimwenguni, n.k.

Karatasi ya kazi

Jaribio – Karatasi ya maswali

Kichwa cha habari chenye hati inayotangaza Haki za Binadamu	Haki ya muhimu kwa watoto wote	Mashirika yanayofanya kazi pamoja na Msalaba Mwekundu au Shirika la Nusu Mwezi
Haki ambayo baadhi ya watu wananyimwa kwenye nchi yao	Haki ya Binadamu ambayo wewe mwenyewe umenyimwa	Shirika au Taasisi inayopigania Haki za Binadamu
Wajibu wetu kuhusu Haki za BInadamu	Mfano wa Ubaguzi	Haki ambayo baadhi ya wanawake wananyimwa
Mtu ambaye anapigania Haki za Binadamu	Kuvunja moja ya Haki ya kuishi	Mfano ambapo Haki ya faragha inavunjwa

KICHWA CHA HABARI

"Kusambaza Habari ni kuzidisha Habari"

Mada: Vyombo vya Habari

Utata: Hatua ya 3

Ukubwa wa Kundi: 10 - 24

Muda: Dakika 180

Maelezo ya jumla: Hii ni motisha: Kundi la watangazaji wa habari watatayarisha kichwa cha ukurasa wa gazeti tayari kwa kuchapishwa. Mada zifuatazo zitajadiliwa kwenye vikundi vidogo:

- Chuki, maneno matupu na usawa katika vyombo vya habari
- Picha na wajibu wa Vyombo vya Habari katika kuchambua Haki za Binadamu

Lengo/Shabaha:

- Haki ya Mawazo, Maoni, na Uhuru wa kujielezea
- Haki ya kuwa na faragha
- Haki ya Maendeleo, Maisha na Afya

Lengo:

- Maslahi juu ya Haki za Binadamu kwa kutumia kazi na picha
- Mjadala mkubwa na vyombo vya habari - jinsi vinavyojihusisha na matatizo ya Haki za Binadamu
- Kujifunza mawasiliano na ushirikiano

Vifaa:

- Chumba kikubwa ambamo vikundi kama 2 au 3 pamoja na kundi zima la mjadala vinaweza kukutana pamoja.
- Picha 40 toka kwenye magazeti
- Karatasi na kalamu
- Karatasi kubwa (DIN A3) au karatasi ya bango na kalamu za rangi
- Mkasi na gundi kwa kila kikundi
- Meza yenye nafasi ya kutosha ya kufanyia kazi, kiasi kwamba vikundi vyote vinaweza kuweka kazi zake mezani ili ziweze kuonekana kwa kila mtu.

Matayarisho: Chagua picha kama 40 – 45 hivi toka kwenye magazeti. Kila kikundi kidogo kinahitaji picha 40. Kwa hiyo unahitaji nakala

nyingi toka kila Gazeti au itabidi utoe nakala kwa kutumia mashine ya kuchapisha karatasi.

- Weka nakala ya picha kwenye meza.

Utangulizi:

1. Elezea juu ya zoezi hili. Eleza kwamba jioni wahariri wa habari watakutana ili kuzungumzia juu ya kichwa cha habari tayari kutoa gazeti hilo siku ifuatayo. Hili ni gazeti la kata/mtaa au kijiji chako, ambapo kila gazeti linapenda kumtaarifu kila mtu juu ya mambo muhimu yanayotokea hapo kijijini na ulimwenguni pamoja na suala la Haki za binadamu.
2. Vifanywe vikundi kama 8 hivi. Kila kikundi kifikirie kuwa ni timu ya wanahabari wanaoshughulikia gazeti moja. Kazi yao ni kubuni na kupangilia jinsi ya gazeti hili linalotoka kesho litakavyofanana.
3. Kila kundi litafute jina la gazeti lake.
4. Zungumza kwenye kundi la pamoja ni vipengele vipi na mpangilio upi unakuwepo kwenye kichwa cha habari cha gazeti la kawaida.
5. Waonyeshe wahariri hizo picha mlizoweka mezani. Wapite na kuangalia picha hizo zilizowekwa mezani bila kutoa maoni yoyote. Waeleza kuwa wanatakiwa kufanya kazi na picha hizi, ambazo wanaweza kuzitumia kwa kufikiria wao wenyewe na kutoa rai zao.
6. Baada ya hapo vikundi zitaanza kufanya kazi peke yao. Gawa vifaa hivyo yaani karatasi, gundi, mikasi, lakini usigawe kwanza picha.
7. Wape maelekezo kwanza. Kila kundi litapewa muda wa nusu saa, wachague taarifa kama 4-5 hivi kuandika kichwa cha habari, kuchagua picha na kufikiria mpangilio wa habari utakavyokuwa. Wasiandike makala ndefu. Kichwa cha habari na mistari michache inatosha kabisa. Badala ya kuandika taarifa nzima wajadili athari ya kichwa cha habari. Wape maoni yako kuwa kwanza wajadili ni mada zipi na matatizo gani yaandikwe kwenye gazeti hili. Waeleze kuwa baada ya dakika kumi picha za wahariri wa habari zitafika.
8. Baada ya kila kikundi kufanya kazi kwa dakika kumi, wape kila kundi picha kadhaa.
9. Baada ya kurasa zote kukamilika, zitawekwa mezani ili kila mtu aweze kuzisoma. Baada ya hapoyatafuata maandalizi ya mwisho natathmini.

Maandalizi ya mwisho na Tathmini

Anza na mazungumzo ya zoezi lenyewe na kujadilijuu ya vyombo vya habari, matatizo ya Haki za Binadamu na dhamira za msuala mbali mbali.

- Ni vipi vikundi vimeandaa kazi yake? Wameamua vipi juu ya kuendesha kazi zake na ni taarifa zipi watazichapicha? Je, wote wameweza kushiriki na kuchangia chochote kwenye kazi hii?
- Je, ni vipi wamechagua hizo mada au matatizo waliyoyagusia? Lipi lilitangulia, mada au picha? Yaani wametangulia kutafuta mada na baadaye kuchagua picha inayohusu mada hii au wamechagua picha yoyote iliyowapendeza na kuanza kuandika makala juu yake?
- Ni mada zipi zimechaguliwa ziandikwe kwenye gazeti hili? Kulikuwepo moja inayohusu Haki za Binadamu? Kuna mada ambayo mtu alitaka iwekwe lakini imebidi iachwe?
- Kichwa cha habari kinaonekana vipi ukilinganisha na magazeti mengine? Je, wametumia madana picha zinazofanana au hapana?
- Je, kuna vikundi vingi vilivyotumia picha inayofanana lakini kwa namna tofauti?
- Je, watu wanafuatilia vipi taarifa za habari, kwenye magazeti, kwenye luninga (TV), kwenye Radio au kwenye mtandao (Internet)? Kwa nini unafuatilia au hufuatilii taarifa za habari?
- Je, washiriki walikuwa na picha halisi walipofikiria kichwa hicho cha habari? Au walikuwa na picha nyingine kwenye fikira zao? Ni tofauti zipi zilikuwepo?
- Ni aina gani ya taarifa za habari inatawala kwenye vyombo vya habari?
- Je, matatizo ya Haki za Binadamu yanazungumziwa vya kutosha kwenye vyombo vya habari?
- Moja ya swali kubwa linaloulizwa juu ya vyombo vya habari ni usawa na ukweli wa matangazo. Je, kwa kauli ya washiriki inawezekana matagazo yakafanyika kwa kuzingatia usawa na ukweli?
- Je,ni mada zipi za Haki za Binadamu umeziweka kwenye kichwa cha habari?
- Ni picha zipi za vijana zinatawala kwenye sehemu nyingine za ulimwengu?
- Kuna mada ya muhimu inakosekana kwenye picha hizi?

Ushauri kwa kiongozi wa Mjadala

Katika kuchagua ni picha zipi zitumike kwenye zoezi hili, ni muhimu kuwa makini kwa wingi wa picha na kujaribu kuepuka ubaguzi. Taarifa nyingi za habari zinaelezea juu ya maafa, vita, vifo nawala hakuna taarifa iliyo nzuri (K.m. Afrika zinaonyeshwa picha za vita tu na balaa la njaa). Wape fursa timu ya waandishi wa habari ili badala ya picha zenye taarifa mbaya wachague picha zenye taarifa nzuri na za kupendeza. Zingatia mgawanyo mzuri wa kijiografia na usawa wa kijinsia, picha za vijana na vitu ambavyo ni muhimu katika maisha yao, ikiwemo picha nzuri zinazoonyesha jinsi ya kubadili mambo na kuwa mazuri. Chagua

picha zenye matukio ya wakati huu, zenye kuonyesha utu na zinazoonyesha maisha yalivyo kwenye tamaduni mbalimbali na mada zinazohusu mambo ya kimataifa.

Orodha ifuatayo inayo mambo ya kusisimua (inahusu orodha ya picha zilizoko kwenye zoezi la “Kiwanda cha Habari” na imeandikwa chini ya “Namna nyingine”):

Mwanamke Mtangazaji wa habari Ramani ya kudia Kundi la wapiga picha kwenye nchi za “kusini” mwa dunia Wanawake wanajenga bwawa Msaada kwa mkosefu wa ajira Wachimba migodi wa kiafrika Dawa ya kuulia wadudu Tangazo la chakula cha haraka Ardhi iliyokauka Watoto wanaocheza majini Kusafisha gari Kuchoma mafuta Hatu za Greenpeace Wingu la moshi toka viwandani Matangazo ya pombe Matangazo ya Coca-Cola	Mama mchuuzi wa bandarini Soko barani Asia Mwanamke mpweke Makazi duni Ngara Wingi wa takataka Polisi Michoro Bunge Bangi Kambi ya wakimbizi Watoto waishio kweye kambi ya wakimbizi Mchezo wa mpira Jaribio la Chama cha kupigania Haki za Binadamu (Amnesty International)	Maandamano Philippine Jeshi la Umoja wa Mataifa Jugoslawia Ndege za kivita Wapiganaji wa msituni Askari wawili waliokufa Magunia ya nafaka yaliyorundikwa Mkutano wa akina mama Uzazi wa mpango Kuzuia Ukimwi Kundi la watu Usafiri wa mabasi ya Umma Maonyesho ya magari Jam ya magari barabarani Kijana na kipaza sauti Simu ya mkononi

Kwenye kuanzisha mjadala na kuelezea juu ya makala inavyostahili kuwa, eleza ni vipi vichwa vya habari vinatakiwa kuandikwa na vipi hadithi nzima inatakiwa kuwasilishwa. Kwanza ni kuandika ufupisho wa yale ya muhimu halafu taarifa nzima. Zungumzia jinsi picha zinavyotakiwa kutumika ili kuvuta umakini wa wasomaji. Zungumzia pia yale ambayo picha hazionyeshi. Zungumzia pia jinsi ya kukata picha, ili kuvutia macho ya mtazamaji, na kile mpiga picha anachotaka kuonyesha. Jadiliana ni maelezo yapi yawekwe chini ya hiyo picha.

Njia nyingine

Badala ya zoezi hili unaweza kuonyesha taarifa ya habari kwenye radio au luninga (TV). Kwa kutumia lungina tunashauri kutumia “slide” za filamu kwenye chumba chenye giza, ili kutoa hisia ya luninga. Kuna slides ambazo zimetengenezwa kwa ajili hii. Zinaweza kuazimwa toka Shirikisho la Ulaya la Utamaduni na Elimu - EFIL

Mapendekezo ya kazi ya baadaye

Jadili hoja mojawapo kuhusu haki mbalimbali kwa ajili ya taarifa ya habari. Je, hoja hizi zinajadilia vipi nchini wako? Washiriki wanaweza kuwasiliana na gazeti litolewalo katika sehemu unayoishi, kituo cha Radia au kituo cha luninga (TV). Jadili na watangazaji wa habari juu ya kazi yao, jinsi wanavyotoa matangazo yao kwa usawa na kwa ukweli, na ni vipi suala la kimataifa la Haki za Binadamu linatangazwa katika vyombo vya habari. Endapo kundi litaweza kufikiria haraka na kufurahia mada hizi, wanaweza kuanza zoezi jingine liitwalo "Dakika moja tu". Zoezi hili linahusu uhusiano uliopo kati ya Michezo na Haki za Binadamu.

Mawazo ya Utendaji

Yawezekana baadhi ya vituo vya matangazo ya Radio vikakubali vikundi vyenu kutoa matangazo yake kwa kutumia vyombo vyao. Mnaweza kuanzisha mradi wa kundi lenu: Fanya uchunguzi na kutoa matangazo juu ya mada inayohusu kundi lenu, kwa mfano: "fikiria kimataifa tenda kitaifa".

Taarifa nyingine

Kutafakari mada zilizozungumziwa kwenye mazoezi yenu:

(a) Vyombo vya Habari

1. Kama ilivyo kwa watu wazima, vijana nao wanajishughulisha sana na matokeo katika vyombo vya habari. Tungeweza kujiuliza: Tuelewe vipi taarifa hizi? Je, kweli tumepata taarifa za kutufaa?
2. Siku hizi vyombo vya habari vimezidi kuwa vya kibiashara. Urahisi wa kutoa matangazo ya kijuujuu, yenye ubaguzi, na yenye kulenga misisimko yanatupa wasiwasi mkubwa. Inakuwa vigumu kupata mtangazo ya kina naya ukweli!
3. Jambo la muhimu ni kutoa matangazo mazuri, yenye ukweli, yanayohusu kutokuwepo na usawa, na hasa inapohusu nchi ambazo bado hazijaendelea. Taarifa za habari kuhusu nchi ambazo hazijaendelea zinaelezwa na vyombo vya habari toka nchi za magharibi (Ulaya). Matokeo haya ni mabaya naya kuonea kwani hayatangazi yale ya ukweli.

(b) Mada za Haki za Binadamu

Vyombo vya Habari ni muhimu sana, vinaeleza umma masuala yahusuyo Haki za Binadamu. Lakini ni lazima vizingatie jinsi mada hizo zinavyoelezwa na kwa nini. Ni juu yetu kuwa makini na kuchunguza vizuri hizo taarifa zinazoletewa, zina ukweli gani ndani yake. Kwa mfano wapiganaji wa vita wataelezwa kufuatana na mwelekeo

wa siasa kwenye gazeti fulani kuwa ni wapiganaji wa ukombozi, na kwenye gazeti jingine kuwa ni magaidi. Ili kuwafanya watu waamini mawazo haya, utakuta kundi la watu fulani wanaitwa “wendawazimu”. Kwa mfano kabila fulani litaitwa ni la kijasiri, ikiwa linapigania haki zake za kulinda utamaduni wake (k.m. Wamasai). Lakini kama kabila hilo hilo litahusishwa na uwindaji (k.m. wanyama wa porini), basi litaitwa “kabila la wauaji”

(c) Dhamira

Baadhi ya picha zionyeshe jinsi vijana wanavyojitolea kwa masuala mbalimbali. Wewe kama mwalimu au mfanyakazi wa idara ya jamii ni wajibu wako kuwapa vijana motisha ili wapiganie dunia yenye usawa. Tujiulize, tunaweza kutimiza vipi azima hiina tufikirie kama mambo tunayowapa vijana yanawasaidia na kuwatosha. Pengine jibu litapatikana kwa zile “slides” watakazochagua wenyewe.

IBARA YA SABA

MAISHA YETU YA BAADAYE

Maendeleo yetu hayapimwi kwa wingi wa utajiri tulionao, bali kama tunawapa cha kutosha wale wasiokuwa nacho. *Franklin D. Roosevelt*

Mada: Watoto, mazingira, Haki za Binadamu

Utata: Hatua ya 3

Ukubwa wa kundi: 15 – 20

Muda: Dakika 60

Maelezo ya jumla: Washiriki wa zoezi hili wanaandika, wanauliza na kujadili matumaini na hofu juu ya maisha ya kizazi kijacho.

Mada za kujadiliwa ni:

- Suala la mazingira, linalohusu kizazi kijacho
- Vijana na familia
- Maisha katika sehemu unayoishi

Lengo/Shabaha:

- Haki ya kutoa maoni yako na kupata maoni na taarifa za habari
- Haki ya kupata msaada wa kujiendeleza kwa ustawi wako
- Haki ya kuishi maisha yanayomstahili binadamu

Lengo:

- Kujadili juu ya maisha ya hapo kijijini, juu ya haki na wajibu.
- kujifunza juu ya kujadili kiuwazi, kufanya kazi pamoja kama timu na kuendeleza mawazo ya baadaye.
- Kuiona dunia kama fursa nzuri ya kuleta maendeleo, ambapo vijana wanategemewa kutoa mchango wao.

Vifaa:

- Karatasi za mchoro
- Karatasi kubwa zenye alama
- Rangi
- Kalamu za wino wa rangi
- Vifaa vya kuchora vyenye karatasi ya rangi, magazeti, matawi, mchele, maharage, mahindi, majani ya miti na ganda la konokono.
- Gundi

- Picha za kijiji unachoishi ambazo zilipigwa zaidi ya miaka 10 iliyopita

Utangulizi:

1. Zungumzia juu ya mabadiliko ya wakati. Waombe washiriki wafikirie huko nyuma wakati walipokuwa bado wadogo, nyumba ya wazazi wao na kijiji chao vilifananaje na mabadiliko yaliyopo hivi sasa. Je, vyumba katika kituo cha mafunzo vimetengenezwa au vimepata vifaa vipya? Kuna nyumba mpya zilizojengwa hapo? Kwa nini vitu vimebadilika na nani ameamua kufanya mabadiliko hayo?
2. Uliza maswali ya haraka, ni yapi yangefanyika kama vikundi vingeulizwa?
3. Baadaye zungumzia uhusiano uliopo baina ya uamuzi ufanywao na watu wengine na Haki za Binadamu. Je, Haki za Binadamu ni mwelekeo ulio mzuri kutoa uamuzi wako juu ya jambo fulani? Je, Haki za Binadamu zitasaidia hapo baadaye au hapana? Kwa nini?
4. Wape moyo washiriki ili watumie zoezi hili kufikiria maisha yao ya baadaye yanavyoweza kuathirika kutokana na yale wayatendayo.
5. Gawa vikundi vyenye washiriki watatu mpaka wanne.
6. Gawa karatasi na kalamu na watake wafikirie jinsi makazi yao kijijini au mjini yanavyoweza kufanana hapo baadaye. Kikomo chake hakina mwisho, bali kitategemea fikra zao.
7. Mara kikundi kitakapojadili na kubuni ni kitu gani wafanye, basi waanze kuhamisha mawazo yao na kuchora kwenye karatasi kubwa kwa kutumia rangi.
8. Baada ya kumaliza kazi hiyo kila kundi litaonyesha kazi yake na kueleza walipata wapi mawazo hayo. Baada ya kila onyesho toa muda wa kuuliza maswali , lakini mjadala mzima utafanyika mwishoni kwenye maandalizi ya mwisho na tathmini.

Maandalizi ya mwisho na Tathmini

Hakikisha ni vipi washiriki kwenye vikundi vyao walivyofanya kazi pamoja, walivyofikia uamuzi na jinsi walivyoendesha shughuli nzima.

- Je, wote wameweza kutoa mchango wao kama inavyostahili? Je, vikundi vidogo vimetumia vipi vipaji vya pekee vya washiriki wake?
- Ilikuwaje kutoa maoni yako mwenyewe?
- Je, ilikuwaje kutoa maoni yako juu ya kazi za wengine?
- Je, ungeweza kubadili mawazo yako kama ungefanyakazi moja tu na kundi zima ili kutimiza matakwa na haja za wenzako?
- Vipi umefurahia kazi yako kwa kuwa „Mbunifu wa maisha yako ya baadaye“?
- Je, unadhani mawazo yako hayo yanaweza siku moja kutimia? Kwa nini?
- Je, unadhani watu wazima wangekuwa tayari kusikiliza mawazo yako hayo? Kwa nini?
- Ni lipi limekushangaza katika mipango yako hiyo?

- Ni haki zipi zingekustahili kama mwananchi wakati huo wa baadaye?
- Ni wajibu gani ungekuwa nao wewe kama mwananchi hapo baadaye?
- Je, vijana wanaweza kufanya kitu gani ili kuimarisha na kuendeleza demokrasia kwa maisha yao ya baadaye?

Maoni kwa kiongozi wa mjadala

Kichwa cha habari cha zoezi hili kinaitwa „Maisha yetu ya Baadaye“. Maisha yetu ya baadaye hayakutayarishwa yabakie hivyo yalivyo, bali yanaweza kubadilishwa na sisi wenyewe. Kwa hiyo kuna uwezekano mkubwa wa kuleta mabadiliko hayo na ni wajibu wa vijana kujenga maisha yao ya baadaye wanayoyataka. Ili kuyafanya mabadiliko haya yatokee unaweza kuonyesha picha za sehemu yako ilivyokuwa miaka kumi au ishirini iliyopita. Unaweza kuuliza pia juu ya mabadiliko ya kimataifa. Washiriki wanaweza pia kufikiria jinsi mtandao ulivyokuwa kama muujiza miaka thelathini iliyopita. Hivi sasa mitandao imeenea karibu kila mahali, mashuleni, kwenye maktaba, n.k.

Tarehe muhimu:

12. August Siku ya Kimataifa ya Vijana

Ikiwa washiriki hawajui ni vipi makazi yao ya hapo baadaye yatafanana, unaweza kuwauliza maswali yafuatayo:

- Nani ataishi huko?Watu waliozaliwa hapa au wageni? Watakuwa na umri gani? Je, watakuwa na familia?
- Maisha ya kila siku yanafananaje? Je, utanunua mahitaji yako pale dukani? Je, utatembelea sehemu gani?
- Je, utahitaji huduma gani ya afya (Zahanati, Mganga wa meno, n.k)?
- Je, shule yako itafanana vipi?
- Je, utayaendesha vipi maisha yako ya kijamii? Utafanya nini kwenye wakati wako wa starehe?
- Ni mifugo ipi ya wanyama utakuwa nayo nyumbani?
- Kazi yako itafanana vipi?
- Ni maendeleo yapi ya teknolojia yatakuwepo?
- Mazingara yatafananaje?

Njia nyingine:

Njia nyingine unaweza kutumia “*magurudumu ya baadaye*”. Washiriki watafanya kazi kwenye vikundi vyao vidogo. Kila kundi litachagua mada yake (k.m. Elimu, Familia, Kijiji, Kazi au Afya) na kuchora mduara wa baadaye. Mduara wa mazingira kwa mfano ungekuwa na vitu muhimu katikati na pia mduara mwingine unaogawanya mduara huo katika sehemu

mbalimbali ambapo unaweza kujaza vitu kadhaa, k.m. sehemu ya kutovuta sigara, miti mingi, mto msafi, ufugaji mzuri.

Mapendekezo ya kazi ya baadaye:

Fanya uchunguzi juu ya mipango ya mendeleo na uwezekano wa kushawishi watu. Jihusishe kwenye masuala ya kutoa uamuzi shuleni, kwenye klabu yako ya michezo au kwenye shirika lako kwa kushiriki katika baraza la ushauri au kugombea nafasi ya uongozi ili uweze kuchaguliwa kushika wadhifa wowote ule. Unaweza kufanya mazoezi mengine yanayohusu maisha ya baadaye. Zoezi liitwalo "Njia hii ya nchi ya usawa inakwenda wapi", linajishughulisha na masula ya usawa wa jinsia na "athari za mtandao". Pia linahusu matukio ya baadaye ya teknolojia mpya.

Wakati tunafikiria maisha ya baadaye, tunaweza kuanza kujenga jamii itakayokuwa na usawa. Ikiwa vikundi vitaamua mada ihusuyo uonevu na uelewano na jinsi ya kuheshimiana, basi vinaweza kuendelea na zoezi liitwalo " Je, inawezekana njia nyingine"?

Mawazo ya Utendaji

Onyesha mpango wako kwenye Baraza la kijiji, yaani uongozi wa Kata na kujaribu kuwahusisha viongozi wake. Mpango wako unaweza kujadiliwa kwenye mpango wa maendeleo ya Kijiji au wa Kata.

MIMI NI NANI?

Mimi ni mimi, wewe ni wewe, na yeye ni yeye….,lakini sote tuna uhusiano wa pamoja

Mada: Usawa wa jinsia

Utata: Hatua ya 2

Ukubwa wa kundi: 8+

Muda: dakika 25

Maelezo ya jumla: Zoezi hili linahusu kundi linalonongeneza, maswali ya haraka, majadiliano ya kundi juu ya utambulisho.

Lengo/Shabaha:

- Usawa wa Heshima
- Haki ya kulindwa dhidi ya Ubaguzi
- Haki ya Maisha, Uhuru na Usalama wa binadamu

Lengo:

- Utu na upekee wa binadamu
- Kuangalia ni uhusiano gani tulionao na watu wengine
- Kuleta mshikamano na heshima

Vifaa:

- Kalamu za rangi, kila mtu na rangi tofauti
- Karatasi moja kwa kila mtu
- Bango la karatasi na kalamu ya kuweka alama

Utangulizi:

1. Kwa kuanza washiriki wawiliwawili wananongonezana pamoja. Wajifanye hawajuani na wanajitambulisha kwa mwenzao.
2. Uliza maswali ya haraka yafuatayo: Ni mambo gani ya kupendeza au ya muhimu unapashwa kuyajua unapotambulishana na mtu kwa mara ya kwanza? Nukuu mambo ya muhimu: Jina, umri, jinsia, uraia, ameoa/ameolewa/bado; kabila, kazi/shule, mziki uupendao, aina ya michezo uipendayo, vitu uvipendavyo/usivyovipenda, n.k.
3. Mwishoni washiriki wajaribu kugundua ni vitu gani walivyonavyo wenyewe vinavyofanana na washiriki wengine katika kundi. Gawa kalamu na karatasi. Kazi iliyopo ni kujitambulisha wewe mwenyewe kwa kutumia mchoro. Fikiria kuwa wewe

ni nyota na unaiangazia mwenyewe jamii yako. Washiriki wachague vipengele 8-10 vilivyo muhimu ili kujieleza kwa kuchora.

4. Baadaye pita na kulinganisha nyota yako na ya wengine.Ikiwa utampata mtu aliyechora nyota yake inayofanana na yako, basi andika jina lake. Ikiwa watu wawili watafanana kila mmoja aandike jina lake kwene nyota ya mwingine. Wape muda wa dakika 15 hivi.
5. Kutana pamoja katika mjadala wa pamoja na waulize upekee wa kila mtu ulivyo. Maswali yanaweza kuwa kama haya:
   - Ni vipengele vipivinavyomtambulisha mtu na utu wake (sifa, maslahi yake, n.k.) na vile vinavyofanana na wengine?
   - Ni vipi washiriki wanafanana au kutofautiana?
6. Mwisho uliza maswali ya haraka, ni vipengele vipi vya hiari yako mwenyewe umevichagua na vipi ni vya kuzaliwa. Viandike kwenye sehemu mbili kwenye hilo bango la karatasi.

Maandalizi ya mwisho na Tathmini:

Zungumzia washiriki wamegundua nini juu yao wenyewe na juu ya wengine. Je, haya yanamaani gani kwa haki za Binadamu?

- Kila mmoja ameweza kujifunza nini juu yake mwenyewe? Je, ilikuwa vigumu kujua ni kipengele kipi ni cha muhimu kwako mwenyewe?
- Kulikuwepo na mshangao juu ya kulinganisha nyota zenu? Ni kipi kilikuwa zaidi, fisa zinazofanana au zisizofanana?
- Tofauti zipi zilikuwepo miongoni mwa kundi?Je, hii imeleta kuelewana katika kundi au imefanya kazi ya pamoja iwe ngumu?
- Kulikuwepo kipengele ambacho kilimfanya mtu kusema kwa sauti „Hapana, siyo mimi“? K.m. hapana, mimi si mcheza mpira; mimi siyo mwana muziki; n.k.
- Ni vipengele vipi vinamtambulisha mtu na utu wake? Ni vipi vinasababishwa na mazingara ya kijamii na ni vipi vya kuzaliwa navyo visivyoweza kubadilika?
- Ni vipengele vipi vinahusiana na jinsia katika jamii na vipi nivya kuzaliwa navyo na haviwezi kubadilishwa? Kuna aliyeandika neno „Mvulana au Msichana“? Neno Mvulana au msichana linahusishwa na nini? Je, uhusiano huu wa jinsia zote mbiliunalingana baina ya wavulana na wasichana?
- Je, mtu anahukumiwa kufuatana na utu wake au kundi lake?
- Je, washiriki wanaonajekuwa na uhuru wa kuwa hivyo ulivyo na upendavyo? Hii ina maana gani kwako wewe binafsi na kwa jamii yako na hasa juu ya Haki za Binadamu za usawa na heshima?

Maoni kwa kiongozi wa mjadala

Kichwa cha zoezi hili siyo kwamba kuna kosa! Ni kutaka tu kuwatatanisha.

Wakati wa maoezi ya mwanzo unaweza kuwapa dokezo ili kuwaongoza inavyokusudiwa. Chukua mfano wako mwenyewe au mtu yeyote unayemfikiria:

Mfugaji hodari, Karagwe, Mkulima hodari, Mkufunzi, Mwana muziki, Msafiri, Mcheza mpira, Daktari, n.k.



Wape washiriki rangi mbalimbali na kuwaeleza kuwa kila mtu aliyetajwa hapo juu ni yeye pekee na kundi litengeneze mfano wa „Upinde wa Mvua“. (Huuni kama mfano wa Afrika Kusini, inayojulikana kama Taifa la „Upinde wa Mvua“, ambapo wenyeji wake ni watu wa rangi mbalimbali). Ikiwa washiriki wa vikundi watatumia rangi mbili au tatu zinazofanana, basi watake watumie maandishi tofauti. Unaweza kufanya zoezi hili likawa jepesi, ambapo nyota zitakuwa na urefu tofauti kutegemea ni vipengele vipi vimechaguliwa.

Mwishoni mwa maswali ya haraka, unaweza kutumia hoja zifuatazo:

- Kipengele cha Utambulisho, ambapo mtu anajichagulia kwa hiari yake: jina, rafiki, kazi, uanachama katika chama cha siasa, muziki aupendao, mavazi, klabu ya mpira aipendayo, kijiji anakoishi.
- Kipengele cha utambulisho, kwa kuzaliwa: jinsia, umri, ukubwa, rangi ya macho.
- Baadhi ya vipengele vinaweza kuleta utata, kwa mfano uraia, majukumu kutegemea jinsia, dini, kabila lako (kama ni dogo), au taifa lako, n.k.

Mjadala kuhusu utambulisho na vipengele ambavyo vinahusu jamii, vikiwa vya kuzaliwa na hivyo kutoweza kubadilika, vinaleta utata, hasa vikigusa imani ya dini, au majukumu ya

kijinsia. Waulize washiriki walivyokua tangu utotoni na ni vipengele vipi vimebadilisha utambulisho wao tangu miaka yote hiyo, na ni vipi ambavyo unadhani haviwezi kubadilika. Kutokana na mjadala huu ni wazi kuwa binadamu wote wanastahili haki bila kujali kabila lao, uraia, rangi ya ngozi, mafanikio yao maishani, kuzaliwa kwao au sifa yoyote ile.

Mapendekezo ya kazi ya baadaye:

Kutokana na zoezi hili panatokea mijadala mbalimbali. Haki za Binadamu ni za kila mtu na kila mahali, ubaguzi na uadui dhidi ya wageni, haki za watoto na kushiriki kisiasa.

Ikiwa washiriki watapenda kuendelea na mada ya Utambulisho na masuala ya jinsia , unaweza kufanya zoezi la “Mashujaa“ ukurasa wa 164.

JE NCHI YA USAWA INAELEKEA WAPI?

„Kikwazo ni njia“ - maneno ya hekima ya Zen

Mada: Usawa wa kijinsia, Ubaguzi na uadui dhidi ya wageni, Elimu

Utata: hatua ya 3

Ukubwa wa kundi: 4+

Muda: dakika 90

Maelezo ya jumla: Zoezi hili linahitaji vikundi vidogo na mawazo ya ubunifu,washiriki wanatumia michoro kuelezea Usawa wa kijinsia na Ubaguzi dhidi ya wanawake.

Lengo/shabaha:

- Uhuru wa kujikwamua tokakwenye ubaguzi wa kijinsia
- Haki ya kuoa kwa hiari yako mwenyewe kwa kujichagulia mme au mke umpendaye
- Haki ya ulinzi wa mzazi kabla na baada ya kujifungua mtoto

Lengo:

- Kukuza uelewano na makubaliano juu ya malengo ya usawa wa kijinsia
- Mawazo ya ubunifu juu ya fikra za maisha ya baadaye
- Kukuza Haki na Heshima

Vifaa:

- Karatasi (DIN A4) na kalamu kwa kila kikundi kwa kazi za haraka
- Karatasi iliyojipinda (A3) au bango la karatasi kwa kila kikundi
- Kalamu za rangi za kuchora kwa vikundi vidogo
- Ramani ya jimbo lako au kijiji chako inayoonyesha mito, milima, daraja, n.k.

Matayarisho:

1. Angalia vizuri hiyo ramani na kutafakari vitu vyote vilivyomo.

Utangulizi:

1. Kwenye zoezi hili washiriki watachora kwa kuwazia tu njia ya kuelekea nchi ya Usawa, ambako kuna usawa kati ya jinsia. Nchi hii ipo tu kimawazo.
2. Waulize washiriki kama wanajua hadithi ambayo maadili yanafundishwa kupitia kwenye lugha yao.
3. Angalia kwa uangalifu ramani hiyo. Onyesha jinsi mipaka ilivyochorwa, milima na mito, misitu na nyumba vilivyosimama.
4. Vikundi vya watu 3-5 vitundwa. Wagawie karatasi na kalamu na wape dakika 15 kwa maswali ya haraka kwa maswali yafuatayo:
    - Tunafikiriaje nchi ya usawa ilivyo?
    - Ni matatizo yapi tunakumbana nayo njiani kuelekea nchi hiyo ya Usawa?
    - Tunawezeje kupambana na matatizo haya?
5. Sasa gawa karatasi iliyojipinda (A3) na kalamu za rangi. Kila kundi lichore mandhari ya nchi ya usawa ilivyo hivi sasa na itakavyokuwa hapo baadaye na kuonyesha njia inayounganisha pampoja nchi hizo. Fikiria mwenyewe mandhari ya mazingira, vizuizi na vifaa vya teknolojia kandokando ya njia hiyo.
6. Vipe vikundi muda wa dakika 40 ili kuchora ramani zao. Waonyeshe mambo yote ya kusifika kwenye ramani zao.
7. Mwishoni wawasilishe ramani zao katika maongezi ya mwisho ya pamoja.

Maandalizi ya mwisho na Tathmini:

Zungumza kwanza juu ya kufanya kazi kwa pamoja. Jinsi ramani itakavyochorwa, jinsi nchi ya Usawaitakavyofanana na jinsi vikwazo vya kufika huko vitakavyoweza kutatuliwa.

- Je, zoezi limependeza? Kwa nini?
- Kati ya maswali hayo matatu ya haraka, ni lipi lilikuwa gumu na kwa nini?
  Ni lipi lilikuwa rahisi na kwa nini?
- Ni alama gani zinaitambulisha nchi hiyo ya Usawa?
- Ni vitu gani vinazuia jamii ya sasa kuwa kama nchi ya Usawa?
- Je, ni vitu gani vinabidi kubadilishwa kama tunataka kujenga jamii yenye usawa wa kijinsia?
- Kama ungelinganisha nchi yako na nchi nyingine duniani kuhusu suala la usawa wa jinsia kati ya wanaume na wanawake na kutoa maoni yako kwa maksi kuanzia 1 (nzuri sana) hadi 10 (bado kukamilika), je ungeipa nchi yako alama gani?
- Ni kundi gani linabaguliwa katika jamii yako? Ubaguzi huo ukoje? Ni haki zipi za Binadamu zinavunjwa?
- Ni vipi unaweza kusaidia vikundi vinavyobaguliwa kwa kuvipa „Uwezo“ ili viweze kudai haki zake?
- Elimu inasaidia vipi katika uwanja huu?

Maoni kwa kiongozi wa mjadala

Ikiwa washiriki watakuwa na matatizo ya kueleza mawazo yao kwa kutumia michoro, unaweza kuwapa mfano:

- mwanamke anajenga daraja la elimu ili kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake kwenye taasisi ya mahakama.
- Mwanamme anafurahia kazi yake kama mwalimu wa shule ya chekechea.

Inabidi ufikirie mifano mbalimbali iliyoko kwenye jamii yako inayoonyesha ubaguzi wa kijinsia.

Tarehe muhimu

(25. November – Siku ya Kimataifa ya kuondoa unayanyasaji dhidi ya wanawake)

Njia nyingine: Vikundi vinaweza kutumia takataka za kutupwa ili kujenga mfano wa mazingira ya nchi hiyo ya Usawa. Hivyo unahitaji vifaa vidogo vidogo vinavyopatikana kwenye sehemu yako, kama vile nyasi, majani ya miti, kamba, nyuzi, udongo, n.k.

Mfano wa ramani ya mji wenye njia toka hali ya sasa kuelekea mji wa maisha ya baadaye unaweza kutumika bila shida yoyote katika mazoezi mbalimbali kwa kutumia fikra zako na kutafuta njia ya kutatua matatizo yaliyopo.

Mapendekezo ya kazi ya baadaye

Chunguza zaidi mada hiyo na majukumu ya kijinsia au maswali mengine yaliyoulizwa. Unaweza kutafuta habari toka sehemu mbalimbali kama vile maktaba ya hapo shuleni, kwenye vitabu, mtandao au kumwuliza mtu anayehusika na suala hili toka taasisi mbalimbali zinazoshughulikia masuala ya usawa katika jamii yako.

Mawazo ya Utendaji

Angalia kisiasa hapo shuleni kwako kwenye klabu yako au mahali pako kazini jinsi usawa wa kijinsia unavyotendeka. Jadili ni vipi masuala haya yanaweza kutimizwa kisiasa, ni mambo gani yafanyike ili kuleta mabadiliko haya na kuzibadili taasisi hizo kwenye nchi hiyo ya Usawa?

Habari zaidi:

Mpango huu katika zoezi hili unaitwa „Uwezo“ au „Uwezeshaji“. Hii ndiyo njia au matokeo ya Elimu, iitwayo „Elimu ya Ukombozi“.

Tafsiri inayopatikana kwenye Shirika la „Oxfam“ inasema hivi:

„Uwezo au Uwezeshaji ni mapigano dhidi ya Unyanyasaji wa mamillioni ya watu, ambao katika jamii zao wamefungiwa njia zote kwa kugandamizwa na kunyimwa Haki za Binadamu“

(Oxfam: www.oxfam.org.uk)

UPATIKANAJI WA DAWA

"Jitihada za raia wenye wasiwasi duniani zinaweza kuleta mabadiliko" (*Zackle Achmat, kampain ya mpango wa matibabu*)

Mada: Afya, Utandawazi (kimataifa), Ubaguzi na Chuki dhidi ya wageni

Utata: hatua ya 4

Ukubwa wa kundi: 16-40

Muda: dakika 190

Maelezo ya jumla: Zoezi hili linafanana na mchakato wa kisheria dhidi ya kampuni ya madawa huko Afrika Kusini mwaka 2001. Inahusu:

- Ukimwi (HIV/AIDS) na upatikanaji wa dawa
- Kusawazisha matakwa yenye utata

Lengo/Shabaha:

- Haki ya maisha na heshima
- Haki juu ya mali

Lengo:

- Kufahamu utata uliopo juu ya Haki za BInadamu
- Njia tofauti za kutafuta na kulinganisha uamuzi(zinazopingana na zenye makubaliano)
- Kujifunza Mawasiliano na kufanya kazi kwa pamoja

Vifaa:

- Bango la karatasi na kalamu
- Kila mshiriki apewe nakala ya maelezo kwenye kundi dogo
- Kila mshiriki apewekadi moja nyekundu na kijani (10 x6cm)
- Nafasi ya kutosha kwa mjadala wa pamoja na vikundi vidogo

Utangulizi: Zoezi hili lina sehemu mbili

1. Sehemu ya kwanza ni mashtaka ya kesi
2. Sehemu ya pili ni kutafuta suluhisho au makubaliano

Sehemu ya kwanza: Mashtaka (dakika 65)

1. Elezea kiini cha tatizo hili: HIV/AIDS ni janga kubwa lililoikumba dunia yote, na hasa Kusini mwa Afrika limeenea sana. Mamillioni ya watu Afrika Kusini wanateseka na kufa, kwa sababu hawawezi kumudu gharama kubwa za madawa haya. Dawa zilizo nafuu kama (Generika), ndiyo njia pekee ya kuokoa watu. Lakini mashirika makubwa hayataki! Mashirika hayo yanataka kulinda umiliki wake wa kibiashara na yamejiunga pamoja kuhakikisha kwamba hakuna nchi itakayonakili bidhaa zake na kuziuza kwa bei nafuu. Mashirika haya yameishtaki serikali ya Afrika Kusini kwa kugawa na kuuza madawa haya kwa bei nafuu!!!
2. Washiriki waigize mashtaka ya kesi hii ambayo ilifanyika huko Afrika Kusini mwaka 2001. Swali ni: Je, hiyo hoja ya kumiliki bidhaa inashinda haki ya kulinda maisha ya binadamu na heshima yake?
3. Washiriki waunde makundi 4 yanayolingana: Kampuni ya madawa ya Pharma AG, Serikali ya Afrika Kusini, Kampain ya mpango wa matibabu TAC, na Mahakimu.
4. Kila kundi lipe majukumu yake
5. Vipe vikundi muda wa dakika 25 ili kusoma majukumu yaliyoandikwa kwenye kadi ili kutayarisha hoja zao na mwaswali yatakayoulizwa kwenye kesi hii. Kila kundi lichague mwakilishi wake atakayewakilisha kundi hilo na mashahidi wawili watakaosaidia kujibu maswali mahakamani.
6. Baada ya vikundi kuwa tayari, wote watajikusanya pamoja lakini wakibaki pamoja kwenye vikundi vyao hivyo vinne.
7. Sasa Kampuni ya madawa Pharma AG, Serikali ya Afrika Kusini na Kampain ya mpango wa matibabu TAC, kila mmoja atapewa muda wa dakika 5 kutoa hoja zake na kuuliza maswali. Mahakimuwatatambulisha kila kikundi.
8. Sasa Hakimu au mahakimu watakuwa na muda wa dakika 10 ili kujibu maswali toka kwenye vikundi na kutoa mukhtasari wa hoja zilizoongelewa.

Sehemu ya pili: Kutafuta suluhisho au makubaliano (muda wa dakika 100)

1. Hapa pia vitaundwa vikundi vinne. Kila kundi kitakuwa na mwakilishi wa zamani wa Kampuni ya madawa ya Pharma AG, Serikali ya Afrika Kusini, Kampain ya mpango wa matibabu TAC, na Mahakimu.
2. Wape maelezo juu ya kazi za kila kundi. Hakikisha wameelewa wajibu wao na jinsi ya kutumia kadi nyekundu na kadi ya kijani. Vikundi vitapewa muda wa dakika 30 ili kujaribu kutafuta suluhisho au makubaliano na madai ya upande mwingine ili kutafuta jawabu.
3. Baadaye waite wote kwenye mazungumzo ya pamoja ili kusikiliza matokeo ya pamoja. Kila kundi litapewa dakika 5 kutoa maelezo yao. Andika mapendekezo ya ufumbuzi na maswali kwenye bango la karatasi.
4. Baada ya maelezo ya kila kundi na kusikia msimamo wao, jadili juu ya mashtaka na uamuzi uliotolewa. Maswali yafuatayo yanaweza kuulizwa:
   - Je, ilikuwa vigumu kupata mwafaka?
   - Je, ni wapi kuna urahisi au ugumu wa kuendesha mashtaka haya?

- Je, ilikuwa vigumu kupata mwafaka wa pamoja na upande mwingine kuwashirikisha wahusika wote ili kutoa mawazo yao?
- Ni suala gani lilikuwa ni tatizo kubwa sana?

Maandalizi ya mwisho na Tathmini:

Tathmini imeanza tayari katika sehemu ya pili ya majadiliano haya. Wahamasishe washiriki wafikirie ni haki zipi za Binadamu zimechukua nafasi ya muhimu katika mashataka haya. Maswali yafuatayo yanaweza kuulizwa:

- Je, kuna mtu yeyote aliyewahi kusikia mashataka kama haya?
- Ni mawazo gani yalikuwepo hapo mwanzo?
- Je, mawazo haya yamebadilika baada ya kufanya zoezi hili?
- Je, ni vipi sehemu hizi mbili za kukubali au kupinga suala hili zinaweza kulingnishwa? Ni zipi zinatoa uamuzi wa kuridhisha? Ni vipi unaweza kutafsiri matokeo mazuri?
- Ni Haki zipi za Binadamu zitajadiliwa katika mshataka haya?
- Matatizo haya yanahusina vipi na hali halisi ya kijamii ya washiriki hawa?
- Hii ina maana gani na wakazi wa kijijini mwako?

Maoni kwa kiongozi wa mjadala

Zoezi hili linachukua muda mrefu kwani linahusu masuala magumu na inabidi washiriki wafikirie kwa makini sana. Sehemu hizo mbili si lazima ziendeshwe kwa siku moja mfululizo. Zinaweza kuendeshwa kwa siku mbili.

Kadi nyekundu na ya kijani zinasaidia kurahisisha kujua uamuzi ulivyotolewa na ulivyokataliwa. Washiriki wataonyesha mwishoni mwa majadiliano na mashtaka katika sehemu ya pili kadi nyekundu na kukubaliana kwa uamuzi uliotolewa. Baadhi ya vikundi vinaweza kufikia makubaliano katika sehemu ya pili na vingine vikatofautiana. Katika mjadala washiriki watapewa fursa ya kujua ujasiri na udhaifu kwa uamuzi utakaotolewa. Omba kundi ambalo limefikia uamuzi, siyo tu kutoa uamuzi wao bali pia hoja zao za muhimu, waeleze sababu zilizowafanya waamue hivyo. Kwa lile kundi ambalo halikufikia uamuzi wake, waeleze yale ambayo yamewafanya wasikubaliane.

Dokezo la muhimu: ni muhimu kueleza wazi hali ya wenye ukimwi ilivyo katika jamii yako na kuunganisha shughuli zenu kwa pamoja na wale wenye ukimwi.

Mapendekezo ya kazi ya baadaye

Jadiliana juu ya haki za kuishi kwa heshima katika nchi yako na kuhusu matatizo ya afya.

Tafuta habari kuhusu matatizo ya afya na haki za Binadamu. Soma vitabu na kuangalia kwenye mtandao wa mashirika yafuatayo:

www.aerzte-ohne-grenzen.de

www.tac.org.za

www.medico-international.de

www.who.int

Mawazo ya Utendaji

Chunguza katika sehemu unayoishi ni nani anahusika na masuala ya Afya na uliza ni vipi unaweza kusaidia kama inawezekana.

Kalenda ya Haki za Binadamu

Kalenda ifuatayo ni jaribio la kwanza kufanya maadhimisho ya kukumbuka Haki za binadamu duniani kote. Tarehe hizo zimechaguliwa kutokana na matukio mbalimbali kama siku zinazotambuliwa na Umoja wa Mataifa - UNO, NGO; matukio muhimu ya kihistoria na siku za kuzaliwa watu muhimu waliopigania Haki za Binadamu. Orodha hii haijakamilika wala kuisha na inaweza kusaidia kuhimiza vijana kuendelea na kazi hii muhimu.

Unaweza kutoa nakala ya kalenda na kuitundika ukutani ili kutoa motisha juu ya Haki za Binadamu, kwani inaonyesha masuala mengi toka nyanja mbalimbali. Pengine hii inaweza kusaidia kujiuliza maswali kadhaa na kutafuta sikukuu muhimu za hapo kijijini au za kitaifa. Hizi zinaweza kuongezwa kwenye kalenda hiyo ili kila kundi liwe na kumbukumbu zake walizogundua wenyewe.

Katika sura ya pili zimeonyeshwa tarehe maalumu. Hivyo kalenda hii ni kama chombo cha kufanya maendeleo ya kila mwaka kujikumbusha haki za Binadamu. Kila wiki au kila mwezi kunaweza kufanyika shughuli muhimu. Kwa mfano:

- Tarehe 3. Mai, ambayo ni siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Ulimwenguni, unaweza kufanya zoezi lililopo kwenye ukurasa 220.
- Tarehe 25. November, siku ya kimataifa ya kuondoa Unyanyasaji dhidi ya Wanawake, unaweza kufanya zoezi „mambo ya Ndani“ – ukurasa 167.
- Tarehe 22. April, vikundi vinaweza kujishughulisha vyenyewe kwa kuhudhuria mikutano ya mashirika mbalimbali, kwa mfano siku ya mazingira duniani.

Kwa kuwa Haki za Binadamu zinabadilika kila mara na kila mwaka zinafanyiwa marekebisho, ni vizuri pia kalenda hii kuifanyia marekebisho. Wajibu wenu kama wasomaji wa makala hii ni kujaribu kukumbuka Haki za Binadamu kila mwaka.

Kalenda ya Haki za Binadamu

Tarehe	Maadhimisho	Shughuli
08. Januari	Siku ya Kimataifa ya Kisomo cha Watu Wazima	Elimu kwa Wote
20. Februari	Siku ya Upinzani wa Amani	Kituo cha Nguvu za Umeme
21. Februari	Siku ya Kimataifa ya Lugha ya Mama (UNESCO)	Kikwazo cha lugha
01. March	Siku ya Kimataifa ya kukomesha adhabu ya kifo	Ikiwa itakuja kesho
08.March	Siku ya Kimataifa ya Wanawake	Mashujaa na Mashujaa
21.March	Siku ya Kimataifa ya Mashairi	Mchezo wa picha
21.March	Siku ya Kimataifa ya kukomesha Ubaguzi wa Rangi	Unafanya nini dhidi ya Ubaguzi wa Rangi
22.March	Siku ya Kimataifa ya Maji Duniani	Mtandao wa Maisha
23.March	Siku y Kimataifa ya Hali ya Hewa	
24. March	Siku ya Kimataifa ya Ugonjwa wa Kifua kikuu (WHO)	
07. April	Siku ya Kimataifa ya Afya Duniani (WHO)	Dakika moja tu
08. April	Siku ya Kimataifa ya Kabila la Roma	Hatua moja mbele
22. April	Siku ya Kimataifa ya Mazingira Duniani	Mtandao wa Maisha
23. April	Siku ya Kimataifa ya Vitabu na hati Miliki (UNESCO)	
30. April	Siku ya Kimataifa ya kuteketezwa (Holocaust – Yom Haschoa)	Unafanya nini dhidi ya Ubaguzi wa Rangi

01.Mei	Siku ya Kimataifa ya Wafanyakazi	Mishahara isiyolingana, Muungano wa Wafanyakazi
03. Mei	Siku ya Kimataifa ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Ulimwenguni (UNESCO)	Kichwa cha Habari
08.Mei	Siku ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu na Nusu Mwezi	Bingo ya kulia
15.Mei	Siku ya Kimataifa ya familia	Kazi na Watoto
17. Mei	Siku ya Kimataifa ya Mawasiliano ya simu (ITU)	Athari za Mtandao
22. Mei	Siku ya Kimataifa ya tofauti za Biologia	
31. Mei	Siku ya Kimataifa dhidi ya uvutaji (WHO)	
04.Juni	Siku ya Kimataifa ya Watoto, ambao wanaathirika na mateso	Je, inawezekana njia nyingine?
05. Juni	Siku ya Kimataifa ya Mazingira Duniani (UNEP)	Bistani kwa siku moja
12. Juni	Siku ya Kimataifa dhidi ya ajira ya watoto	Haki za Watoto
15. Juni	Siku ya Kimataifa ya Chakula Duniani	
17. Juni	Siku ya Kimataifa ya kupambana na jangwa na ukame	
20. Juni	Siku ya Kimataifa ya Wakimbizi Duniani	Je, naweza kuingia ndani?
21. Juni	Siku ya Kimataifa ya Amani na Maombi	Wote sawa, wote tofauti
26. Juni	Siku ya Umoja wa Mataifa ya kusaidia waathirika wa mateso	
26. Juni	Siku ya Kimataifa ya Azimio la Umoja wa Mataifa	Kikwazo cha Lugha

Jumamosi ya kwanza Julai	Siku ya Kimataifa ya Vyama ya Ushirika	Cheza pamoja

11. Julai	Siku ya Kimataifa ya Idadi ya watu duniani	
06. Agosti	Siku ya Kimataifa ya Kumbukumbu ya Hiroshima (kukumbuka maafa ya Bomu ya Atomik nchini Japan, 1945)	
07. Agosti	Siku ya Kimataifa ya mageuzi ya jinsia, Haki za Kimataifa na Siku ya Elimu	Mimi ni nani?
09. Agosti	Siku ya Kimataifa ya wenyeji wa asili	Uvuvi wa Nyangumi
12. Agosti	Siku ya Kimataifa ya Vijana Duniani	Maisha yetu ya Baadaye
23. Agosti	Siku ya Kimataifa ya kumbukumbu ya Biashara ya Utumwa na kukomesha biashara hii - (UNESCO)	
Jumanne ya kila mwezi wa September	Siku ya Amani	Bajeti ya mfukoni
08. Septemba	Siku ya Kimataifa ya Kisomo cha Watu Wazima (UNESCO)	Kamusi ya Utandawazi
16. Septemba	Siku ya Kimataifa ya Utunzaji wa Tabaka – Ozoni	

Jumatatu ya Kwanza Oktoba	Siku ya Kimataifa ya Maendeleo ya Makazi (Miji bila makazi duni)	Hadithi ya miji miwili
Jumatano ya pili Oktoba	Siku ya Kimataifa ya kuzuia Maafa duniani	
01.Oktoba	Siku ya Kimataifa ya Wazee	
01.Oktoba	Siku ya Wanamuziki Duniani	
05. Oktoba	Siku ya Kimataifa ya Walimu Duniani (UNESCO)	Kila *sauti*/kura inahesabika
10. Oktoba	Siku ya Kimataifa ya Afya ya kiakili Duniani	Michezo kwa wote
16. Oktoba	Siku ya Kimataifa ya Chakula (FAO)	
17. Oktoba	Siku ya Kimataifa kuondoa Umaskini Duniani	Kupambana na fedha na nguvu
24. Oktoba	Siku ya Kimataifa juu ya taarifa kuhusu masuala ya Maendeleo	Tahadhari, tunawaangalia!
24. Oktoba	Siku ya Umoja wa Mataifa	Mkakati wa uchaguzi, kupigania Haki za Binadamu
03.Novemba	Siku ya Wanaume Duniani	Mashujaa
09.Novemba	Siku ya Kimataifa dhidi ya ufashisti na Antisemitism	Tunafanya nini dhidi ya Ubaguzi wa rangi?
09. Novemba	Kuanguka kwa Ukuta wa Berlin 1989	Kuanzisha mitandao
11. Novemba	Siku ya Kimataifa ya Sayansi na Amani	

16. Novemba	Siku ya Kimataifa ya kuvumiliana (UNESCO)	Vurugu katika maisha yangu
20. Novemba	Siku ya Watoto Duniani	Haki za Watoto
21. Novemba	Siku ya Luninga Duniani (TV)	Michezo ya Picha
25. Novemba	Siku ya Kimataifa ya kuondoa Unyanyasaji dhidi ya Wanawake	Njia ya kwenda nchi ya Usawa iko wapi?
29. Novemba	Siku ya Kimataifa ya Mshikamano na Taifa la Wapalestine	Wote wanafanana – wote ni tofauti
01.December	Siku ya Ukimwi (AIDS) Duniani – WHO	Upatikanaji wa Dawa
02.December	Siku ya Kimataifa ya kumbukumbu ya Biashara ya Utumwa na kukomesha biashara hii - (UNESCO)	
03.December	Siku ya KImataifa ya Walemavu	Kutambua Vipaji
05. December	Siku ya Kimataifa ya kujitolea kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii	Kuchukua msimamo
10. December	Siku ya Haki za Binadamu	
18.December	Siku ya Kimataifa ya Uhamiaji	Kupiga hatua mbele
Siku ambayo Uhuru wa kupiga kura ilianzishwa nchini mwako		Kupiga Kura au kutopiga Kura
1.Januari	Sikukuu ya Mwaka Mpya	
12. Januari	Sikukuu ya Mapinduzi Zanzibar	
26. April	Sikukuu ya Mwungano wa Tanzania	
01.Mai	Siku ya Kimataifa ya Wafanyakazi	
07.Julai	Sikukuu ya Saba Saba	
08. Agosti	Sikukuu ya Wakulima	

14. Oktoba	Siku ya Mwalimu Nyerere (Mwenge wa Uhuru)	
09. December	Sikukuu ya Uhuru na Jamhuri	

Ufafanuzi wa Mpango wa Utekelezaji

Hatua madhubuti zinahitaji maandalizi mazuri. Washiriki wafikirie kwa makini wanachohitaji na jinsi ya kufikia lengo hilo. Ikiwa watajua wanachotaka kufanya, basi wanaweza kumaliza haraka kazi yao. Kwa malengo makubwa inashauriwa kwanza kutengeneza mpango wa utekelezaji kama hatua ya kwanza. Lile ulifanyalo ni bora kuzaa matunda mazuri.

Jaribu kufuata hatua hizi nne na kundi lako:

1. Chunguza msimamo wako kwanza – Chambua yale ya muhimu
2. Amua ni matatizo gani ungependa kuyatatua na vipi utafikia ufumbuzi wake
3. Fikiria kama uwezo wa kundi au raslimali walizonazo zinatosha
4. Sasa anza kazi

Tumesimama wapi?

SWOT – hii ni njia inayotumika kama chombo cha kupanga mikakati ya maendeleo. Njia hii inaweza kutumika hata nje ya vikundi.

Mfano wa Mkakati huu wa SWOT:

Kundi letu lina nguvu kiasi gani?

- Ni kubwa
- Tunao muda na tunataka kufanya chochote
- Baba yake John ni mwanasiasa
- Mahala pa kukutana ni katikati ya mji/kijiji
- Helena anaweza kuzungumza vizuri mbele ya watu
- Ishengoma anayo radio

Kundi letu lina udhaifu gani?

- Viongozi wengi
- Hatuna fedha yoyote mfukoni
- Wasichana wachache
- Hatujawahi kufanya hivyo
- Wengi wetu wanaishi mbali kutoka shuleni
- Kufanya kazi kwenye kundi hakuendi vizuri

Kuna nafasi gani nje ya kundi?

- Kwenye taarifa ya habari mara nyingi zinatangazwa Haki za Binadamu
- Karibu uchaguzi utafanyika
- Kuna fedha kwa ajili ya kuanzisha mradi wowote na wakimbizi
- Kwenye kijiji cha jirani kuna kundi la kutetea Haki za Watu
- Ukumbi mpya unafaa kwa michezo ya kuigiza

Ni hatari au matatizo gani yapo kwa kazi yetu?

- Hali ya uchumi ni mbaya sana
- Baadhi yetu tunakabiliwa na mitihani
- Halmashauri ya kijiji inatishia kuzuia mkutano usifanyike
- Kuna chuki kubwa dhidi ya wakimbizi, eti wanachukua kazi za watu wengine
- Nje ni joto sana kuweza kufanya kazi yoyote.

Kifupi cha **SWOT**ni:

Strengths = nguvu: ambapo kundi linajisikia vizuri

Weakness = udhaifu: ambapo kundi halijisikii vizuri

Opportunity = matarajio: uwezekano wa kutumia faida yao nje ya kundi

Threats = Hatari/matatizo: Vipingamizi nje ya kundi, vinavyozuia matarajio yao

Gawa kundi katika vikundi vidogo vinne – nguvu, dhaifu, matarajio na hatari. Waite tena washiriki pamoja na waulize kama wanakubaliana na maoni yaliyotolewa na vikundi vingine.

Maelezo hayo hapo juu ni msaada tu utakaosaidia kupata maoni mengine. Mchoro huo wa SWOT ufanywe na kila kikundi.

Je unapenda kwenda wapi?

Ni tatizo gani ungependa kuliendea? Je, unapenda kuzungumzia juu ya udhalimu au uvunjaji wa Haki za Binadamu kwa ujumla?

Maswali ya haraka na mada ya Haki za Binadamu

Kama mazoezi yaliyotajwa kwenye kitabu hiki yatakuwa yamezungumziwa, kutakuwepo bila shaka na mawazo kadhaa. Kama bado na mmeanza sasa hivi, unaweza kufanya maoni yafuatayo. Toa maelezo kwa kila mada. Mwishoni waanze kufikiria mkutano ujao watakuwa wamefanya utafiti upi, ili baadaye kufanya uamuzi:-

- Hukumu ya kifo nchini mwako
- Ukimwi (AIDS) katika Bara la Afrika
- Kituo cha nguvu za Nyuklia kilichochakaa
- Tabia mbaya dhidi ya wakimbizi
- Ajira za watoto wadogo
- Uhuru wa matangazo katika nchiyako au nchi nyingine
- Haki ya Elimu kwa wachache katika lugha yao ya asili
- Fujo/vurugu za nyumbani

Ni kundi gani linateseka katika nchi yako au hapo kijijini kutokana na kuvunjwa kwa Haki za Binadamu?

Baada ya kuona mada zote na kundi likawa tayari, unaweza wakati wa kuuliza maswali ya haraka kufanya orodha ya mada zinazowagusu sana washirika. Ni vipi zinagusa sana hisia zao?

Jaribu kupunguza mada hizo zifikie kama 3 au 4. Ikiwa washiriki watashindwa kukubaliana, basi wasaidie kutoa uamuzi kwa kupiga kura.

Kuthibiti Malengo

Katika hatua hii ya kuchora „mti wa matatizo“ kwa mada iliyochaguliwa inaweza kusaidia sana. Inaweza kusaidia kuweka mkazo kwenye chanzo cha tatizo lako ili kujua sababu zinazotokana na suala hili. Pengine hii itakufanya kuanza kushughulika na tatizo badala ya kuanza na mada yenyewe moja kwa moja.

- Andika kwanza mada mnayotaka kuongelea katikati ya bango la karatasi ya upinde
- Weka sababu zote na ziunganishe na mizizi ya mambo yote muhimu ya awali
- Chukua kila mzizi mmoja na kufikiria chanzo chake. Chora sababu zote unazofikiri zimesababisha tatizo hili. Fuata kila mzizi mpaka ufikie mwisho. Pengine mti una mizizi mirefu kwenda chini zaidi ya ulivyofikiria.
- Pia matawi ya mti huu yanaweza kukua namna hiyo. Ndiyo dalili ya chanzo cha mada hii. Unaweza kugundua sasa kwamba hoja kubwa uliyoanza nayo ni mzizi au tawi la mti huo.
- Utakapokuwa umemaliza angalia tena mti wako. Je, utapenda kuiendea kazi yako kama hapo mwanzoni au bora uanze kutafuta chanzo na sababu? Je, umepata msaada wowote na “mti wa matatizo” kuiendea mada yako?

Je, unafikaje huko?

Kubuni Mkakati

Ukishapata picha kamili ya kundi na likaamua tatizo la kushughulikia, basi utakuwa tayari kwa hatua inayofuata: Fikiria jinsi ya kutatua tatizo hilo.

Yafuatayo ni muhimu kuyafikiria:

1. Tatizo lenyewe unalotaka kulishighulikia: Kimetokea nini kwenye zoezi lililopita?
2. Walengwa: Ni nani umelenga kumzungumzia?
3. Ni mabadiliko yapi ungependa yawafikie walengwa wako: watu wafanye nini kutokana na hatua ulizochukua?
4. Ni vipi mabadiliko haya yatatokea? Unawezaje kushawishi walengwa wako?
5. Ni njia gani zitasababisha mabadiliko haya? Fikiria hatua zilizoelezwa kwenye sehemu ya 1 na fikiria mawazo yako mwenyewe. Ni njia ipi ni bora kuitumia?

Pitia awamu zote za mipango hii (sehemu 2) na kujadili awamu hizo kwenye vikundi. Wanavikundi waafikiane juu ya yaliyomo kwenye mipango hiyo.

Kujipanga binafsi

Mwisho kuna mpango wa utekelezaji wa kufanya, ili kuratibu masuala kadhaa. Kusahau hatua hii kunaweza kusababisha kusahau mambo fulani ya muhimu na hivyo kutotimiza lengo lililokusudiwa.

Maamuzi yafuatayo yanabidi yafikiwe:

- Kuna kazi gani?
- Nani anachukua kazi gani?
- Lini inabidi kufanya kazi hiyo?

1. Andika kila kitu ili uweze kufuatilia ni vipi mambo yanaendelea. Kwa hali hii unahitaji karatasi kubwa mbili za upinde na kalamu
2. Hakikisha kuwa wote wanaelewa ni kitu gani kinaongelewa sasa. Chagua mtu wa kuandika mukhtasari. Andika kichwa cha habari hapo juu. Andika kazi zote zinazotakiwa kufanyika kwanza kwa maswali ya haraka na andika haya kwenye hilo bango la karatasi ili yaonekane kwa kila mtu.
3. Ikiwa utatayarisha mkutano, fikiria dhana zote toka mwanzo hadi mwisho. Hakikisha una kila kitu kinachohitajika ili usiweze kusahau chochote.
4. Wape sasa orodha na amua ni kazi gani ifanyike na muda gani; sasa au baadaye. Weka alama kwa kila swali kwa kutumia alama yoyote, kama J, B, au S.
5. Bango la pili la karatasi litumike kama „karatasi ya uamuzi“. Orodhesha kazi zote kwenye mstari unaofuatana, kwa kuandika upande wa kushoto nini kinatakiwa kufanyika na upande wa katikati ni nani anatakiwa kufanya kazi hiyo. Katika upande wa kulia onyesha muda, ni lini watamaliza kazi hiyo.

6. Gawa kazi hiyo kwa usawa unaolingana. Usiwaachie watu wawili au watatu peke yao. Fikiria itakuwaje kama mmoja ameugua, au mwingine akawa na kazi nyingi za kufanya na asiwe na muda!

Mfano ufuatao unaonyesha jinsi karatasi ya uamuzi inavyoweza kufafanana:

Karatasi ya Uamuzi

Mkutano: Hatua za Mitaani kuhusu Haki za wachache		
Kazi ya kufanya	**Nani wa kutekeleza**	**Lini kazi imalizike**
Kubuni vipeperushi	Ali, Juma, Ishengo,Kato	Kukutana tarehe 10. Sept. na 17. September
Kupanga kutolewa/kuchapishwa	Dar es Salaam, Dodoma	Baada ya tarehe 20.Sept.
Kutengeneza bango na kulitundika	Wote	Kwenye wiki kuanzia tarehe 24. September
Kununua vifaa vya kutundika	Ibrahim, Kintu, Yohana	Kwenye wiki kuanzia tarehe 17.
Watu wengine wanaopendezwa	Amina. Fatuma	Kwenye wiki kuanzia tarehe 17.
Ongea na Halmashauri ya kijiji	Mkiza, John, Wamara	Tarehe ya Mwaliko ikisha kujulikana
Kutoa taarifa kwa Polisi	Mkiza, John, Wamara	
Watu mashuhuri wajulishwe		
Vikundi vya wachache vitaarifiwe		
Kuandika Hotuba		
Baada ya hapo fanya usafi		

Ni mpango upi unataka kuanza?
Haki ya kutolazimishwa*
kupewa mateso*
Kwamba....baadhi ya mateka....*
Kabila la wachache linabaguliwa*
Fulani Y ni kiongozi mbaya*
Serikali inafanya biashara na silaha za kuteketeza binadamu*
Ni mabadiliko yapi mnapenda yafikiwe?
Mabadiliko ya fikra kwa walengwa*
Mabadiliko ya maoni ya Umma*
Kupata ujuzi mpya*
Kuwashirikisha watu wengine*
Kutangaza kwenye vyombo vya Habari*
Kutunga sheria mpya*
Kumchagua mshauri*
Kusahihisha Udhalimu*
Mjadala juu ya Mada hii*
Ni nai walengwa wa kundi lako
* Vijana
*Wakazi wa sehemu hiyo
*Akina Mama
*Wanasiasa
*Wafanya biashara
*Jumuiya ya Kimataifa
Ni njia gani utazitumia kwenye walengwa wako?
Taarifa kwa vyombo vya habari*
Mtandao (Internet)*
Kampeni na mikutano ya hadhara*
Sanduku la barua, Vipeperushi, Mabango*
Matangazo au Taarifa*
Makala, Takwimu*
Maandamano barabarani*
Mafunzo, Mjadala*
Semina/Warsha*
Barua kwa Serikali*
Ni vipi Mabadiliko hayo yatafanyika?
*Kupitia njia ya kushawishi/kutoa hoja
*Kuwatishia watu: kuwafanya wawe na woga ili wafanye hiyo utakayo
*Kupitia njia za kisheria
*Uchaguzi
*Kutoa tahadhari
Kuwapa watu uwezo wa kujiamulia watakayo
*Taarifa kuhusu masuala muhimu
*Shinikizo toka kwa umma
*Shinikizo toka Jum,uiya ya Kimataifa

Viungo mbalimbali kwenye Mtandao kuhusu Elimu ya Haki za Binadamu

Mashirika ya Ujerumani na Mipango

Shirika la Elimu ya Siasa kwaUraia	www.bpb.de
D@dalos	www.dadalos.de
Server a Elimu ya Ujerumani	www.bildungsserver.de
Taasisi ya Ujrumani ya Haki za Binadamu	www.institut-fuer-menschenrechte.de
Kituo cha Mafunzo ya Ulaya na Utafiti kwa Haki za Binadamu na Demokrasia (ETC)	www.etc-graz.de
Jukwaa la Habari la Haki za Binadamu Uswiz MERS	www.humanrights.ch
Taasisi ya Haki za Binadamu-Ludwig Boltzmann Wien	www.univie.ac.at/bim
Haki za Binadamu Shuleni	www.menschenrechte-in-der-schule.de
Sehemu ya Uratibu ya Haki za za Binadamu - Amnastey International	www.amnesty.de/de/2910
Shirika la Huduma za Haki za Binadamu Austria	www.humanrights.de
UNESCO – Chuo Kikuu cha Otto-von-Guericke, Magdeburg Ujerumani	www.menschenrechtserziehung.de
Mradi wa UNESCO Shuleni	www.unesco.de www.unesco.arbeitsgebiet/ups
Wikipedia – On-line-Encyklopidia	www.wikipedia.org
WUS – World University Service	www.wusgermany.de

Viungo mbalimbali kwenye Mtandao kuhusu Elimu ya Haki za Binadamu

Mashirika ya Kimataifa na Mipango

Maktaba ya Chuo Kikuu cha Minnesota	www.umn.edu/humanrts
Kamishna Kuu ya Haki za Binadamu – UNO	http://193.194.138.190 /education/main.htm
Human Rights Education Associates	http://www.hrea.org/
Haki ya Elimu	http://www.right-to-education.org/
Mashirika ya Kimataifa na Kimkoa ya Elimu ya Haki za Binadamu	http://www.unhchr.ch/hredu.nsf
The People`s Movement for Human Rights Leraning (PDHRE)	http://www.pdhre.org/materials
Shahada ya Masters, Haki za Binadamu na Demokrasia, Venedig, Italia	http://www.uv.ruhr-uni-bochum.de